JACKPOT BABA LAO!
TZS. 374,935,160
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 2

**‘KIUNDWE** kitengo maalum uchunguzi rushwa ya ngono’




UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumatatu Oktoba 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581101
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Rais Samia: Punguzeni kasi kuzaa

**KITUO** cha afya kina vizazi 1,000 kwa mwezi... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Nyakanazi mkoani Kagera wakati akielekea mkoani Kigoma jana. **PICHA: IKULU**

## CRDB YATAJWA BENKI BORA TANZANIA KWA MARA YA NNE

UKURASA 3



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kushoto) na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki hiyo, Tully Mwambapa wakionyesha cheti cha tuzo ya ‘Benki Bora Tanzania’ walichokabidhiwa na Joseph Giarraputo, Mwanzilishi na Mhariri Mtendaji wa Global Finance (wa pili kulia) katika hafla ya kukabidhi tuzo kwa Benki Bora Duniani jijini Washington D.C, Marekani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Museveni aweka karantini wilaya mbili kukabili Ebola

UKURASA 2

UKURASA WA 8

### MA-RC NA MA-DC WAONYWA KUINGILIA UTENDAJI WA MAHAKAMA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani, amewaonya wakuu wa mikoa, wilaya na viongozi wengine wa umma kuingilia...

UKURASA WA 25

### WALIMU 14 MBARONI TUHUMA UDANGANYIFU MTIHANI LA VII

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia walimu 14 kwa tuhuma za kukiuka sheria, kanuni na taratibu za mtihani wa darasa...

## Mashine zazimwa kwa siku 1,000 hujuma mapato ya halmashauri

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA YATINGA MAKUNDI AFRIKA UK. 32
KATUNI UK. 6

# Samia: Punguzeni kasi ya kuzaliana

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka wananchi kupunguza kasi ya kuzaa ili huduma za kijamii na fursa za maendeleo zilizoko zitosheleze katika kuboresha maisha ya kila Mtanzania.

Akihutubia mamia ya wananchi katika Kata ya Runzewe wilayani Bukombe mkoani Geita jana wakati akihitimisha ziara yake ya kikazi iliyoanzia mikoa ya Kagera na baadaye kuijumuisha Kigoma na Geita, Rais Samia alisema jana kuwa serikali inaboresha huduma za kijamii ili kila mtu anufaike nazo.

Kauli ya Rais ilikuja baada ya Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka kuwataka wananchi wa eneo hilo kuendelea kuzaa kwa kuwa huduma za kijamii zinaendelea kuboreshwa.

"Sasa mnataka nini? Zaeni tu mama yupo, madarasa yanajengwa, zaeni tu vituo vya afya vinajengwa, zaeni tu mama amefungua fursa, wawekezaji wanakuja," alisema Shaka.

Baada ya Shaka kumaliza kuzungumza, Rais Samia alisema: "Mheshimiwa hilo la zaeni tu hapana bwana, jana (juzi) nilisimama Buseresere, ninaambiwa kituo kimoja kinazalisha watoto 1,000 kwa mwezi, sasa hapo baada ya miaka mitatu ni madarasa mangapi? Kama ni vituo vya afya vingapi, tani za chakula ni ngapi? Punguzeni kidogo speed (kasi)."

Rais Samia, akiwa mkoani Kigoma, alifungua miradi ya maendeleo ikiwamo Hospitali ya Wilaya ya Kakonko ikigharimu zaidi ya Sh. bilioni 3.5.

Alisema kukamilika kwa hospitali hiyo kutaondoa adha ya wananchi kutembea umbali mrefu, huku akiahidi kuendelea kutoa vifaa tiba na dawa kwa ajili ya matibabu yote muhimu kwa ngazi hiyo.

"Serikali itaendelea kuleta vifaa vya vipimo vyote ambavyo mwanadamu akiumwa anatakiwa kupimwa, tumeona baadhi ya vifaa vipo, lakini bado vingine havipo, serikali italeta vifaa kwa ajili yenu wananchi, ninawataka wananchi kutunza miundombinu hiyo na mingine yote ili iwasaidie kwa muda mrefu," alisema Rais.

Tanzania ina Sera ya Idadi ya Watu iliyoridhiwa na serikali mwaka 1992 kwa lengo la kupunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu (ambalo sasa ni la asilimia 2.7 kwa mwaka) ili kuhakikisha idadi yao inaendana na huduma za jamii zilizoko.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kakonko, Ndaki Stephano alisema hadi sasa mradi huo umetumia zaidi ya Sh. bilioni 2.9.

Alisema halmashauri hiyo ilipokea Sh. milioni 500 za kununua vifaa tiba ambavyo vimeshanunuliwa na kuanza kutumika huku Sh. milioni 57.9 zitumika kulipa fidia wananchi waliopisha mradi huo huo.

Stephano alisema hospitali hiyo ina upungufu wa wafanyakazi 174 kati ya 200 wanaohitajika, huku waliopo ni 22 ambao hawatoshelezi mahitaji ya huduma bora.

Rais Samia, akiwa Nyakanazi, alifungua kituo cha njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 220 wenye urefu wa kilomita 144.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme (TANESCO), Maharage Chande, alimweleza Rais kuwa ujenzi huo utaondoa hasara ya Sh. bilioni 60 kwa mwaka inayotokana na kununua mafuta ya jenereta kwa ajili ya kupata nishati hiyo maeneo ya Biharamulo, Ngara, Loliondo, Kibondo na Kasulu.

Waziri wa Nishati, January Makamba alisema licha ya mkoa huo kuchelewa kupata umeme, itakuwa na kituo kikubwa cha kuzalisha na kusafirisha nishati hiyo kutokana kuna na mradi mwingine wa kujenga kituo cha kuzalisha umeme cha Malagalasi.

Rais pia alifungua barabara ya Nyakanazi-Kabingo yenye urefu wa kilometa 50 iliyogharimu Sh. bilioni 43, ikiiunganisha wilaya hiyo na wilaya jirani na kurahisisha huduma ya usafiri na kukuza biashara kwa wananchi.

***Imeandikwa na Jenifer Gilla (DAR) na Adela Madyane (KIGOMA)**



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Sukari nchini (SBT), Filbert Mponzi (wa pili kulia), na baadhi ya wajumbe wa bodi hiyo wakimsikiliza msimamizi wa kitengo cha umwagiliaji katika kiwanda cha sukari cha TPC kilichoko mkoani Kilimanjaro, baada ya wajumbe hao kutembelea visima vinavyotumika kumwagilia mashamba ya miwa katika kiwanda hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Museveni aweka karantini wilaya mbili kukabili ebola

**KAMPALA,** UGANDA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ametoa amri ya watu kutotoka nje ya nyumba kwa muda wa wiki tatu katika wilaya mbili zilizoathirika zaidi na ugonjwa wa ebola, ili kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo kusambaa zaidi.

Nchi hiyo ilikumbwa na mlipuko wa janga la ebola Septemba 20, mwaka huu, ambapo mpaka sasa taifa hilo limeendelea na jitihada mbalimbali ikiwamo kutoa masharti 21 ili kukabiliana na ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Rais Museveni usiku wa kuamkia jana, zuio hilo la kutokutoka nje ni miongoni mwa masharti 21 ya kukabiliana na mlipuko huo.

Taarifa hiyo ilisema mpaka kufikia juzi, watu 58 walithibitishwa kuambukizwa ebola, 19 wamefariki dunia na 20 wamepona wakiwamo madaktari na wafanyakazi wa sekta ya afya.

Masharti pamoja na zuio litaanza kutekelezwa leo 'jana' katika wilaya za Mubende na Kasanda kulikobainika mgonjwa wa kwanza, pia nyumba zote za ibada zimefungwa pamoja na maeneo ya starehe kama baa, kumbi za disko, vibanda vya filamu na shughuli zote za michezo.

Taarifa hiyo ya Rais Museveni ilibainisha kuwa usafiri binafsi na umma yakiwamo mabasi na pikipiki pia umewekewa zuio la kutotembea usiku kuanzia saa moja jioni hadi saa 12 asubuhi.

Uamuzi huo wa Rais Museveni umetokana na ombi la chama cha madaktari nchini humo la Septemba mwaka huu kutaka kuwekwa karantini wilaya zilizo na maambukizi. **BBC**

# 'Kiundwe kitengo maalumu uchunguzi rushwa ya ngono'

**Na Sabato Kasika**

WADAU wa kutetea haki za wanawake wamependekeza rushwa ya ngono isijumuishwe na rushwa nyingine, badala yake iundiwe kitengo maalumu cha kuichunguza kwa kuwa inatweza utu wa mwanamke.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni mkoani Dar es Salaam, Seleman Bishagazi, alitoa rai hiyo juzi wakati wa mafunzo kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uamuzi na mbinu za kufanya ujasiriamali.

Mafunzo hayo yaliyoanza Agosti mwaka huu, yanaendeshwa na kituo hicho yakihusisha wanawake wa kata za Majohe na Kipunguni kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT) na yanatarajiwa kufikia tamati Desemba mwaka huu.

"Tunaomba uchunguzi wa rushwa ya ngono uundiwe kitengo maalumu chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwani inadhalilisha na kutweza utu wa mwanamke, haifai kuunganishwa na rushwa nyingine," alisema Bishagazi.

Mkurugenzi huyo alisema kumekuwapo visa na mikasa vinavyotolewa na baadhi ya wanawake katika mafunzo hayo kwamba baadhi yao wanakiri walishatoa rushwa ya ngono kutokana na kubanwa na mazingira, hivyo wakaamua 'kujirahisisha' ili kufanikisha kile wanachokihitaji.

"Lakini utoaji wa rushwa hiyo umekuwa ukiibua mijadala, huku sehemu kubwa ikilaumu wanawake bila kufanya uchambuzi wa kina ili kujua chanzo cha kuendelea kuwapo kwa rushwa hiyo," alisema.

Bishagazi alisema rushwa hiyo ikiachwa ichunguzwe na Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU), ipo siku wahusika wataambiwa kuwa mtoa rushwa na mpokea rushwa wote wana hatia bila kujali kwamba kuna upande unatoa rushwa hiyo kwa kulazimishwa.

Alisema ni muhimu kuchunguza na kugundua hao wanaojipeleka au kujidhalilisha lengo lao ni nini hasa. Je, mifumo ya utoaji haki iko sawa? Na kama ingekuwa sawa, hakuna mtu anakubali kujirahisisha.

"Kimsingi, hakuna mwanamke yeyote ambaye yuko tayari kudhalilisha utu wake hivihivi, awe mwanamke mtu mzima au mwanafunzi. Ukweli ni kwamba kuna tatizo kwenye mfumo wa utoaji haki, mtu anaweza asiombe rushwa hiyo, lakini vitendo tu vinaonyesha kuwa anaitaka," alisema.

Mshiriki wa Mafunzo hayo, Livia Mhagama alisema njia itakayosaidia kumaliza rushwa hiyo ni kila kiongozi sehemu yake ya kazi kuzingatia taratibu, kanuni na sheria ili kuziba upenyo wa mtu 'kujirahisisha' kwake ili asaidiwe.

Tausi Shaban, mshiriki mwingine wa mafunzo hayo, alisema mazingira kuanzia kwenye siasa na kwingineko si rafiki kwa wanawake, akidai kuwa wanabaniwa hadi wanafikia kujidhalilisha ili wapate nafasi za uongozi.

Tausi anatoa rai kwamba rushwa hiyo inapaswa kuchunguzwa kwa kina, akitamka: "Inaumiza kuona mwanamke au kusikia mwanamke amepata nafasi ya uongozi kwenye chama baada ya kuombwa rushwa ya ngono na kutoa au amejirahisisha," alisema Tausi.

Mwaka 2019, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu rushwa ya ngono vyuo vikuu, ikibainika kujumuisha mhadhiri kwa mwanafunzi; mhadhiri kwa mhadhiri; mwanafunzi kwa mwanafunzi; na mhadhiri/ofisa utawala chuoni kwa mfanyakazi wa chini chuoni.

Katika uchunguzi wake, Nipashe pia ilipata takwimu kutoka TAKUKURU zilizobainisha kuwa asilimia 18 ya wajasiriamali wanawake wanaouza bidhaa zao kwenye masoko yasiyo rasmi, wamedhalilishwa kwa rushwa ya ngono ili kupata maeneo na uwezesho mwingine wa kuendesha biashara hizo.

HABARI KITAIFA

# Mashine za POS zazimwa kwa siku 1,000 kuhujumu mapato

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imebaini mambo manne katika halmashauri zilizohojiwa kuhusu hoja za ukaguzi za mwaka 2020/21 ikiwamo mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki (POS) kuzimwa na hivyo halmashauri kushindwa kukusanya mapato.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Stanslaus Mabula alibainisha hayo mwishoni mwa wiki baada ya kamati hiyo kukutana na Halmashauri za Wilaya ya Mlele, Kongwa na Kondoa kuhusu yaliyobainishwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21.

Alisema kuna halmashauri mashine za POS zimezimwa kwa takribani siku 1,000, akitahadharisha kuwa kama itaendelea hivyo, kuna mapato mengi yataendelea kupotea na halmashauri hazitafikia malengo zilizojiwekea.

Mabula pia alisema wamebaini halmashauri nyingi zina tatizo la matumizi ya fedha na utawala na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Fedha nyingi sana zinapelekwa katika halmashauri lakini kumekuwa tatizo la miradi mingi kutokamilika kwa wakati," alisema.

Mabula alisema hali hiyo inatokana na miradi mingi kuanza kwa kutegemea nguvu za wananchi hasa katika sekta ya afya na elimu.

"Kuna ujenzi wa zahanati na vituo vya afya umeanza kwa nguvu za wananchi lakini mwisho wa siku havikamiliki, na hilo limekuwa tatizo kubwa katika halmashauri karibia zote tulizokutana nazo.

"Tumeiagiza TAMISEMI miradi hii yote iwe na mpango mkakati wa kuhakikisha inakamilika. Kwa mfano, unakuta halmashauri ina maboma 186 ambayo yameanzishwa kwa nguvu za wananchi lakini yamefika pale yamesimama,"alifafanua.

Alitaja jambo lingine waliloligundua ni mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya halmashauri inayotolewa kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu ambayo ugawaji wake umekuwa hauzingatii uwiano wa kisheria uliopangwa.

"Wanawake wamekuwa wakipewa fedha nyingi kuliko vijana. Kamati inaagiza wafuate mgawanyo huu kwa kuwahakikisha vijana wanapewa uelewa wa kutosha kuhusu mikopo hii," alisema.

Makamu Mwenyekiti huyo alibainisha kuwa hadi kufikia Novemba Mosi mwaka huu vikao vya Bunge vitakapokuwa vinaanza, watakuwa wamechambua na kuhoji halmashauri 27 kwa kipindi cha wiki tatu.

# CRDB yatajwa Benki Bora Tanzania kwa mara ya nne

**Na Mwandishi Wetu,** WASHINGTO D.C

BENKI ya CRDB imetambuliwa kuwa Benki Bora Tanzania kwa mwaka wa nne mfululizo, jambo ambalo linalodhihirisha uimara wake kiuongozi na ubora wake katika sekta ya fedha.

Tuzo hiyo ya Benki Bora Tanzania imetolewa na jarida la kifedha la Global Finance la New York na ilitolewa wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyofanyika katika Klabu ya Kitaifa ya Waandishi wa Habari, ikihudhuriwa na viongozi zaidi ya 900 wa sekta ya fedha kutoka ulimwenguni kote.

Utambuzi huo unaonyesha ukuaji endelevu wa benki, unaonufaisha wateja, wawekezaji na uchumi wa nchi. Tuzo hiyo pia imejikita katika mkakati wa benki wa mabadiliko ya kidijitali, ambao umesababisha matokeo ya kisasa ya kidijitali katika kuendesha ajenda ya ujumuishaji wa fedha nchini.

"Tunajivunia kutambuliwa kama Benki Bora ya Tanzania na Global Finance kwa mara nyingine tena. Huu ni utambuzi kwamba tuko kwenye njia sahihi ya kutoa uzoefu tofauti kwa wateja wetu na kujenga thamani kwa wanahisa wetu huku tukibadilisha sekta ya fedha nchini," alisema Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB.

Kwa miaka minne iliyopita, benki hiyo imekuwa ikiboresha utaratibu wake wa utoaji huduma ili kuwapa wateja huduma za kiwango cha kimataifa katika masuala ya biashara za rejareja na jumla, kupanua wigo wa bidhaa zake na kuimarisha wigo wake kwa kuwekeza kwenye chaneli za kidijitali.

Nsekela alitoa tuzo ya Global Finance kwa wateja wakubwa wa benki, wanahisa na wawekezaji wanaosaidia biashara ya benki.

Kwa sasa Benki ya CRDB ndiyo benki kubwa zaidi nchini Tanzania, ikiwa na mali ya zaidi ya trilioni 10 za kitanzania. Benki hiyo pia inaongoza kwa amana za wateja (Sh. trilioni saba za kitanzania) na mikopo (Sh. trilioni sita za kitanzania).

Jopo la waamuzi wa tuzo limeichagua Benki ya CRDB mahususi kwa ajili ya mafanikio yake katika vipimo vyote muhimu vya biashara.

"Katika kipindi cha mwaka jana, tumeshuhudia Benki ya CRDB ikifanya maboresho makubwa katika utoaji wa huduma, hususan huduma za kibenki za kidijitali," alisema Joseph Giarraputo, Mwanzilishi na Mkurugenzi wa Uhariri wa Global Finance.

Giarraputo pia alitaja tuzo hiyo inatambua kazi iliyofanywa na CRDB katika kusaidia sekta za biashara na wajasiriamali wadogo na wa kati katika kuishi, kupona na kustawi katika kukabiliana na baa la COVID-19.

"Juhudi zote hizi zimeendelea kuimarisha benki hii, na kusababisha utendaji mzuri," Nsekela alisema.

Alibainisha kuwa faida ya ukopeshaji kwa mwaka wa fedha uliopita ilifikia Sh. bilioni 268.2 sawa na ongezeko la asilimia 62.3 kulinganishwa na Sh. bilioni 165.2 mwaka 2020.

Alisema benki ilipata faida ya Sh. bilioni 174 katika nusu ya kwanza ya mwaka kulinganishwa na Sh. bilioni 88 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Nsekela alihusisha mafanikio yao hayo na utendaji mzuri na mazingira mazuri ya biashara nchini, akiishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Hii ni tuzo ya pili kwa Benki ya CRDB ya 'Benki Bora Tanzania' mwaka huu, baada ya kutwaa tuzo hiyo kutoka kwa jarida maarufu la fedha na uchumi la Uingereza la Euromoney mwezi Julai.


## NGOMENI ENTERPRISES

**NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI LOTE UNALODAIWA NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **crdb bank** makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa Pamoja na gharama za dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/ MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | ISMAIL JUMA MNANGO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MTAA WASAKU - MKONDOGWA – TEMEKE NA KISEMVULE - MKURANGA | 2.11.2022 KUANZIA SAA 4:00ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2. | MASOMI RUMISHAEL | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO GOBA,DAR ES SALAAM, MANISPAA YA UBUNGO. | 31.10.2022 KUANZIA SAA 4:00ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 3. | EDSON BRIGHTON BEBWA | FREMU ZA BIASHARA ZILIZOPO KIZINGA, MAJOHE AREA, BLOCK D,PLOT NO. 122 WILAYA YA ILALA. | 9.11.2022 KUANZIA SAA 4:00ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 4. | BEATRICE GERAZI MTAKYAWA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO SARANGA, KIMARA WILAYA YAUBUNGO. | 7.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 5. | ANGELA THIMOTHY MSUYA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIMARA STOP OVER, MTAA WA AMANI, WILAYAYA UBUNGO. | 7.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 6. | IRENE SPARTA MAMKWE | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIVULE,WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM. | 17.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 7. | LIGHTENESS KITENGE | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KITUNDAWILAYA YA ILALA | 17.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 8 | GODFREY MATAJI | NYUMBA YA MAKAZI ILIPO KWA ZOO –CHANIKA WILAYA YA ILALA. | 18.11.2022 KUANZIA SAA 4: 00 ASUBUHI NAKUENDELEA |

117096702

**MASHARTI YAMNADA.**
1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
CRDB BANK PLC, HEAD QUARTER. NGOMENI ENTERPRISES, DSM. SIMU: 0719974916/ 0784252048



**MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED**
"Sisi Kazi tu"

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **WICOM FINANCE LIMITED** tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba/viwanja/Pikipiki. Mnada utafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini. mnada utafanyika kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea

| SN | JINA LA MTEJA | DHAMANA-MAHALI ILI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | NEEMA ESSAU MWAISAMILA | NYUMBA DSM-PUGU KINYAMWEZI | 1/11/2022 |
| 2 | BAKARI FAKIH BAKARI | NYUMBA-DSM PUGU KINYAMWEZI | 1/11/2022 |
| 3 | SAMWEL MUGISHA ISHABAKAKI | NYUMBA-DSM PUGU KINYAMWEZI | 2/11/2022 |
| 4 | MFAUME MTOKO MBEGU | NYUMBA-LINDI LIWALE NANGANDO | 5/11/2022 |
| 5 | RAJABU ALLY MNUNGU | KIWANJA-LINDI NACH- MAJENGO C | 3/11/2022 |
| 6 | DANIFORD DANIFORD CHITOPELA | NYUMBA –LINDI NACHINWEA MWENGE | 4/11/2022 |
| 7 | HAMISI RASHIDI MTESA | NYUMBA-MTWARA MJI MPYA | 9/11/2022 |
| 8 | AHMADI HUSSEIN CHIPULUPULU | VIWANJA(2)MASASI NYASA | 7/11/2022 |
| 9 | PETER PAUL MATHIAS | NYUMBA-LINDI RUANGWA K/HEWA | 2/11/2022 |
| 10 | SAIDI JUMA KIOKA | BOMA-LINDI-RUANGWA NAMAKONDE | 2/11/2022 |
| 11 | MBUSILO MATIKU MONATA | BOMA-LINDI RUANGWA KILIMAHEWA | 2/11/2022 |
| 12 | SHABANI HEMEDI MANZI | KIWANJA-LINDI RUANGWA KILIMAHEWA | 2/11/2022 |
| 13 | STEVEN SIMON MWASE | MTWARA-MASASI NYASA | 8/11/2022 |
| 14 | HAJI AMIRI MMANGO | KIWANJA -MTWARA T/HIMBA MJI MPYA | 10/11/2022 |
| 15 | ISSA ABASI MALUA | KIWANJA-LINDI LIWALE LIKONGOWELE | 5/11/2022 |
| 16 | ISSA HAMISI ISSA | FREM ZA BIASHARA –T/HIMBA MJI MPYA | 10/11/2022 |
| 17 | KILAZA JUMA CHITEMANGO | KIWANJA-LINDI NACH MJINI | 4/11/2022 |
| 18 | HUSSEIN MOHAMED MUSSA | NYUMBA-T/HIMBA MJI MPYA | 9/11/2022 |
| 19 | NOEL COSMAS MAKOTA | NYUMBA-LINDI NACH STESHENI | 4/11/2022 |
| 20 | ZUHURA SELEMANI MTANGA | BOMA-LINDI NACH-KILIMANI HEWA | 4/11/2022 |
| 21 | SAIDI SAIDI LIPWECHE | KIWANJA-LINDI LIWALE NANGANDO | 6/11/2022 |
| 22 | HAMIMU CHANDE MKEKA | KIWANJA-LINDI LIWALE LIKONGOWEL;E | 6/11/2022 |
| 23 | LIJAWA ZAWADI JUMA | NYUMBA-MTWARA T/HIMBA MJINI | 9/11/2022 |
| 24 | SUZANA FAUSTIN MROPE | BOMA- NACHINGWEA TUNDURU YA LEO | 3/11/2022 |
| 25 | HAJI MAGNUS MILANZI | NYUMBA- NACHINGWEA NAMATULA | 4/11/2022 |
| 26 | ABDALLAH OMARI MAENJELA | BOMA –LINDI NACHINGWEA | 3/11/2022 |
| 27 | HARUNA YUSUFU POGONYA | KIWANJA-LINDI NACHINGWEA | 4/11/2022 |
| 28 | RASHIDI ISMAIL MZUI | PIKIPIKI-LINDI LIWALE NANGANDO | 5/11/2022 |
| 29 | REHEMA HUSSEIN MKAMUJANGE | KIWANJA-T/HIMBA MATOGORO | 10/11/2022 |

117095702

**MASHARTI YA MNADA**
1. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena
2. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4. Dhamana itauzwa "kama ilivyo"

meneja mbuzax 0654 147 100


## ANATAFUTWA



217095281

**JINA: RICHARD WASONGA**

**Mtajwa hapo juu anatafutwa na Polisi kufuatia taarifa zilizoko kwenye Jalada namba AR/RB/10649/2022**

**Yeyote atakayemuona au mwenye taarifa ya mahali alipo anaombwa azitoe kituo chochote cha Polisi kwa kutumia RB Namba: AR/RB/10649/2022 au kwa kupiga simu +255 784 812 851 au +255 683 233 721.**

# Uzoefu SADC kumbeba Tax Mambo ya Nje

Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan tangu alipoingia madarakani Machi mwaka jana, amekuwa akifanya mabadiliko ya uongozi katika ngazi mbalimbali ikiwamo Baraza la Mawaziri.

Mabadiliko hayo ya mara kwa mara yamekuwa endelevu kutokana na pangua pangua ambazo amekuwa akizifanya, hali ambayo imekuwa ikiwafanya wateule wake katika nafasi zote, kuanzia wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya ya mikoa pamoja na mawaziri, kutokujua hatima yao.

Hiyo pia inatokana na kauli aliyoitoa Rais Samia kwamba kila uteuzi anaofanya haweki nukta bali koma, akimaanisha kuwa ni endelevu na yanaweza kufanyika mabadiliko wakati wowote.

Katika kuthibitisha hilo, Oktoba 2 mwaka huu, alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri kwa kuwabadilisha wizara mawaziri wawili na kumwacha mmoja. Rais alimteua Dk. Stergomena Tax kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Innocent Bashungwa kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kabla ya mabadiliko hayo, Bashungwa alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Dk. Tax alikuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Tax amechukua nafasi ya Balozi Liberata Mulamula ambaye aliwekwa kando katika mabadiliko hayo. Nafasi ya Bashungwa ilichukuliwa na Angellah Kairuki ambaye sambamba na kupewa nafasi hiyo, aliteuliwa na Rais kuwa mbunge.



Waziri wa mambo ya nje Stagomena Tax

### DK. TAX GUMZO

Pamoja na mabadiliko aliyoyafanya, gumzo lilikuwa kwa Dk. Tax kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuchukua nafasi ya mwanadiplomasia nguli, Balozi Mulamula.

Baadhi ya wadadisi na wachambuzi wa masuala ya kimataifa walihoji kama viatu vya Balozi Mulamula vinaweza kumtosha huku miongoni mwao wakisema amepewa sehemu sahihi na wana imani kwamba anaweza kufanya vizuri kutokana na uzoefu wake kwenye medani ya siasa za kimataifa.

Dk. Tax ambaye ni mchumi mbobezi kitaaluma, ni mwanamke wa tatu kushika wadhifa huo tangu Uhuru wa Tanganyika na baadaye Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa taifa la Tanzania.

Mbali na Balozi Mulamula, mwingine aliyetumika katika nafasi hiyo ni Balozi Dk. Asha Rose Migiro ambaye alikuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo kabla ya kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN).

### UZOEFU KUMBEBA

Pamoja na kuwa na shahada ya uzamivu (Ph.D) katika masuala ya uchumi, moja ya turufu ambazo zinaonyesha kuwa zitambeba katika nafasi hiyo, ni uzoefu wake katika masuala ya ushirikiano wa kimataifa na kikanda.

Kabla ya kuingia katika Baraza la Mawaziri, Dk. Tax alikuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), nafasi aliyoitumikia kwa miaka minane mfululizo. Hii ni moja ya sifa kuwa kwa kutumika katika nafasi hiyo na kwa mafanikio makubwa, viatu alivyovivaa vinamtosha.

Dk. Tax pia ni mbobezi katika masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa kutokana na uzoefu wake. Kabla ya kuteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa SADC, alikuwa Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo ilikuwa kiungo muhimu katika kuimarisha ushirikiano ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kuwapo kwake katika wizara iliyokuwa ikishughulikia ushirikiano wa kikanda wa Afrika Mashariki, ni uzoefu unaombeba mchumi huyo mbobezi kwa kuwa alikuwa kinara wa watendaji kutoka Tanzania katika kuhakikisha nchi inanufaika katika eneo hilo.

Kwa uzoefu wake wa kuwa katika SADC na iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ni imani kwamba ataiwakilisha vyema Tanzania katika masuala ya ushirikiano wa kimataifa zikiwamo jumuiya na taasisi za kimataifa ambazo nchi ni mwanachama wake.

Tanzania imekuwa na ushirikiano na mataifa mbalimbali na kupitia uhusiano huo, imeingia mikataba mbalimbali ambayo ina manufaa baina ya pande husika.

Katika ziara ya karibuni ya Rais Samia Falme za Umoja wa Kiarabu (UAE), kwa mfano, Tanzania iliingia mikataba kadhaa ya ushirikiano ikiwamo ya kibiashara ambayo kwa namna yoyote inanufaika nayo.

### DIPLOMASIA YA UCHUMI

Tanzania katika vipindi tofauti imekuwa ikitekeleza Sera ya Mambo ya Nje ambayo imekuwa na milengo anuai kulingana na madhumuni ya wakati husika pamoja na mazingira ya kisiasa na kuichumi kimataifa.

Baada ya uhuru, Tanzania ilikuwa ikitekeleza sera hiyo kwa kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, ukombozi wa Afrika na uhusiano wa kikanda na kimataifa lakini sasa imegeukia diplomasia ya uchumi ili kujenga mtazamo wenye maslahi ya kiuchumi kwa nchi na wananchi wake.

Mataifa mengi duniani kwa kutambua hilo, yamebadilisha uelekeo wa kutoka katika diplomasia ya zamani iliyokuwa inalenga zaidi kutekeleza masuala ya kisiasa na kuelekea kwenye utekelezaji wa diplomasia ya uchumi inayosisitiza kuboresha na kuendeleza maslahi mapana ya kiuchumi.

Katika kutekeleza hilo, Tanzania iliandaa na kutumia Sera ya Mambo ya Nje inayozingatia diplomasia ya uchumi ili kupata maslahi ya msingi ya taifa na kuwawezesha wananchi wake kupiga hatua za kimaendeleo.

Sera hiyo imezingatia kupanga, kukuza na kulinda maslahi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kuhakikisha uhusiano mzuri kati ya Tanzania na mataifa mengine na taasisi za kimataifa unazingatia maslahi ya kiuchumi na kudumisha amani na usalama.

Kadhalika, sera hiyo pia imeainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 - 2025 ikisisitiza kuwa CCM itaihimiza serikali kuendelea kushiriki kwenye utengamano wa kikanda na kuendeleza diplomasia ya uchumi kwa kuzingatia maslahi muhimu ya nchi ili kunufaisha Watanzania wote.

Diplomasia ya uchumi inachangia katika kuharakisha utangamano wa kisiasa na kiuchumi na kijamii kwa kuweka mazingira muhimu yatakayoiwezesha Tanzania kushiriki kwa ukamilifu katika majadiliano ya kikanda na kimataifa.

Katika utekelezaji wa diplomasia ya kichumi, Tanzania serikali imeendelea kujikita zaida kushirikisha mataifa ya kigeni kujinufaisha kiuchumi katika sekta za biashara na uwekezaji, kilimo, utalii, elimu, afya, mikopo ya riba nafuu na kupata teknolojia ya kisasa.

Hata mabalozi wanaoiwakilisha nchi katika mataifa mbalimbali, wameelekeza nguvu zao katika kuhakikisha kupitia masuala hayo, Tanzania inanufaika katika nyanja mbalimbali ikiwamo kuwavutia wawekezaji katika mataifa mbalimbali kuwekeza katika sekta mbalimbali nchini. Pia wamekuwa wakitafuta fursa ambazo Watanzania wanaweza kunufaika nazo katika mataifa hayo.

Kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Tax sasa anakuwa kinara wa kuhakikisha diplomasia ya uchumi inaipaisha Tanzania katika medani ya kimataifa na nchi kunufaika katika uchumi, elimu, uwekezaji, sayansi na teknolojia.

### ALIKOTOKA

Pamoja na kufanya kazi serikalini kwa nyakati tofauti baada ya kuhitimu masomo kwenye vyuo vikuu mbalimbali, Dk. Tax alianza kujulikana zaidi mwanzoni mwa miaka ya 2000 baada ya kuteuliwa kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA) au kwa Kiingereza BEST.

Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, alipoingia madarakani, alimteua kuwa Naibu Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Mipango na Uwezeshaji Kiuchumi iliyokuwa chini ya Waziri Dk. Juma Ngasongwa.

Muda mfupi baadaye aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara na baadaye Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki wakati huo kabla ya kwenda SADC alikotumika miaka minane katika nafasi ya Katibu Mtendaji.

Baada ya muda wake kumalizika, alirejea nchini na kwa kutambua uwezo, uzoefu na sifa zingine, Rais Samia alimteua kuwa Mbunge na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wiki moja iliyopita akateuliwa katika nafasi yake ya sasa.

## TANGAZO



A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serengeti Girls inawezekana robo fainali Kombe la Dunia

**TIMU** ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Girls, juzi ilipata ushindi wake wa kwanza kwenye Fainali za Kombe la Dunia kwa wanawake wa umri huo zinazoendelea nchini India baada ya kuifumua Ufaransa kwa mabao 2-1.

Ushindi huo wa Serengeti Girls umekuja baada ya kupoteza kwa mabao 4-0 dhidi ya mabingwa watetezi wa kombe hilo, Japan kwenye mchezo wao wa ufunguzi Jumatano iliyopita.

Kwa matokeo hayo sasa Serengeti Girls inahitaji kushinda mechi yao ya mwisho kesho dhidi ya Canada ili kujihakikishia nafasi ya kutinga robo fainali kutoka Kundi lao la D linaloongozwa na Japan ambayo yenye ponti sita ikifuatiwa na Tanzania yenye alama tatu huku Ufaransa na Wacanada hao kila moja ikiwa na pointi moja.

Kwa kiwango kilichoonyeshwa na Serengeti Girls juzi hadi kuifanya Ufaransa kupata bao lao pekee kwa mkwaju wa penalti, tunaamini kama ikikaza na kujituma vilivyo dhidi ya Canada, robo fainali inawezekana kabisa jambo ambalo itakuwa imeandika rekodi nyingine baada ya hiyo ya kushiriki kwa mara ya kwanza michuano hiyo.

Kama imeweza kuifunga Ufaransa ambayo mchezo wa kwanza ilitoka sare na Canada, tunaamini endapo benchi la ufundi litalofanyia kazi mapungufu machache yaliyojitokeza mechi mbili zilizopita, ushindi unawezekana bila tatizo.

Sisi tunaamini kikubwa kilichoisumbua Serengeti Girls katika mchezo wa kwanza ni homa tu ya kuanza michuano hiyo mikubwa duniani kwa umri wao, ambayo sasa imeshatoweka na kilichobaki ni kuonyesha tu uwezo wao ili kushinda mchezo huo wa mwisho wa hatua ya makundi.

Aidha, kwa Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, anapaswa kufanyia kazi zaidi safu yake ya ulinzi na kuitaka kuwa makini zaidi na ili kuepuka kufanya madhambi ndani ya eneo la hatari kama ambavyo imewagharimu katika michezo miwili iliyopita dhidi ya Japan na Ufaransa.

Hii ni kutokana na michezo yote miwili kusababisha penalti ambazo zimewanufaisha wapinzani wao Japan na Ufaransa kwa kupata bao, jambo ambalo linaweza kuwagharimu zaidi mechi ijayo kama lisipofanyiwa kazi kwa umakini zaidi.

Lakini hii ni fursa kwa wachezaji wa Serengeti Girls kuonyesha wanaweza kwa kila mmoja kupambana hadi tone la mwisho kwani si tu kwamba ushindi wao ni fahari kwa Tanzania, bali fainali hizo zinaweza kuwa mwanzo wa wao kutoka kimaisha endapo wataendelea kufanya vizuri zaidi.


Tunatambua uwapo wa mawakala wengi katika michuano hiyo, ambayo kwa Afrika ina wakilishwa na mataifa matatu; Morocco, Nigeria na Tanzania na timu hizo kila moja ikiwa imevuna pointi 3 katika michezo miwili ya awali.

Hivyo, kwa wachezaji ambao wataonyesha uwezo wa juu wanaweza kununuliwa na klabu kubwa Ulaya kwenda kucheza soka la kulipwa na kujipatia maslahi makubwa zaidi na kuinua maisha yao kwa ujumla.

Kwa mantiki hiyo, wachezaji wa Serengeti Girls, huu ni wakati wa kupambana na kuiwezesha Tanzania kufika robo fainali, nusu na hatimaye fainali, kwani kadri wanavyosonga mbele kwa kufanya vizuri kwenye michuano hiyo ndivyo wanavyotanua wigo wa kujitangaza zaidi na uwezo wao kuonekana.

Sisi tukiwa kama wadau namba moja wa michezo nchini tunaungana na Watanzania wote kwa ujumla kuwaombea na kuwatakia kila la kheri katika maandalizi yao ya mchezo wa kesho dhidi ya Canada ili kupata ushindi na kuitangaza vema Tanzania kwani tunachokitaka si tu kuona wakifika robo fainali, bali nusu, fainali na kisha kutwaa ubingwa huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongereni Serengeti Girls kuiheshimisha Tanzania

Na Adam Fungamwango

**INAWEZEKANA** nchini India, Ufaransa au watu wa nchi zingine zinazoshiriki Kombe la Dunia la Wanawake chini ya miaka 17, mwaka huu, walikuwa hawafuatilii sana habari za Tanzania, lakini sasa wanaweza kuanza kufanya hivyo baada ya Timu ya Taifa, Serengeti Girls kuishangaza dunia.

Timu hiyo ambayo awali ilikuwa haitarajiwi kufanya chochote au kuzungumzwa sana, iliwashtua wengi ilipotoa kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Timu ya Taifa ya Ufasansa kwenye mechi ngumu iliyochezwa Uwanja wa Fatorda, Goa nchini India inakofanyika michuano hiyo.

Kwa tulioangalia mechi hiyo, haikuwa nyepesi hata kidogo, badala yake ilibidi wachezaji wa Tanzania kupambana kuweza kuwazuia mawinga wenye kasi wa timu hiyo, wakiongozwa na mchezaji wao tegemeo alionekana kuwa mwiba kwenye safu ya ulinzi ya Serengeti Girls, Lucia Calba, ambaye ndiye aliyefunga bao la kufutia machozi.

Timu ya Taifa ya Tanzania chini ya miaka hiyo, inaingia kwenye vitabu vya kumbukumbu ya soka la Tanzania na dunia nzima kuwa pamoja na kutinga fainali hizo, ilishinda mechi yake ya kwanza dhidi ya Ufaransa.

Pia, rekodi haitofutika kuwa mchezaji Diana Mnally ndiye Mtanzania wa kwanza kufunga bao kwenye michuano ya kombe hilo la dunia chini ya umri huo kwa Tanzania.

Inawezekana kama baadhi ya watu wanaona kawaida tu wala hawashtuki, lakini ukiangalia mazingira ya jinsi timu zetu Afrika zinavyojiandaa na wenzetu Ulaya ni vitu viwili tofauti.

Jinsi wachezaji wetu wanavyopatikana, kuvumbuliwa na utamaduni wetu na wenzetu Ulaya ni tofauti.

Kutokana na hali hiyo inabidi si tu kuipongeza Serengeti Girls kwa kuifunga Ufaransa, lakini kuwapongeza kwa kushinda dhidi ya timu na nchi ambazo zina skauti bora ya kutafuta, kukusanya wachezaji, kuwatunza na kuwatayarisha kuliko sisi.

Hata ukiangalia jinsi wanavyocheza, unaona kabisa kuwa wachezaji wa timu pinzani wameanza kucheza soka wakiwa bado wadogo sana kutokana na uwezo mkubwa wa kumiliki mpira na kupiga pasi.

Wachezaji wetu wengi bado hawapatikani shuleni wakiwa bado wadogo, lakini wazazi wa Kitanzania ni wazito mno kuwaruhusu watoto wao wa kike tena chini ya miaka 17 kwenda kucheza soka, kukaa kambini au kwenye vituo vya soka.

Wengi wanaanza mpira ukubwani, na hadi anakubaliwa basi kunatokana na msukumo wa mtu au watu fulani ambao wamecheza soka kwenye ukoo au familia, vinginevyo ni marufuku.

Ndiyo maana nasema inawezekana bado kuna vipaji vya wachezaji wengi vipo mitaani, lakini vimefichwa na wazazi. Labda kwa ushindi huo wa Serengeti Girls na wazazi kuwaona watoto wa wenzao wanacheza Kombe la Dunia, wakiwaangalia kwenye luninga, wanaweza kulegeza masharti.

Pamoja na changamoto zote hizo, bado hazikuwazuia vijana hao kuonyesha kile walichojaaliwa nacho na kuweza kuifanya Tanzania kuwika na kuzungumzwa kila kona nchini India na kwingineko.

Ushindi huo pia unaweza kukuza utalii, kwani jana ilishuhudiwa baadhi ya Watanzania waliokuwa huko wakiimba na kucheza, watu wa mataifa mengine wakiwaangalia na kutabasamu.

Nchi yetu sasa itaanza kuzungumziwa vizuri, kila mmoja akitamani kuifahamu zaidi na hata kufika kuishuhudia.

Ni kama DR Congo, watu wanavyopenda kwenda kutokana na kuheshimishwa na wanamuziki maarufu wa huko, Brazil kwa ajili ya soka na wanasoka maarufu kama kina Pele na Jamaica kwa ajili ya Bob Marley.

Mbali na pongezi, tunaendelea kuiombea timu hiyo izidi kuiheshimisha nchi kwa kushinda mechi ijayo dhidi ya Canada ili mbali na kukuza utalii, lakini watu wa mataifa ya nje waanze kuvutiwa na wachezaji wa Kitanzania, wawachukue kwa ajili ya kucheza soka la kulipwa kwenye nchi mbalimbali.

Nina uhakika baada ya michuano hii, kuna baadhi ya wachezaji hawatocheza tena soka hapa nchini.

## Wanaofanya shughuli kando njia SGR watakiwa kuondoka

**Na Pilly Kigome**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, amewataka wananchi wote wanaofanya shughuli za kiuchumi na kijamii kando mwa njia ya reli waondoke kuupisha mradi wa treni ya mwendo wa haraka (SGR).

Mwakibete alitoa amri hiyo mwishoni mwa wiki katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa Reli yaliyofanyika, jijini Dar es Salaam.

Alisema wananchi wanatakiwa watambue uwapo wao kukaa maeneo hayo ni hatari kwa kuwa treni hizo zina mwendo kasi na kuondoka kwao kutaepusha ajali zinazoweza kuzuilika.

Alisema shughuli hizo zinazofanyika katika maeneo hayo pembezoni mwa njia za reli zinaharibu miundombinu kwa kuwa serikali imeshatumia takribani Shilingi trilioni saba katika mradi wa SGR.

Pia aliwataka watumishi kwenye taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ikiwamo TRC, TAZARA, LATRA na TANROADS kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuwataka wawe waaminifu na kuondoa uzembe unachangia kusababisha ajali na kugharimu maisha ya wananchi.

Pia aliliagiza Shirika la Reli (TRC) kushughulikia changamoto zinazowakabili wafanyakazi wake ikiwamo malimbikizo ya mishahara ili kuwezesha wafanyakazi kuwa na ari ya kujituma kufanya kazi. Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, alisema mamlaka hiyo itahakikisha inasimamia na kulinda usalama wa wananchi katika usafiri wa reli.

Pia aliwataka wananchi kila mmoja kuwa mlinzi wa mwenzake katika uhujumu wa miundombinu ya reli kwa kuwa ni maendeleo katika kulijenga taifa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzani (TRC), Masanja Kadogosa, ameishukuru serikali kwa kuwekeza katika sekta ya reli nchini kwa ujenzi wa reli ya kisasa ambayo kupitia mradi huo kutakuwa na mabadiliko makubwa katika shughuli za kiuchumi na mifumo ya ishara na mawasiliano.

Alisema katika kuhakikisha usalama wa wananchi na watumiaji wa reli, wameanza kutoa elimu na wataweka uzio katika njia nzima ipitayo reli ili kulinda usalama wa watu na wanyama.



Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku nchini, Victor Mwambalaswa, akisikiliza maelezo ya ofisa wa Kampuni ya Tumbaku Mkwawa mjini Morogoro, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hukumu anayedaiwa kumuua na kumfukia mkata tiketi leo

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu leo inatarajiwa kutoa hukumu dhidi ya mshtakiwa Hemed Ally anayetuhumiwa kumuua mkata tiketi Farihani Maluni eneo la Sharif Shamba, Ilala jijini Dar es Salaam na kumfukia mbele ya nyumba aliyokuwa amepanga. Hukumu hiyo inatarajiwa kusomwa na Hakimu Mkazi Mkuu, Joyce Minde wa mahakama hiyo baada ya pande zote kufunga ushahidi wao na kuwasilisha majumuhisho ya mwisho ya kesi hiyo kwa njia ya maandishi.

Upande wa mashtaka ulifunga ushahidi wake kwa mashahidi wanane na vielelezo kadhaa likiwamo godoro linalodaiwa kufungwa pamoja na mwili wa marehemu Maluni na kisha kufukiwa ardhini.

Katika kesi hiyo, mshtakiwa Ally alijitetea mwenyewe akiongozwa na wakili wake, Caroline Kigembe, akidai kuwa siku ambayo inadaiwa alimuua Maluni, alikuwa mahabusu kwa tuhuma za kupotea kwa marehemu huyo.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Binadamu na Vifo vya Shaka, Innocent Mosha alidai kuwa Maluni kabla ya kuuawa na kufukiwa, alifungwa kamba ya katani mikononi na kichwani alifungwa plasta.

Alidai kuwa haikuwa rahisi kujua chanzo cha kifo cha Maluni, lakini kutokana na kuwapo plasta eneo la fuvu alihisi aliuawa kwa kuzibwa mdomo na kumsababishia akose pumzi.

Alidai kuwa Februari 9, 2015, akiwa katika eneo lake la kazi Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alipelekewa taarifa na Ofisa Upelelezi wa Mkoa wa Ilala ikimtaka kwenda Sharif Shamba ndani ya Wilaya ya Ilala kuchunguza mwili wa binadamu unaohisiwa kufunikwa ndani ya ua la nyumba.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Salome Asey, Dk. Mosha alidai alichukua vifaa vyote vya kazi na kuongozana na askari polisi hadi eneo la tukio.

Alidai walipofika eneo hilo majira ya saa sita kasoro mchana, alikuta vijana wakiwa wameishaanza kufukua eneo hilo, ambapo ndani ya shimo walikuta matofali mapya, masalia ya mwili yaliyokuwa yamezungushiwa ndani ya godoro, huku mikono ya masalia yale ya mwili ikionekana kufungwa kwa katani na fuvu likiwa na plasta.

Inadaiwa Juni mwaka 2014, Ally alimuua Maluni eneo la Sharif Shamba ndani ya Wilaya ya Ilala na kumfukia mbele ya nyumba aliyokuwa akiishi.

## KABWELA



# NMB yasimika bendera Mlima Kilimanjaro ikihamasisha utalii

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa Benki ya NMB wamefanikiwa kupanda na kusimika bendera ya taasisi hiyo kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro kama sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja Duniani.

Benki hiyo pia imelitumia tukio hilo kuwahamasisha wafanyakazi wake na Watanzania kwa ujumla kushiriki utalii wa ndani ili kusaidia kukua kwa shughuli hiyo yenye fursa lukuki kibiashara na tija kiuchumi.

NMB ilianza rasmi kushiriki kuutangaza utalii wa ndani hivi karibuni na kutangaza kushiriki kusaidia kuchangia kukua kwake Jumamosi iliyopita huko Moshi wakati wa kuwapokea wafanyakazi wake sita waliofanikiwa kupanda mlima huo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo iliyofanyika kwenye lango la Mweka, Meneja wa Kanda ya Kaskazini wa Benki ya NMB, Dismas Prosper, alisema timu ya watu sita iliyokwea mlima huo mrefu kuliko yote barani Afrika ilitumia siku saba kutimiza azma hiyo.

Alisema kufanikiwa kwa timu hiyo kusimika bendera ya NMB kwenye Kilele cha Uhuru ni jambo kubwa kwa wafanyakazi hao na benki hiyo ambayo ndiyo kinara katika shughuli na huduma za kifedha nchini. "Kwanza kabisa, dhamira ya safari hii ni kufanikiwa kuupanda Mlima Kilimanjaro na kusimika bendera ya Benki ya NMB kwenye kilele chake kama namna ya kipekee kwetu kusherehekea Wiki ya Huduma kwa Wateja.

"Pia uongozi wa NMB unalitumia zoezi ili la kuupanda Mlima Kilimanjaro kuhamasisha utalii wa ndani na kuchangia maendeleo ya shughuli za kitalii nchini," alisema.

Prosper pia alisema tukio la kusherehekea Wiki ya Huduma kwa Wateja mita 5,895 (urefu wa mlima huo) kutoka usawa wa bahari, lina maana kubwa kwa namna benki hiyo inavyozingatia huduma bora kwa wateja na katika nafasi yake kama kiongozi wa kibenki sokoni.

Alisema kitendo hicho pia kutambua umuhimu wa biashara ya utalii na jukumu la msingi la sekta hiyo katika uchumi wa taifa na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Kaimu Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro, Iman Kikoti, alisema kitendo cha wafanyakazi wa NMB kupanda Mlima Kilimanjaro kinaimarisha nafasi ya benki hiyo kuendelea kuwa karibu na sekta ya utalii na mshirika wa kimkakati wa maendeleo ya taifa.

Pia alibainisha kuwa uamuzi wa NMB wa kuhamasisha utalii wa ndani ni kielekezo cha utayari wake kuchangia maendeleo na ustawi wa tasnia hiyo ili ichangie kikamilifu kuchochea kukua kwa uchumi nchini na ujenzi wa taifa.

Kikoti aliipongeza NMB kwa hilo, akisema utalii wa ndani ni hazina kubwa kwa taifa ambayo inahitaji ushirikiano wa wadau kuufanya kushamili na kuchangia kukua kwa sekta nzima ya utalii nchini.

"Kwa sasa mchango wa utalii ni mdogo, hivyo uamuzi wa NMB kusaidia kuuchangamsha ni jambo jema na la kimaendeleo linalopaswa kuungwa mkono na wadau wote wa sekta binafsi," alisisitiza.

Kiongozi wa safari hiyo iliyoanza Oktoba 8, mwaka huu, kwenye Lango la Machame, Alfred Shayo ambaye ni Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, alisema kamwe hawatajutia kushiriki kwenye jambo hilo lililowafunza mambo mengi ya kimaisha na kikazi.

Kwa mujibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Sekta ya Utalii inchini inaingiza asilimia 25 ya fedha za kigeni na kuchangia pato la taifa kwa asilimia 17.5 huku ikitoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa maelfu ya wananchi.



Wafanyakazi wa Benki ya NMB pamoja wasindikizaji wao wakishikilia vyeti walivyotunukiwa baada ya kupanda Mlima Kilimanjaro katika kusherehekea huduma kwa wateja kwa benki hiyo. Wafanyakazi hao walitumia siku saba kupanda na kushuka mlima ili kuisimika bendera ya Benki ya NMB kileleni mwa mlima huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ma-RC na ma-DC waonywa kuingilia utendaji wa mahakama

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani, amewaonya wakuu wa mikoa, wilaya na viongozi wengine wa umma kuingilia au kuzuia utekelezaji wa amri na tuzo zinazotolewa na mahakama kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha sheria na katiba ya nchi.

Alitoa onyo hilo wakati akizungumza na wadau wa mahakama Mkoa wa Singida juzi alipotoa mada kuhusu matarajio ya Tume ya Utumishi wa Mahakama kutoka kwa wadau.

Jaji Siyani alisema kumekuwa na tatizo la kuingilia kazi za mahakama ambapo baadhi ya viongozi wa umma wamekuwa wakitaka hata amri za wito wa mahakama zipitie kwenye ofisi zao.

Jaji Siyani alisema viongozi wa serikali wa ngazi zote ni wadau wakubwa wa mahakama, hivyo wanao wajibu wa kuisaidia kutimiza wajibu wake wa kikatiba.

"Katika nchi yetu mahakama ndio chombo kilichopewa kauli ya mwisho ya utoaji haki, hivyo kuzuia kwa namna yoyote utekelezaji wa amri ya mahakama ni kukiuka matakwa ya utawaka bora," alionya.

Aliongeza kuwa mara kadhaa uingiliaji wa kazi za mahakama umekuwa ukifanywa na viongozi wa umma kwa kile kinachosemwa kulinda haki za wanyonge, kuzuia uvunjifu wa amani au kutoa fursa ya upatanisho baina ya mlalamikiwa na mlalamikaji.

Jaji Siyani alisema ni vyema viongozi wa umma wakajizuia kuingia kwenye mtego huo na badala yake kama kuna mazingira yanayohitaji mchakato wa kuzuia amri za mahakama, basi viongozi wa mahakama wa ngazi za wilaya, mkoa na hata kanda na wadau wajulishwe ili kufuata utaratibu wa kisheria.

Alisema matarajio ya tume ni kuona kuwa hawatakuwa kikwazo katika mfumo wa utoaji haki bali kuwe na ushirikiano wenye tija ili wananchi wa pande zote wananufaike na matunda ya haki zao.

"Viongozi wasiingie kwenye mtego wa kukiuka matakwa ya utawala bora, bali wawasiliane na mahakama na eneo la hukumu ndilo ambalo linapigiwa kelele sana kwamba lina matatizo katika mahakama," alisema.

Jaji Siyani alisema tume na mahakama zinatarajia kutakapotokea shida kama vile za kimaadili, wahusika watachukuliwa hatua ikiwamo kupelekwa kwenye kamati zinazohusika na kushughulikia na maadili kwa viongozi.

Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma alisema eneo la mahakama ni lazima liwe safi, hivyo halipaswi kuwa na vitendo vya rushwa ambavyo vinasababisha wananchi kutokuwa na imani na chombo hicho.

## Mpango kabambe kukabili uharibifu mazingira waletwa

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imewasilisha mpango kabambe wa miaka 10 wa usimamizi wa hifadhi za mazingira kwa lengo la kutatua athari zinazojitokeza ikiwamo uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji.

Akiwasilisha mpango huo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira, Dk. Thomas Bwala, alisema wameonyesha maeneo tisa yanayohitaji kupewa kipaumbele na hatua zinazochukuliwa ili kurudisha mazingira katika hali yake ya zamani.

Aliyataja baadhi ya maeneo hayo kuwa ni uharibifu wa ardhi, uchavuzi wa vyanzo vya maji, ukatwaji na uharibifu wa misitu, uharibifu wa makazi ya wanyama pori na wa viumbe hai, mimea vamizi na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

"Kila changamoto mpango kabambe huu umeainisha hali ikoje katika hizo changamoto na tumeeleza sababu gani zilizosababisha kufikia hapa tulipo, athari zipi zimejitokeza na hatua gani zichukuliwe,"alisema Dk. Bwala.

Alisema wadau wote watashirikiana pamoja na sekta binafsi kila mmoja kuhakikisha anachukua hatua na jambo la msingi ni kuboresha mazingira ya nchini.

"Tunahitaji kupata mahitaji yetu kutoka katika mazingira na ni muhimu kuyatunza mazingira ili kuhakikisha na kesho yanaendelea kuwa imara kwa mfano eneo la kilimo cha mpungu wote tunahitaji mchele, je, ikitokea hakuna maji ya kuzalisha huo mchele kila mtu anatakiwa kujua tunahitaji kupata mahitaji lakini tutunze mazingira ambayo yanatupa maji na tunazalisha vyakula," alisema.

Aliongeza kuwa lengo kubwa ni kuweka vipaumbele na kuonyesha maeneo ambayo kila mmoja wao anatakiwa kuyafuata, ili kuwapo na maendeleo endelevu ikiwamo afya na mazingira kutunzwa.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, alisema mpango huo utatekelezwa katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka huu hadi mwaka 2032.

Alisema lengo la kuandaa mpango kabambe ni kutokana na nchi ya Tanzania kuwa na mazingira tofauti kutokana na ukubwa wake, hivyo wameainisha changamoto za kimazingira ambazo zinapatikana.

"Kuna changamoto ya ufugaji ambao haufuati utaratibu unaharibu ardhi yetu na uoto wa asili unapotea. Tumeonyesha ni mikoa ipi ambayo imepata changamoto hiyo na ukataji wa miti unaleta ukame katika maeneo mbalimbali na tumeonyesha mikoa yenye hilo tatizo," alisema Maganga.

## Serikali kukopa bilioni 200/- kuboresha mahakama

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI inakusudia kuchukua mkopo wa gharama nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB) wa Dola za Marekani milioni 90 (Sh. bilioni 200) zitakazotumika kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya mahakama.

Mtendaji wa Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapo baada ya Tume ya Utumishi wa Mahakama ilipofanya ziara mkoani humo kwa ajili ya kuzungumza na Kamati za Maadili na wadau mbalimbali wa mahakama.

Alisema mahakama imejipanga ndani ya miaka miwili ifikapo 2024 ujenzi wa majengo yawe yamekamilika ili kwenye kila mkoa kuwe na Mahakama Kuu pamoja na kuhakikisha wilaya zote zinakuwa na mahakama kusogeza huduma karibu kwa wananchi.

Prof. Gabriel alisema, suala la haki ni la muungano, kutajengwa Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki (IJS) Zanzibar na vituo kama hivyo vilishajengwa sita katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mwanza, Morogoro, Kinondoni na Temeke maalum kwa ajili ya kesi za mirathi.

Kuhusu miundombinu, alisema mahakama hivi sasa ni moja ya taasisi zilizo juu katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi wa mahakama.

Alisema mahakama itaendelea kuboresho mawasiliano ili kuwapo mashauri yanayoendeshwa kwa njia ya mtandao kupunguza adha ya mahakimu na majaji kusafiri.

Prof. Gabriel alisema mahakama hivi sasa inatamani kufikia hatua ya kutumia AI (Efficiency Intelligence) ubongo bandia ili hakimu au jaji anaposoma hukumu kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili itafsiriwe papo hapo na kuandikwa.

"Jaji au Hakimu ataongea pale kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili hukumu hiyo itatafsiriwa kwa muda ule ule na kumalizika na inaandikwa, huko ndiko mahakama tunakotaka kwenda katika matumizi ya TEHAMA," alisema.

Prof. Gabriel akizungumzia mahitaji ya watumishi wa mahakama, alisema waliopo ni takribani 6,000 kati ya mahitaji ya watumishi 10,350.

"Tunaishukuru serikali hadi kufikia Juni 2022 ilituongezea watumishi 215, tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan hata katika uteuzi wa majaji," alisema.

# SBT yaahidi Watanzania neema ya sukari

**Na Mwandishi Wetu**

BODI mpya ya Wakurugenzi wa Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), imeliahidi taifa neema ya sukari ndani ya miaka mitatu ijayo huku mwenyekiti wake, Filbert Mponzi, akisema upungufu wa bidhaa hiyo sasa utakuwa historia.

Mkurugenzi Mkuu wa SBT, Prof. Kenneth Bengesi, alisema taifa sasa hivi linakabiliwa na nakisi ya tani 60,000 za sukari na kunahitaji ongezeko la uzalishaji wa wastani wa tani 20,000 kwa mwaka.

Wakizungumza wiki iliyopita mjini Moshi, wajumbe hao walisema taifa lina kila kitu kinachohitajika ili kufikia lengo kuu la sukari la nchi na kufanya bidhaa hiyo kupatikana kwa urahisi.

"Hii ni pamoja na kuwapo sera wezeshi, kukua kwa uzalishaji, ambao takwimu za SBT uliongezeka kwa karibu asilimia 17 ndani ya miaka sita kuanzia mwaka 2013. Pamoja na ukuaji huu, uhitaji wa sukari ni mkubwa kuliko kiasi kinachozalishwa na kusambazwa," alisema.

Mponzi alisema jitihada za kuongeza uwezo wa uzalishaji wa ndani zitahitaji uboreshaji zaidi wa mazingira ya biashara ya sekta hiyo ili kuunganisha eneo la uendeshaji na kuvutia wawekezaji wapya.

"Wakati anaizindua bodi hii, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitupa maelekezo zaidi ya kumi ya kumwongozo hata hivyo, alisisitiza jambo moja kwamba ni lazima bodi hii mpya ihakikishe kuwa taifa linajitosheleza kwa sukari ifikapo mwaka 2025," Mponzi aliwaambia waandishi.

"Hili ndilo lengo letu kuu na kipaumbele cha serikali, ambalo linaweza kufikika kama tutakuwa na sera wezeshi na kuyaweka sawa yale mambo yote yanayokwaza kukua kwa sekta hii," alisema jijini Arusha.

Alisema maendeleo ya uchumi wa sukari nchini ni moja ya vipaumbele vya kilimo vya serikali kukabiliana na ongezeko la uhitaji wa sukari kwenye soko la ndani.

Prof. Bengesi alisema mienendo kadhaa kwenye sekta inaashiria kuwapo kwa mafanikio mazuri katika hilo huku serikali ikiipa bodi mpya ya SBT jukumu la kuhakikisha azma ya taifa ya kujitosheleza kwa sukari inatimia ifikapo mwaka 2025.

"Ziara hii ya wajumbe wa Bodi TOC na nyingine watakazozifanya ni kwa ajili ya kuwapa nafasi kuanza kujua tasnia wakijiandaa kutekeleza majukumu yao," Prof. Bengesi alisema. Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPC, Marius Jacobs, alisema sekta kwa sasa inakua vizuri na kuwawezesha wazalishaji kuzalisha zaidi ili wasaidie kupunguza changamoto ya kuagiza sukari nje.

Jacobs alisema uwekezaji huo umekuwa wa tija kwa kuwa umeimarisha uzalishaji kitaifa na kwa kampuni hiyo hadi tani 110,000 huku matarajio yakiwa ni kuongezeka hadi tani 115,000 mwaka 2025.

Sukari inayozalishwa nchini tangu kampuni hiyo ibinafsishwe tayari wamewekeza zaidi ya Sh. bilioni 250 kukarabati mitambo, kuongeza uzalishaji na kukiendesha kiwanda kisasa zaidi.

Alisema sukari iliongezeka kwa asilimia 16.6 kutoka tani 307,431 hadi 359,219 kati ya mwaka 2013 na 2019 kabla ya kufikia 367,000, mwaka jana.



Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), wakipata maelezo kuhusu uzalishaji katika Kiwanda cha Chai Mponde, wilayani Lushoto, Mkoa wa Tanga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PIC yaridhishwa uwekezaji kiwanda cha chai Mponde

**Na Mwandishi Wetu,** LUSHOTO

WAJUMBE wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), wameridhishwa na uwekezaji uliofanywa katika Kiwanda cha Chai Mponde, wilayani Lushoto, Mkoa wa Tanga.

Waliyasema hayo baada ya kutembelea kiwanda hicho kilichoko Kata ya Mponde, Jimbo la Bumbuli Oktoba 15, ili kuona uwekezaji huo uliofanywa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR).

"Kwa niaba ya Kamati nichukue fursa hii kuwapongeza sana, nadhani nyuso zetu mmeziona tumeridhika na kile tulichoona, naomba spirit (moyo) hii mliyoanza nayo msiipunguze muwendelee nayo," alisema Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, George Malima ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa.

Malima alisema, kazi ya kamati yake ni kuangalia serikali ilikoweka mitaji.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ameruhusu fedha nyingi kuja kwenye kiwanda hiki ili muweze kuwekeza na hivyo kutoa ajira za kutosha na kuinua maisha ya Watanzania, hiyo ndiyo hasa nia ya Mheshimiwa Rais," alibainisha.

Naye Dk. Julius Chaya, ambaye ni Mbunge wa Manyoni na Mjumbe wa Kamati hiyo ya PIC, alisema wakati wawekezaji hao walipokutana na Kamati hiyo bungeni jijini Dodoma, waliona wazo hilo la uwekezaji ni zuri kwa kuwa uwekezaji ndiyo umekuza ajira kwenye maeneo mbalimbali duniani.

"Tunawapongeza mnapofufua hivi viwanda, wananchi wanapata ajira, wakulima nao wanapata mahala pa kuuza mazao yao kwakweli tunaishukuru serikali, lakini tunaishukuru mifuko yote kwa kazi nzuri," alisisitiza Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar na Mjumbe wa Kamati, Mariam Mwinyi.

Baadhi ya wajumbe wametoa ushauri kwa uongozi wa kiwanda kujipanga vizuri katika eneo la masoko hususan ya nje, kwa kuwa wanunuzi wakubwa wa bidhaa za kilimo licha ya kusisitiza ubora, pia hupenda hakikisho la kupata bidhaa kwa mwaka mzima bila kusitisha.

Akiwakaribisha kiwandani hapo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Emmanuel Humba, alisema wamefarijika na ujio wa kamati kwa kuwa ni ishara ya kutambua juhudi zilizofanywa na wawekezaji hao watatu.

"Kiwanda hiki kama mlivyoona kinawahusu wananchi, wawekezaji tunaongeza nguvu tu, lakini watakaofanya kiwanda hiki kifanye kazi ipasavyo ni wananchi wenyewe," alisema. Alitoa mfano kuwa wakati akiwa kiwandani alikutana na mkulima mmoja aliyeleta majani yake ya chai kilo 15 na alionyesha furaha kuwa alisema baada ya kuuza ana uhakika wa kupata mahitaji mbalimbali ya nyumbani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda cha Chai, Anselim Peter alisema, kusudio la kufufuliwa kiwanda hicho ni kuwawezesha wananchi wa Lushoto, Bumbuli na maeneo jirani kupata kipato na kuwainua kiuchumi kwa kuwa wengi wanategemea zao hilo.

"Tunategemea kwamba kiwanda kitanufaisha takriban asilimia 70 ya wakulima wa chai kutoka Lushoto, Bumbuli Korogwe na maeneo jirani, kiwanda hiki ni muhimu kwa uchumi wa eneo hili na karibu asilimia 100 kimekamilika," alisisitiza.

Alisema awamu ya kwanza ya kufufua kiwanda hicho ilikuwa ni kukarabati majengo na mitambo ambayo ilikufa wakati awamu ya pili ilikuwa ni kuboresha kiwanda kwa ujumla wake na kutengeneza menejimenti.

# Meneja TARURA Wilaya ya Kilombero atumbuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** KILOMBERO

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Mhandisi Victor Seff, amemwondoa kwenye majukumu yake aliyekuwa Meneja wa TARURA Wilaya ya Kilombero kwa kushindwa kusimamia kikamilifu miradi.

Miongoni mwa miradi aliyoshindwa kusimamia ni ujenzi wa boksi kalavati katika barabara ya Mawala-Mofu-Ikwambi, yenye urefu wa Kilometa 30 iliyoko Halmashauri ya Mlimba, Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro.

Akiwa katika ziara yake mwishoni mwa wiki ya kukagua miradi wilayani Kilombero, Mhansisi Seff alibaini upungufu katika usimamizi wa miradi ikiwamo ujenzi wa boksi hilo ambalo limejengwa chini ya viwango vya mkataba.

"Nimekagua na kujiridhisha kwamba mradi huu umejengwa chini ya kiwango, kwa kweli sijaridhishwa kabisa na usimamizi wa hapa, hivyo nimemwondoa kwenye nafasi yake kuanzia leo aliyekuwa Meneja wa TARURA Wilaya ya Kilombero na atapangiwa majukumu mengine," alisema Mhandisi Seff.

Aidha, Mtendaji Mkuu alimtaka mkandarasi aliyejenga mradi huo chini ya viwango vya mkataba kubomoa kwa gharama zake na kukamilisha ujenzi wa boksi hilo jipya ndani ya kipindi cha mwezi mmoja. Aliagiza mameneja wa TARURA nchini kusimamia kikamilifu miradi kwenye maeneo yao na hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atayeshindwa kutimiza majukumu yake ili kuhakikisha fedha inayotolewa na serikali inaendana na ubora wa miradi inayotekelezwa.

TARURA inaendelea na kazi ya kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo ya mtandao wa barabara za wilaya wenye jumla ya Kilometa 144,429.77 nchini ili kuhakikisha wananchi wanazifikia huduma za kijamii na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.



Mwanzilishi wa Ikupa Trust Fund, Stella Ikupa ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum CCM (katikati) na Kaimu Meneja wa Uhusiano wa Jamii Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Zuwena Senkondo (kushoto), wakikabidhi kitanda cha kujifungulia kwa ajili ya wanawake wenye ulemavu kwa viongozi wa Hospitali ya Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga mwishoni mwa wiki. Msaada huo ni sehemu ya fedha zilizotolewa na Taasisi ya Nos Vies en Partage (NVeP) inayofadhiliwa na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi Kimara Misale wanufaika mradi maji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HATIMAYE wakazi wa Kijiji cha Kimara Misale, Kata ya Dutumi, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha wameepuka kero ya maji kwa kukamilika kwa mradi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Wakazi hao kwa muda mrefu walikuwa wakitumia maji ya Mto Ngerengere na Ruvu na kusababisha baadhi yao kuliwa na mamba na wengine kupata ulemavu, wanapokwenda kutafuta maji.

Wakizungumza na Nipashe muda mfupi baada ya kukabidhiwa mradi wa maji na RUWASA, walisema awali walikuwa wakitembea umbali wa kilometa mbili hadi tano kufuata huduma hiyo.

Nasra Jafari, aliishukuru serikali kwa hatua hiyo ambayo inawezesha kufanya kazi zao za nyumbani kwa wakati tofauti na zamani walipokuwa wakichelewa kutekeleza majukumu yao kwa kutafuta maji.

Naye Diha Kunga (70), alisema kitendo cha serikali kuwafikishia maji katika kijiji chao kimewasaidia wazee kupata huduma hiyo karibu na wanapoishi bila malipo.

"Hawa RUWASA wametufanyia jambo kubwa tangu kijiji hiki kuanzishwa mwaka huu ndiyo tunapatiwa maji tena sisi wazee tumepata msamaha kila siku tunachota bure hili ni jambo la faraja kwetu," alisema Diha.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya mradi huo, Meneja wa RUWASA, Mhandisi Debora Kanyika, alisema mradi huo umetekelezwa na mkandarasi kampuni ya Buildall Constractors kwa Sh. 498,709,539.89, fedha za UVIKO-19 na wananchi 1,700 watanufaika.

Mhandisi Kanyika alisema mradi huo umehusisha ujenzi wa tangi la juu la lita 50,000 kwenye mnara wa mita 12, vituo vinane vyenye vichotea maji viwili, uchimbaji wa visima viwili katika vitongoji vya Kimara na Kigogo, nyumba ya mashine, ufungaji wa umeme wa jua na uchimbaji ulazaji wa mabomba na ufukiaji wa mtandao wa maji upatao kilomita 8.4.

Alisema kwasasa mradi huo umefikia asilimia 98 na wananchi wanapata maji kwa usimamizi wa Jumuiya ya Watumia maji Kijiji cha Kimara Misale wakati mkandarasi akiwa katika hatua za mwisho.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Salum Mtego, alisema upatikanaji wa mradi huo unawaondoa wananchi kwenye adha ya kutembea umbali mrefu na kuchota maji mto Ruvu.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Kimara Misale, Sudi Omari, alisema wametoa msamaha kwa wazee zaidi ya 40 kupata maji bure ndoo nne kila siku pamoja na wenye ulemavu wawili huku wananchi wengine wakipata huduma hiyo kwa Sh. 100 kwa ndoo tatu.

# Wazazi waelezwa umuhimu kufuatilia wanafunzi kitaaluma

**Na Joseph Mwendapole**

WAZAZI wameshauriwa kufuatilia kwa karibu maendeleo ya watoto wao kitaaluma na tabia ili waweze kufanya vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho na kuwa watu wema kwa jamii.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja Miradi wa Kilua Group, Ammanzy Mohamed kwenye mahafali ya Shule ya Sekondari ya St. Mary's Mbezi Beach, jijini Dar es Salaam.

Alisema wazazi hawapaswi kuwaachia kazi ya kufuatilia mienendo ya tabia na taaluma walimu bali nao wanawajibika kufuatilia kila mara kuangalia kama wanafanya vizuri kitaaluma na wanapogundua mwenendo mbaya watoe taarifa.

Alisema wazazi wanapaswa kutengeneza urafiki wa karibu na walimu wa watoto wao ili wawe wanapata mrejesho wa kinachoendelea badala ya kuwaacha baada ya kulipa ada.

"Nimefurahi kuona vipaji vya aina mbalimbali hapa St Mary's na nina nawapongeza walimu kwa kazi nzuri sana ya kuwalea na kuwafundisha vijana wetu kiasi cha kufanya vizuri kiasi hiki, lakini ninachosisitiza sisi wazazi tushirikiane na walimu kufuatilia tabia za watoto wetu," alisema.

"Kwa maonesho tuliyoona hapa inaonekana hawa wanafunzi watafanya vizuri sana kwenye mtihani wao wa mwisho na nimesikia hapa wanavyozungumza Kiingereza kilichonyooka na Kifaransa kizuri sasa hivi vipaji lazima vifuatiliwe na vilelewe," alisema Ammanzy.

Naye Mkuu wa Sekondari ya Mbezi, Ntipoo Reca, alisema tangu kuanzishwa kwa shule hiyo mwaka 2001 chini ya mwanzilishi wake hayati Dk. Getrude Rwakatare, zimekuwa zikijitahidi kuzalisha wahitimu wenye maadili na walioiva kitaaluma.

Alisema shule hiyo imejitahidi kuweka madarasa ya kutosha ili kuwa na wanafunzi 25 kumwezesha mwalimu kuwa kumfikia kila mwanafunzi wake.

Pia, uongozi wa shule umejitahidi kuweka walimu mahiri na wabobezi wa kutosha kwa masomo wanayofundisha hali ambayo imewawezesha wanafunzi kufanya vizuri kwenye mitihani yao ya kitaifa.

Alisema uongozi wa shule umejitahidi kuweka maktaba kubwa iliyosheheni vitabu kwa wanafunzi wa michepuo yote na maabara kubwa inayowawezesha masomo ya sayansi kwa vitendo.

"Na kwa nidhamu hapa St Mary's tumeweza kwa asilimia kubwa kuwajenga kuwa na nidhamu ya masomo na muda kwasababu wanafuata ratiba zao za masomo za kila siku bila kushurutishwa na mtu na kwenye mtihani wa mwaka huu tuna uhakika wa kutoa daraja la kwanza na la pili tu," alisema Reco.

Naye Ofisa Elimu Kata ya Mbezi Juu, Clarence Makule, alipongeza shule hiyo kwa maendeleo yake ya kitaaluma na kuwataka wasibweteke na mafanikio wanayoyapata kwa kuendelea kuhakikisha wanafunzi wao wanafaulu kwa alama za juu na kushika nafasi za juu kitaifa.

"Walimu wao ni wazuri sana na wengine wamesomea hapa hapa kuanzia shule ya awali na wamefanikiwa kuja kufundisha hapa mimi kama ofisa elimu nawapongeza kwa kazi nzuri ila wasibweteke kwa sababu ushindani ni mkubwa walimu wasome kwa bidii na watimize wajibu wao," alisema.



# UWT Simanjiro wapata Mwenyekiti mpya

**Na Jaliwason Jasson,**
SIMANJIRO

JUMUIYA ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara imempitisha Anna Shinini kuwa mwenyekiti wa jumuiya hiyo.

Katika uchaguzi huo, Anna alipata kura 137 dhidi ya mpinzani wake Agness Brown aliyepata kura 84.

Mwishoni mwa wiki, wajumbe wa CCM Wilaya ya Simanjiro walikuwa wakijiuliza ni nani atakayebeba mikoba hiyo, baada ya uchaguzi wake uliofanyika mwanzoni mwa mwezi huu, kufutwa.

Uchaguzi huo ulifutwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM kutokana na malalamiko ya kugubikwa kwa dosari za wazi.

Kwa mujibu wa Katibu wa UWT, Wilaya ya Simanjiro, Leokadia Fisoo, katika uchaguzi huo uliofanyika juzi wapiga kura halali walikuwa 221, kura mbili ziliharibika.

Fissoo, alisema uchaguzi huo ulirudiwa, baada ya mmoja kati ya wagombea wa nafasi hiyo kukata rufani ngazi ya taifa. Hivyo, malalamiko ya mgombea huyo yalionekana ni sahihi.

Waliokuwa wakiogombea nafasi hiyo ni wale waliopitishwa na Halmashauri Kuu ya CCM, Mkoa wa Manyara, ambao ni Agness Brown, Anna Shinini, Naomi Edward na Rehema Yohana.

**Uchaguzi huo ulifutwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM kutokana na malalamiko ya kugubikwa kwa dosari za wazi.**

# Jaji aona ombwe usimamizi wa makosa ya ujangili

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Tabora, Amour Khamis, amesema kuna ombwe la namna wadau wa haki jinai nchini ambavyo hawasimamii ipasavyo misingi ya maadili ya kazi zao, hasa katika masuala yanayohusu makosa ya ujangili.

Hivyo amewasisitiza majaji, mahakimu, waendesha mashtaka na wapelelezi waandamizi, kuboresha utendaji kazi wao ili kusaidia vita dhidi ya ujangili wa wanyamapori na mazao yake.

Aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya namna bora ya ushughulikiaji wa mashauri ya makosa dhidi ya wanyamapori, ikiwamo ujangili na mazao ya misitu kwa wadau hao.

"Jiwekeeni viwango stahiki vya utoaji huduma, kwa kufanya hivyo mtakuwa mmelinda na kutetea maslahi ya kiuchumi na kuimarisha ulinzi, usalama, amani na utulivu wa taifa," alisema.

Jaji Amour alisema maadili ni nyenzo muhimu katika utoaji huduma bora kwani ni suala mtambuka linalogusa kila hatua ya utendaji wa mnyororo wa haki jinai.

Alisema kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Oktoba 13 mwaka huu na Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori Duniani (WWF), inaonyesha idadi ya wanyamapori duniani imepungua kwa asilimia 69 katika kipindi cha mwaka 1970 hadi 2018, ikiwa ni matokeo ya mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli mbalimbali za kibinadamu.

"Taarifa hiyo inaonesha kuwa idadi ya wanyamapori imepungua na waliopo wamedhoofika kwa ubora kutokana na kuharibiwa kwa mifumo asilia ya ardhi na bahari, uvunaji uliopitiliza wa wanyama na mazao ya misitu na mabadiliko ya hali ya hewa,"alisema.

Kadhalika alisema taarifa iliyotolewa na Taasisi ya Utafiti waa Wanyamapori (Tawiri), inaonyesha kati ya mwaka 2009-2014, idadi ya tembo ilipungua kutoka 109,051 hadi 43,521 sawa na asilimia 60.

Pia alisema kupungua kwa wanyamapori nchini kulichagizwa na udhaifu wa usimamizi wa mipaka, sheria dhaifu za kusimamia wanyamapori, adhabu ndogo zilizokuwa zinatolewa kwa makosa ya wanyamapori, udhaifu wa vyombo vya kusimamia sheria za wanyamapori na uwapo wa rushwa.

Aidha alisema takwimu hizo zinaonyesha kuwa uhifadhi wa wanyamapori na misitu ya asili vipo hatarini na hivyo inahitajika mipango na hatua madhubuti za kukabiliana na hali hiyo na kuwa vita dhidi ya makosa ya wanyamapori ni ya jamii yote.

"Ni muhimu kwetu kuendelea kushirikiana kama wadau katika harakati za mapambano dhidi ya makosa hayo, wote tufanye kazi zetu ipasavyo na kusimamia misingi ya katiba, sheria na taratibu na hivyo kutoa maamuzi ya haki bila kumuonea mtu yeyote,"alifafanua.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Joachim Tiganga, alisema mafunzo hayo yametolewa kwa wakati muafaka, suala la uhifadhi ni moja ya vipaumbele vya taifa na yatasaidia kuongeza ufanisi kwa kiasi kikubwa kwao kuanzia namna bora ya uendeshaji na upelelezi wa mashauri hayo.

"Mnaona namna ambavyo serikali inawekeza kwa kiasi kikubwa sana kwenye utalii na hakuna uhifadhi hakuna utalii, sisi kama wadau tumeweza kukaa pamoja kuwa na uelewa wa pamoja,"alisema.

Mkuu wa mashtaka Mkoa wa Mara, Valence Mayenga, alisema mafunzo hayo yamekuwa nyenzo muhimu kwao hasa katika kulinda rasilimali za taifa, hifadhi na wanyamapori na kuwa wamekumbushana juu ya mbinu bora za upelelezi, uendeshaji wa mashauri na uandishi wa hukumu kwa majaji na mahakimu ambao wanatoa uamuzi.



Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Simanjiro, Mkoa wa Manyara, Anna Shinini (wa pili kulia), akionyesha bango la namba yake kabla ya kushinda nafasi hiyo juzi kwa kura 137 dhidi ya kura 84 za Agnes Brown (kulia). **PICHA: GIFT MY THADEY**

# Tanga, Arusha tishio matukio ya ukatili wa kijinsia

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imesema takwimu mpya za masuala ya ukatili wa kijinsia nchini zinaonyesha kuwa mikoa ya Arusha na Tanga ni tishio kwa matukio hayo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Amon Mpanju, aliyasema hayo wakati wa kilele cha kampeni ya ukeketaji iliyofanyika Mandi Wilaya ya Babati mkoani Manyara.

Alisema kuwa mikoa hiyo inafuatiwa kwa karibu na Ilala na Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Mpanju alisema Arusha ndiyo kinara ikiwa na matukio 4,320, Ilala matukio 2,680, Tanga matukio 2,257 na Kinondoni matukio 1,985.

"Kwa ujumla wake huo, utaona kwamba kati ya Januari hadi Desemba mwaka jana, matukio 29,373 ndiyo yaliyoripotiwa, yakiongozwa na matukio 6,305 ya ubakaji nchi nzima.

Matukio yaliyoripotiwa katika vyombo vya dola, yakigawanywa kwa kila mkoa, utakuwa na zaidi ya matukio 500 kwa mwaka.

"Hizi takwimu ni za kutisha. Ni lazima serikali ichukue hatua, hatuwezi kukubali hali hii iendelee watu wateswe kwa kufanyiwa ukatili," alisema.


Aidha, alisema kwa kipindi hicho yalitokea matukio 5,751 ya ukatili mwingine, akisisitiza matukio 4,108 yalikuwa ya ukatili wa kudhuru mwili.

Kuhusu ukatili wa watoto, Naibu Katibu Mkuu huyo, alisema ukatili kwa watoto kuliripotiwa matukio 11,499 na kati hayo matukio ya ubakaji, yalikuwa 5899, ulawiti 1,114 na watoto waliopata ujauzito walikuwa 1,677.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Lazaro Twange, alisema takwimu zinazotolewa kuhusu ukatili kwenye mkoa huo zinawaumiza viongozi, siyo kwamba wanazifurahia.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA), Dk. Majaliwa Marwa, alisema shirika hilo lipo kwa zaidi ya miaka 40 hapa nchini na wanahakikisha kila mama anajifungua salama.

Dk. Marwa, alisema ukeketaji ni kitendo kinachomwondolea mwanamke utu wake, akisema kwamba UNFPA itaendelea kuisaidia mikoa, ambayo inaongoza kwa ukeketaji ambayo ni Manyara, Mara, Singida, Dodoma na Arusha.





## Wafugaji waliokaidi kuvalisha hereni mifugo kutambuliwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda amesema serikali inamkakati wa kufanya operesheni maalum ya kuwatambua wafugaji ambao wamegomba kuivalisha hereni mifugo yao.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Jiji la Arusha, akizindua kazi ya uwekaji wa hereni hizo kwa njia ya kielektroniki.

Mtanda alisema wafugaji waliokaidi agizo hilo wana nia ovu ya kukwamisha mikakati iliyowekwa na serikali.

Mtanda, alisema mifugo iliyopo katika Jiji hilo kwa sasa ni 16,262, katika uzinduzi huo mifugo 7,000, ndiyo iliyowekwa hereni.

"Lengo kubwa la serikali kuagiza haya yafanyike ni kwa sababu tunataka pale mifugo inapopotea au kuibiwa, ukiingia kwenye kompyuta ijulikane ilipo na kumsaidia mfugaji kupata mifugo yake kirahisi.

"Jitokezeni kuweka hereni mifugo yenu na gharama zake ndogo kwa sababu mifugo mikubwa imegharimu shilingi 1,750 kwa mfugo mmoja, na mtoto ni shilingi 1000." alisema.

Pia alimwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Hargeney Chitukulo na Idara ya Mifugo na Kilimo, kuhakikisha mifugo yote ya jijini humo inawekewa hereni.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji hilo, Chitukulo, alisema Arusha una ng'ombe 10,898, punda 1,201, kondoo 4,163, ambao kati yao ng'ombe 5,000 na mbuzi na kondoo 2,000 imewekewa hereni.

Alisema wafugaji watanufaika na uwekaji huo wa hereni kwa sababu zina alama za kipekee na pale mfugaji atakapoibiwa mfugo wake, itaonekana kwenye mtandao ulipo.

Alisema: "Wafugaji wote wa Jiji hili, nawaomba mhakikishe mnaleta mifugo yenu kuwekwa alama hii ya kielektroniki ili iwaepushe na wizi na kuisaidia serikali kuitambua mifugo iliyopo kwa njia hii".

# DC aagiza TFS, TAKUKURU kuwabaini wanaovuna miti

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

MKUU wa Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, Siriel Mchembe, ameagiza Wakala wa Misitu (TFS) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuanza kuwachunguza wafanyabiashara mbao wanavuna miti na wanaojihusisha na uchomaji mkaa.

Amesema pindi watakapowakamata wapelekwe mbele ya vyombo vya sheria, kujibu sababu za kuihujumu serikali.

Alitoa agizo hilo jana alipokwenda kukagua shughuli za uhifadhi wa misitu katika Kata ya Kang'ata, ambako ni eneo tishio kwa uchomaji wa mkaa.

"Wenyeviti wote wa vijiji ninyi ni vinara wa kula rushwa. Nawaonya kwa mara ya mwisho acheni kushiriki kuhujumu misitu ya hifadhi, acheni kuruhusu watu kuvuna miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

"Tutaendelea kuonana wabaya, kwa sababu kila unapopita wanakwambia tumepewa kubali na Mwenyekiti wa Kijiji. TFS mpitie vibali vyote tulivyovipitishwa mwezi uliopita, vya kuruhusu uvunaji wa misitu ili wenye vibali vyao wajiridhishe kwamba wenyeviti wa vijiji, wamewapa vibali halali au maombi halali. Na taarifa hiyo ipitiwe na TAKUKURU."

Ofisa Mazingira wa Halmashauri hiyo, Zawadi Waziri, alisema ili kunusuru misitu kwa hatua za awali vibali vyote vya uvunaji misitu visimamishwe na kuanza kukaguliwa upya.

"Kwa jinsi uharibifu ulivyotokea, ingependeza kamati ya wataalamu ifanye uchunguzi wa kina na ikiwezekana hata vibali hivi vinavyotolewa vya uvunaji wa misitu visitishwe, kwa sababu uharibifu ni mkubwa na hali ya hewa inazidi kubadilika.

"Kipindi hiki mvua zilitakiwa ziwe zimeanza kunyesha, lakini yote hii inatokana na uvunaji ambao nafikiri wakati mwingine tunashindwa kufanya ufuatiliaji na kujiridhisha kiwango kinachotakiwa kuvunwa kwenye misitu ambayo imepewa vibali."

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Kata ya Kang'ata, Ahmad Magalu, alisema chama hicho kitaangalia hatua za kuwachukulia wenyeviti wote watakaobainika kushiriki kuhujumu misitu hiyo.

"Sisi watu wa chama kwasababu tumewapa dhamana wasimamie vizuri, utaratibu wetu Mwenyekiti wa Kijiji kazi yake ni kusimamia mali za wananchi lakini kwa hali hii inaonekana kabisa ameshindwa kusimamia, tunapatwa na ukame katika vijiji na kata kwa ujumla," alieleza Magalu.

Hivi karibuni Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ilikamata magunia ya mkaa zaidi ya 1,000 katika Kijiji cha Lugala kilichoko Kata ya Kitumbi.



Ofisa Mwandamizi wa Maendeleo ya Biashara wa TADB, Grayson Ferdinand, akieleza huduma zinazotolewa na benki hiyo kwa wananchi waliotembelea banda la benki hiyo katika maonesho ya sita (6) ya ufugaji wa kuku na ndege wafugwao yaliyofanyika wikiendi iliyopita ukumbi wa Kilimanjaro B-Ubungo Plaza jijini Dar es Salaam. TADB imetoa Sh. bilioni 13.5 kwenye ufugaji wa kuku nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi waandika barua kuwaonya maofisa kuacha rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Sikirari wilayani Suha wameandika barua ya kuwaonya maofisa wa taasisi za serikali kuacha tabia ya kutumia vyeo vyao kuomba rushwa ya ngono ili waweze kutoa huduma.

Wanafunzi hao wameandika barua ya wazi kwa umma, wakiwaonya maofisa wa taasisi wa serikali kuacha tabia hiyo, wakisema kwa kuwa kufanya hivyo ni kuchochea ongezeko la matukio ya ukatili nchini.

Kwa mujibu wa Kiongozi wa Klabu ya Sauti Yangu, Nguvu Yangu ya Shule hiyo, Michael Issaya, katika barua hiyo wanafunzi hao pamoja na mambo mengine wameshauri wenye mamlaka kuweka madawati ya ukatili wa kijinsia ili kukabiliana na vitendo hivyo. Sehemu ya barua hiyo inasema: "Enyi wenye mamlaka katika taasisi mbalimbali za kiserikali, msitumie vyeo vyenu vibaya kwa kuomba rushwa ya ngono ndipo mtoe huduma kwani kufanya hivyo ni ukatili wa kijinsia.

"Enyi madereva bodaboda, fanyeni kazi yenu kwa maslahi mapana ya kuzitafutia familia zenu riziki. Achaneni na zile tabia za kuwadanganya mabinti kwa kuwapa lifti na kuwanunulia chipsi kwa mangi; mwisho muwabebeshe vitumbo visivyolingana hata na umri wao. Jueni kuwa sheria ni msumeno na haichagui pa kukata."

Kuhusu mangariba wanaofanya kazi ya ukeketaji kwa usiri wanafunzi wa shule hiyo wameonya wakieleza: "Nanyi mangariba, ninyi mmekuwa mkiendekeza mila na desturi potofu za kuwakeketa wanawake, eti kwa lengo la kuonyesha kuwa wameshakua na wanastahili kuolewa.

"Leo ngoja niwape darasa, eleweni kuwa mnapowakeketa mnasababisha maambukizi ya magonjwa kama UKIMWI na magonjwa mengine, kama vile kaswende na homa ya ini, kwa kuwa huwa mnatumia wembe au kisu kimoja katika kuwakeketa."

Mradi wa Jamii Salama kwa Maendeleo Yetu, Sauti Yangu, Nguvu Yangu, Tupinge Ukatili wa Kijinsia, unatekelezwa na Shirika la KWIECO katika vijiji 12, kwa ufadhili wa Taasisi ya Kimataifa ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom (FNF).

Vijiji vinavyonufaika ni Donyomoruwa, Orkolili, Kilingi, Ngumbaru, Fuka, Koboko Kusini, Embukoi, Lekrumuni, Magadini, Namwai, Gararagua na Mlangoni.

Akizungumza na wananchi na wanafunzi hao, Mratibu wa Mradi huo, Elizabeth Mushi, alisema vilio vya wanawake kwa miaka mingi viliishia mikononi mwa mila na desturi potofu.

Alisema mila hizo zilizowakandamiza na kuwatumia wanawake kama nyenzo ya kupata mali katika jamii, pia zilitumika kuwashurutisha kuolewa ili wazazi waweze kupata mahari, kwa ajili ya kuendesha maisha yao.

Nipashe

# Spotika



**KLABU 5 ZENYE THAMANI KUBWA DUNIANI KWA SASA**



# TIK-TAKA...

Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Neymar, akibinjuka 'tik-taka' kujaribu kufunga kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Benfica iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1 Jumanne iliyopita. Bao la PSG lilifungwa na Lionel Messi dakika ya 22 baada ya kupokea pasi ya mwisho kutoka kwa Neymar huku lile la wenyeji likitiwa kambani na Danilo Pereira aliyejifunga dakika ya 41.
**PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE


MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Mnorway Erling Haaland, ana wastani wa kufunga bao kila baada ya dakika 48, ambao ndio wastani wa juu zaidi kwa mchezaji katika historia ya Ligi Kuu England. Kasi hiyo inamfanya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pep Guardiola kujenga matumaini kuwa mabao ya Haaland yanaweza kumsaidia kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.



# FARASI WATATU WANAOWEZA KUSHANGAZA KOMBE LA DUNIA

Huku Kombe la Dunia likikaribia, makala haya yanaangazia nchi chache ambazo huenda zikaibuka kama farasi wa kushangaza katika Kombe la Dunia la nchini Qatar...

> Hata hivyo, ubora wao unaweza kuwafanya kuwa timu ya kwanza ya Afrika kutinga hatua ya nusu fainali wakati huu.
>
> **Aliou Cissé**
> **Senegal**



**DOHA, Qatar**

KOMBE la Dunia la FIFA 2022, linaanza Novemba 20 nchini Qatar mwaka huu, huku msisimko wa mashindano hayo makubwa zaidi ya soka duniani ukiongezeka. Kwa sasa, makocha wa timu za taifa wanakamilisha mbinu zao na muda kutangaza vikosi vyao unakaribia.

Timu pendwa tayari ziko kwenye midomo ya kila mtu. Wachezaji wa Brazil na Ufaransa wana ubora wa hali ya juu na wanaweza kuwa washindi.

Hata hivyo, Kombe la Dunia limekuwa na mambo ya kushangaza kwa siku za nyuma. Mwaka 2010, Ghana walikuwa midomoni mwa kila mtu, hii ni baada ya 'Black Stars' hao kukosa nafasi ya kutinga nusu fainali kwa mikwaju ya penalti.

Mwaka 2014, Costa Rica walikuwa timu iliyoshangaza kwenye shindano hilo. Kwanza, waliongoza kundi lao lilikuwa likiundwa na Italia, England na Uruguay na kutinga robo fainali. Mwaka 2018, Croatia iliibuka kama timu nyingine ya kushangaza na kutinga fainali kwa mara ya kwanza katika historia yao.

Huku Kombe la Dunia likikaribia, makala haya yanaangazia nchi chache ambazo huenda zikaibuka kama farasi wa kushangaza katika Kombe la Dunia la nchini Qatar.

**#1. Denmark**

Denmark walikuwa farasi wa kushangaza katika mashindano ya Ulaya mwaka jana. Onyesho lao la kuvutia liliwafanya kutinga nusu fainali, na kuzidiwa kwenye penalti ya utata ya Harry Kane. Denmark wanaweza kuwa farasi wa kushangaza tena wenye ubora sawa katika kikosi kinachoelekea Kombe la Dunia.

Upande wa Denmark kwa sasa uko katika nafasi ya 10 katika viwango vya FIFA, na ndivyo ilivyo. Waliongoza kundi lao la kufuzu, wakipoteza mchezo mmoja pekee. Walimaliza wa pili, nyuma ya Croatia, licha ya kuwafunga Ufaransa 2-0 katika mechi yao ya mwisho.

Mara ya mwisho, Croatia iliiondoa Denmark katika michuano hiyo katika raundi ya pili kwa mikwaju ya penalti.

Mwisho wao bora zaidi kwenye Kombe la Dunia ulikuwa mwaka 1998 wakati Brazil walipowatoa katika hatua ya robo fainali.

**#2. Senegal**

Mabingwa wa Afrika wameorodheshwa katika nafasi ya 18 katika viwango vya ubora duniani. Ushindi wao maarufu dhidi ya Ufaransa mwaka wa 2002, unachukuliwa kuwa moja ya mishtuko mikubwa katika historia ya Kombe la Dunia. Hii ni mara ya tatu tu kwa Senegal katika mashindano haya. Mwonekano wao mwingine ulikuwa 2002 na 2018.

Wakiwa na Sadio Mane na Edouard Mendy, Senegal inaweza kuibuka kama moja ya farasi wa kushangaza. Mara ya mwisho, walitolewa nje ya hatua ya makundi na kuruhusu Japan kufuzu mbele yao.

Hata hivyo, ubora wao unaweza kuwafanya kuwa timu ya kwanza ya Afrika kutinga hatua ya nusu fainali wakati huu.

Waliongoza kundi lao katika hatua ya awali ya mchujo kabla ya kuifunga Misri na kufuzu kwa mashindano hayo. Walikabidhiwa kundi gumu na wenyeji, Qatar, Uholanzi na Ecuador.





Baadhi ya nyota wanaounda kikosi cha Senegal.

**#3. Uholanzi**

Timu ya Taifa ya Uholanzi haikuwapo katika michuno ya mwaka 2018. Mwonekano wao wa mwisho, mwaka 2014 ulikuwa wa kukumbukwa walipomaliza wa tatu kwenye shindano hilo.

Wanaongozwa na mtu yule yule aliyewapeleka kwenye Kombe lao la Dunia, Louis Van Gaal. Mtaalamu huyo mwenye umri wa miaka 71, atakuwa na nia ya kuipeleka nchi yake zaidi wakati huu.

Uholanzi haijafungwa tangu Van Gaal arejee kwenye kikosi na wametoka sare michezo minne pekee. Waliongoza kundi lao la Ligi ya Mataifa ya Uefa, wakiishinda Ubelgiji nyumbani na ugenini. Kwa sasa, wako katika nafasi ya nane duniani kwenye viwango vya ubora.

Uholanzi imekuwa katika fainali ya Kombe la Dunia mara tatu na kupoteza zote tatu. Mwaka 2010, walichapwa na Hispania 1-0.

Hata hivyo, kwa ubora wa timu hii katika maeneo yote, wakiwa na wachezaji kama Virgil Van Dijk, Memphis Depay, na Frenkie De Jong, wanaweza kutwaa taji hilo kwa mara ya kwanza katika historia ya taifa hilo.

## MAKALA BONGO

MSAADA

# USIYOYAJUA KUHUSU MWAMUZI BORA WA NGUMI, PENDO NJAU



Mwamuzi Pendo Njau akimpa msaada wa kwanza bondia Mmexico, Allan Pina, baada ya kupokea konde zito kutoka kwa Ibrahim Class hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

**Na Saada Akida**

UNAPOZUNGUMZIA sekta ya masumbwi nchini, itashangaza sana kama hutalitaja jina la Pendo Njau, mwamuzi nguli anayejizolea umaarufu mkubwa kutokana na rekodi yake nzuri na ya kuvutia katika uchezeshaji wa mapambano makubwa Tanzania.

Safari yake katika masumbwi haikuwa rahisi kama mwanamke tangu awali, kwani jamii ilimshangaa kutokana na walio wengi kuamini mchezo huo ni wa wahuni tu na unawahusu zaidi wanaume.

Pendo ambaye ni mama wa watoto wawili ndiye mwamuzi bora wa kike kutoka ukanda wa Afrika anayechezesha mchezo wa ngumi na katika kulitambua hilo, Nipashe lifanya mahojiano maalum naye ili kuujuza umma na zaidi kuhamasisha wanawake kuupenda mchezo huo.

**Historia yake katika ngumi**

Pendo anasema aliwahi kucheza ngumi kwa kiwango kikubwa hadi kuwa bingwa wa World Kickboxing Network (WKN), mchezo wa ngumi na mateke ambao makao makuu ya mchezo huo yako Ufaransa.

"Baadaye nilishiriki mashindano ya Afrika ya Kati kwa kumchapa mdada kutoka Kenya, nilimpiga kwa pointi.

"Nilicheza pambano madogo madogo na mwaka 2017 nikacheza pambano la mwisho la ngumi ambalo nilishinda kwa TKO raundi ya tatu kwa kumpiga mwanadada Amina (sikumbuki jina lake la pili), hapo ilikuwa mwisho wangu wa kucheza ngumi," anasema Pendo.

Anasema kipindi anakumbuka alicheza mechi tatu tu baada ya hapo akaachana na kupanda ulingoni kuzipiga.

"Baada ya kuachana na kupigana ngumi nikajikita katika mchezo wa Kickboxing kwa mafanikio makubwa kama nilivyokwambia awali, niliwahi kuwa bingwa wa WKN na mashindano ya Afrika," anasema mwamuzi huyo wa ngumi.

Anasema aliamua kujikita zaidi kwenye ngumi badala ya michezo mingine kutokana na kuupenda sana mchezo huo lakini anaamini ni kipaji chake hali ambayo imemfanya awe imara zaidi hadi sasa kufika kuchezesha mapambano makubwa bila kutetereka.

"Huu mchezo ninaupenda sana na kipaji changu kwa sababu nilifanya vizuri kipindi nacheza tena kipindi hicho wanawake hawakuwa wengi katika huu mchezo na kucheza na wanaume ambao wamenipa ukomavu hadi nakuwa mwamuzi," anasema Pendo.

**Changamoto kwa wazazi**

"Niliwaficha wazazi wangu kuhusu kujihusisha na ngumi, nilikuwa namuogopa sana baba yangu hakupenda ugomvi na mtaani walimpa jina la 'Mwendapole' na alikuwa mzee wa kijiji kutokana na kuitumikia jamii.

"Alikuwa mzee wa kanisa, lakini mpole sana kwa hali hiyo sikupenda afahamu hilo, kwa mama haikuwa shida kwa sababu alikuwa shujaa sana na alikuwa tayari kupambana na kila mtu," anasema Pendo.

Anasema anaamini ushujaa wake ni urithi kutoka kwa mama yake mzazi kwa sababu anajiamini kwamba ni shujaa wa Tanzania, Afrika na hata katika rekodi ya dunia.

**Ngumi karithi kwa nani**

"Katika familia yangu hakuna mtu aliyekuwa anajihusisha na ngumi hapo awali, ila kaka yangu alikuwa anacheza sarakasi," anasema Pendo.

Anasema kwa sasa mtoto wake wa kike Jesca anajihusisha na mchezo huo na anaamini mwanawe huyo amerithi ujasiri ambao alikuwa nao kipindi akianza ngumi.

**Unyanyasaji kijinsia**

Pendo anasema Waafrika tunaitikadi ambazo hajui ni lini zitaisha. "Nimewahi na naendelea kukutana na changamoto hiyo ya unyanyasaji wa kijinsia, lakini napambana nazo kutokana na ujasiri wangu.

"Wakati nacheza na hadi sasa nakutana na changamoto hiyo, ila nasimamia maneno ya kocha wangu kwa sasa ni meneja anayesimamia kazi zangu Kaseba (Japhet), aliwahi kuniambia nimeingia kwenye huu mchezo nitakutana na vikwanzo vingi ikiwamo kijinsia, sitakiwi kuvikimbia bali nipambane na changamoto hizo."

Anasema anamshukuru kocha wake Kaseba maana hadi sasa anapambana na changamoto hiyo ya unyanyasaji kwa sababu anachokifanya ni kwa ajili ya maisha yake lakini kwa ajili ya taifa.

**Maisha ya ndoa**

"Nina watoto wawili, sijaolewa ila ninaishi na mume wangu...muda wowote mtasikia harusi yangu na kumuona mume wangu, Kaseba si mume wangu ni meneja na bosi wangu amenifundisha kutafuta hela.

"Huyu Pendo unayemwona hapa bila Kaseba nisingekuwa refa ambaye nchini inajivunia kuwa naye, amekuwa akinifundisha nidhamu katika kazi," anasema.

Pendo anasema hajawahi kuwa na uhusiano na meneja wake huyo kwa sababu Kaseba ameoa na ana watoto.

**Ratiba ya ngumi na familia**

"Kitu kidogo sana...mambo ya kutenga muda kwa ajili ya mazoezi, watoto na familia kwa mwanamke ni jambo dogo sana kwa sababu mwanamke ana uwezo wa kufanya kazi nyingi kwa kujitengea muda wa kutosha.

"Ninatumia muda wa asubuhi kwenda mazoezi baadaye kazini na kama unavyoona niko nyumbani nafanya kazi zangu na pia napata muda wa kuongea na majirani zangu," anasema mwamuzi huyo.

**Mafanikio kazini**

Anasema mafanikio ni makubwa kwani amekutana na watu mbalimbali na kufanikiwa ni lazima ukubali na upambane na changamoto zitakazojitokeza mbele yako.

"Nimeweza kupambana nazo na kupata mafanikio makubwa ikiwamo kuwa katika rekodi ya kuwa refa bora wa kike Afrika katika mchezo wa ngumi," anasema Pendo.

**Ndoto zake**

Pendo anasema ndoto hubadilika na kuja kuwa kweli, ila mafanikio kuja yanakuwa machache. "Ndoto zangu ni kuona ngumi Tanzania zinakuwa kubwa zaidi pia Kickboxing kutaka kuifufua na kuwa bora.

"Ninaamini hapa nchini kuna vijana wengi wanacheza Kickboxing, lakini huo mchezo umekufa na sasa tuko katika mchakato wa kuufufua.

"Ndoto zangu pia ni kufikisha ngumi katika daraja kubwa na sasa tunaona jinsi gani wadhamini wanajitokeza."

**Ushauri kwa wazazi**

"Wazazi wanapaswa kuangalia vipaji vya watoto wao na kuvitunza kwa kuwatengenezea mazingira mazuri kwa kile wanachopenda kukifanya.

"Tusipowatunza tunapoteza vipaji katika kujenga taifa letu kwenye sekta ya michezo. Nafurahi kwa miaka hii kuona wanawake wanajikita katika mchezo huu.

"Ukiangalia kwa sasa Fatma Dewji alivyojitolea na kujikita katika ngumi hii inaleta hamasa kwa watoto wa kike ambao wanavipaji vya mchezo huu," anahitimisha Pendo.

## NJE YA UWANJA




DROO ya awamu ya pili ya (raundi ya 32) kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika itafanyika kesho, Jumanne jijini Cairo, Misri. Droo hii hujumuisha timu zilizotelewa Ligi ya Mabingwa raundi ya kwanza na zile za Kombe la Shirikisho zilizofuzu raundi hiyo.




# KLABU 5 ZENYE THAMANI KUBWA DUNIANI KWA SASA

**MADRID, Hispania**

MCHEZO wa soka umeshuhudia baadhi ya klabu za juu zikifurahia mafanikio mengi kwa miaka mingi. Si tu ubora wa wachezaji bali pia miundombinu na uwezo wa klabu hizo kufika sehemu yoyote duniani na vitu hivyo ndio vinazifanya kuwa kubwa.

Licha ya janga la Covid-19, timu za juu hazijaruhusu kuathiri kimo chao na zimekaa na misuli yao ya kifedha. Ni moja ya sababu kwa nini mchezo huo unabaki kuwa moja ya mchezo wenye fedha zaidi duniani.

Hakuna mtindo maalum linapokuja suala la kutathmini thamani ya klabu ya soka. Ikizingatiwa jinsi timu tofauti zinavyoendeshwa na wanunuzi wao, inakuwa ngumu zaidi kukamilisha thamani yake halisi.

Jarida la Biashara la Marekani la Forbes wiki iliyopita lilikuja na orodha ya klabu zinavyothaminiwa zaidi kwa kutumia mbinu zao maarufu za mapato na matumizi. Bila kuchelewa zaidi, hebu sasa tuangalie klabu tano za juu zenye hadhi ya juu na kifahari...

#5. Bayern Munich (Dola bilioni 4.28)

Huwezi kuamini jinsi Bayern Munich ilivyotawala kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, karne hii. Kati ya mataji yao 32 ya ligi, 16 yamekuja katika karne ya 20 huku 'Bavaria' hao kwa sasa wakiwa katika mbio za kuwania taji kwa mara ya 10 mfululizo kwenye ligi.

Uchezaji wao umekuwa wa kuvutia macho ndani na nje ya uwanja kwani wanasalia kuwa klabu yenye thamani zaidi (dola bilioni 4.28) duniani kwa sasa. Bayern Munich wameingia kwenye orodha hiyo kwa tofauti ndogo baada ya kuipiku Manchester City inayoshika nafasi ya sita, ambayo thamani yake ni dola bilioni 4.25.

Thamani ya Bayern imeongezeka kwa asilimia moja tangu mwaka jana, kwani walipata mapato ya dola milioni 726. Huku dola bilioni 1.6 na dola bilioni 1.8 zikipatikana kutokana na haki za utangazaji na kibiashara.

**#4. Liverpool (Dola bilioni 4.45)**

Liverpool wamepata mafanikio mengi chini ya usimamizi wa kocha wao mahiri, Jurgen Klopp. 'Wekundu' hao msimu uliopita walikaribia kushinda taji lao la pili la Ligi Kuu chini ya Mjerumani huyo kabla ya kuzidiwa kete na Manchester City.

Lakini klabu hiyo ya Merseyside inatafuta kufanya marekebisho katika msimu wa 2022-23. Nje ya uwanja, Liverpool wamefanya kazi nzuri kwa kuingiza mapato ya uendeshaji ya dola milioni 104 na kufanya uwekezaji mzuri katika dirisha la uhamisho.

Ikiwa na thamani ya dola bilioni 4.45, Liverpool wameshuhudia thamani yao ikiongezeka kwa asilimia tisa kutoka mwaka jana. Wekundu hao wanabaki kuwa klabu ya pili kwa thamani kubwa nchini England na hakika hawako mbali na wapinzani wao Manchester United.

**#3. Manchester United (Dola bilioni 4.6)**

Mambo hayajakuwa rahisi kwa shabiki yeyote wa Manchester United tangu kustaafu kwa Sir Alex Ferguson. Klabu hiyo inaonekana kupoteza utambulisho wake na utawala katika miaka michache iliyopita kutokana na misukosuko uwanjani.

Licha ya hayo, United wanabaki katika hali nzuri linapokuja suala la uthamani wao. Wakimilikiwa na familia ya Glazer yenye maskani yake nchini Marekani, wababe hao wa Ligi Kuu England wamekuwa wazuri na nguvu zao za kibiashara.

Kwa mapato ya uendeshaji ya dola milioni 128 na dola milioni 663, Manchester United ina thamani ya dola bilioni 4.6. Baada ya kuona ongezeko la asilimia 10 katika hesabu yao, 'Mashetani Wekundu' hao wanabaki kuwa klabu yenye thamani zaidi nchini England na inatumainiwa hivi karibuni itarejea katika njia zake za ushindi chini ya kocha, Erik ten Hag.

**#2. Barcelona (Dola bilioni 5)**

Limekuwa jambo la kushangaza ndani na nje ya Barcelona huku klabu hiyo ikiwa haina hali nzuri ya kifedha. Huku wababe hao wa Hispania wakichagua viboreshaji vya kiuchumi msimu huu wa majira ya joto, wameweza kupunguza deni lao.

Ukweli ni kwamba, Barcelona bado wapo kwenye hatari kubwa ya kuporomoka kiuchumi, lakini inaonekana "kamari" iliyochezwa na rais, Joan Laporta inakwenda vizuri. Pamoja na yote, klabu hiyo ya Katalunya inabaki kuwa moja ya klabu kubwa zaidi duniani.

Licha ya matatizo yao, Barcelona thamani yao imeongezeka kwa asilimia tano tangu mwaka jana na thamani yake inafikia dola bilioni tano. Ingawa juhudi nyingi zitahitajika ili kuwaondoa katika deni lao, kwa hakika ni kazi inayoweza kufikiwa.

**#1. Real Madrid (Dola Bil 5.1)**

Real Madrid walikuwa na kumbukumbu nzuri msimu uliopita waliposhinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Sifa nyingi zimwendee Karim Benzema kwa hilo kwani mabao yake ya wakati muafaka yalikuwa na jukumu muhimu katika ushindi wao.

Mafanikio hayo yaliimarisha thamani ya Madrid kwani sasa thamani yao imeongezeka kwa asilimia saba zaidi ya mwaka jana. Ikiwa na thamani ya dola bilioni 5.1, hakuna klabu ya soka iliyo katika daraja moja 'Los Blancos' hao kwa sasa.

Kupitia njia zao za utangazaji na kibiashara, Real Madrid walipata dola bilioni 2.2 na bilioni 1.9. Haishangazi ni kwa nini wababe hao wa Hispania wana sauti kubwa kibiashara na wanatawala katika mbinu zao kwenye soko la uhamisho.

Real Madrid

## Nukuu

"Je, walimfanya ahisi kama klabu ndio kitu muhimu zaidi au walimfanya ajisikie kuwa muhimu zaidi kuliko klabu? Lakini kuna kitu ambacho ni kikubwa kuliko kitu kingine chochote nacho ni klabu. Nitatumia hadithi yangu mwenyewe. Sikupenda kucheza nafasi ya winga nikiwa Barcelona. Nilichukia, lakini nilifanya hivyo kwa ajili ya timu," **Nyota wa zamani wa Arsenal na Barcelona, Thierry Henry akimchana Kylian Mbappé kwa kujiona ni zaidi kuliko PSG.**



"Mimi ni muumini sasa. Tumewaona wakipanda mara nyingi zaidi ya miaka 10, kila mara unahitaji kuwa na sura nyingine na sura nyingine. Lakini mchakato anaouzungumzia Mikel Arteta kwa miezi 12-18 iliyopita ni kuanza kuzaa matunda na waona wakiwa na nafasi ya ubingwa Ligi Kuu England," **Nyota wa zamani wa Chelsea na Liverpool, Joe Cole akiamini Arteta ataipa ubingwa Arsenal msimu huu**




"Tukiwa na Mane (Sadio), safu ya ushambuliaji ya Bayern inakosa uwiano kila mara. Kila mtu anaweza kuliona hilo. Matokeo: Ni mwanzo mbaya zaidi kwa msimu huu tangu 2010. Mane hahusiki peke yake, lakini anabeba sehemu ya lawama. Mane ni mtembezaji uwanja ambaye hafiki kamwe. Na imekuwa hivi wakati wote, lakini hakuna anayesema kwa sauti: Mane kwa Lewandowski ni nani hasa alikuja na upuuzi huu? Anacheza tu kwa sababu Serge Gnabry na Kingsley wana matatizo," **Mwandishi na mchambuzi wa soka Ujerumani, Alex Steudel.**



# WACHEZAJI 6 WALIOTUPIA PENALTI 7 LIGI KUU BARA



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, akifunga bao la tatu kwa mkwaju wa penalti kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa kwenye raundi ya saba, jumla ya penalti 12 zimepatikana kabla ya mechi ya jana kati ya Ihefu na Dodoma Jiji, huku saba zikiwekwa wavuni na tano zikiota mbawa.

Kiungo raia wa Cameroon, Moubarack Amza wa Coastal Union ndiye anayeongoza kwa kufunga penalti nyingi, akiwa ametupia mbili mpaka sasa. Amza ndiye mchezaji wa kwanza kufunga penalti kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Katika makala haya tumekukusanyia mabao yote saba ya penalti yaliyopatikana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, wachezaji waliokwamisha wavuni na mazingira yaliyosababisha zipatikane, haya sasa...

**#1. Moubarack Amza (Coastal vs KMC)**

Ilikuwa ni Agosti 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, penalti ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ilipofungwa.

Ilikuwa ni mechi kati ya wenyeji Coastal Union waliokuwa wakiutumia uwanja huo kupisha matengenezo ya Uwanja wa Mkwakwani Tanga, dhidi ya KMC. Wenyeji walishinda kwa bao 1-0 lililotiwa kimiani na Amza kwa mkwaju wa penalti dakika ya 37.

Ilipatikana baada ya Ibrahim Ame kushika mpira kwenye eneo la hatari, mwamuzi akitafsiri kuwa mkono wa beki huyo haukuwa kwenye eneo lake la asili, badala yake alikuwa ameitanua kwa ajili ya kuuzuia mpira.

**#2. Clatous Chama (Simba vs Geita)**

Clatous Chama aliifungia Simba bao la mkwaju wa penalti kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Geita Gold Agosti 17 siku hiyo hiyo ambayo Moubarack Azam alifunga.

Hata hivyo, Chama alifunga dakika ya 81, na Azam dakika ya 37, lakini pia mechi hiyo ilichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa saa 1:00 usiku, hivyo bao la Azam kubaki kuwa ndiyo la kwanza.

Augutine Okra alichomoka na mpira kwa kasi akiwazidi mbio wachezaji kadhaa wa Geita Gold, kabla ya Kelvin Nashon kumsukuma akiwa ndani ya eneo la hatari. Jukumu la upigaji akapewa Chama na kuitendea haki. Simba ilishinda mabao 3-0, na bao hilo la penalti lilikuwa ni la tatu kwenye mchezo huo.

**#3. Ismail Mgunda (Prisons vs Dodoma Jiji)**

Mmoja wa mabeki wa Dodoma Jiji alirudisha kizembe mpira kwa kipa wake, Aron Kalambo bila mawasiliano yoyote.

Kipa huyo alishtukia mpira uko karibu, lakini wakati huo huo, straika wa Prisons Hamisi Mcha alikuwa ameutokea na kuunasa, kabla hajampiga chenga kipa, katika harakati ya kuokoa, Kalambo alimuangusha mchezaji huyo na mwamuzi akaamuru tuta.

Ismail Mgunda akapewa mpira ili apige na akaukwamisha wavuni ikiwa ni dakika ya pili tu ya mchezo ambao ulipigwa Uwanja wa Liti mkoani Singida Agosti 20, mwaka huu, Prisons ikiondoka na ushindi wa mabao 2-1.

Dodoma Jiji inautumia uwanja huo kama wa nyumbani kupisha ukarabati, Uwanja wa Jamhuri. Hii ndiyo penalti ya mapema zaidi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**#4. Dario da Silva (Singida vs Mbeya City)**

Kesho yake, Agosti 21, kwenye Uwanja wa Liti Singida penalti nyingine ilipatikana, lakini mechi ilikuwa ni kati ya wenyeji Singida Big Stars dhidi ya Mbeya City.

Ilikuwa yenye utata kidogo, kwani Mbrazil Dario da Silva alimpiga chenga Samson Madeleke na picha za video zilionyesha kuwa beki huyo hakuupata mpira wala mguu wa mchezaji huyo, lakini alijiangusha baada ya kuukokota mpira kwa hatua kadhaa mwamuzi akaamuru penalti. Yeye mwenyewe aliiweka kambani dakika ya 53, timu yake ikishinda mabao 2-1.

**#5. Matheo Antony (KMC vs Polisi Tanzania)**

Kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, kulikuwa na mechi nyingine ya Ligi Kuu, Agosti 21 kati ya wenyeji Polisi Tanzania dhidi ya KMC iliyoisha kwa sare ya mabao 2-2.

Matheo Antony alifanikiwa kufunga bao la mkwaju wa penalti dakika ya 48, lililotokana na mchezaji mwenzake Daruweshi Saliboko kuangushwa ndani ya eneo la hatari na kipa Kelvin Igendelezi.

**#6. Reliants Lusajo (Namungo vs Coastal)**

Straika wa Namungo alipambana na beki Lameck Lawi kwenye mstari wa eneo la hatari na akaanguka chini, mwamuzi akaamuru penalti. Nayo hii iliyonekana ya utata kidogo, lakini haikumzuia Reliants Lusajo kuukwamisha wavuni likiwa ni bao pekee kwenye mechi hiyo likifungwa dakika ya 40, Namungo ikishinda 1-0 ikiwa nyumbani Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, mechi ikipigwa Septemba 17 mwaka huu.

**#7. Moubarack Azam (Coastal vs Kagera Sugar)**

Mpira mrefu ulipigwa ndani ya kiboksi cha hatari cha Kagera Sugar, ulidunda na kumgonga mkononi beki Abdallah Mfuko, mwamuzi akaamuru mkwaju wa penalti.

Amza kama kawaida yake akachukua jukumu la kupiga mpira huo, akaukwamisha wavuni dakika ya sita tu ya mchezo, mechi ikichezwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga ambako Coastal Union ilikuwa imerejea.

Mechi ilichezwa Oktoba 3, mwaka huu Coastal ikipata ushindi wa mabao 2-0, la pili likifunga tena na Amza mwenyewe, lakini safari hii halikuwa la penalti.


## NDANI YA 18



USHINDI wa mabao 2-1 iliyoupata Manchester United dhidi ya Everton katika Uwanja wa Goodison Park wiki moja iliyopita unaifanya klabu hiyo kuwa timu ya kwanza katika historia ya Ligi Kuu England kushinda mchezo wa 100 baada ya kutanguliwa kufungwa bao 1-0.

## FUNDI WA WIKI...



# GABRIEL FERNANDO DE JESUS

| | |
|---|---|
| KUZALIWA: | Aprili 3, 1997 (umri miaka 25) |
| ALIPOZALIWA: | Sao Paulo, Brazil |
| KIMO: | 1.75 m (5 ft 9 in) |
| NAFASI: | Mshambuliaji |
| KLABU: | Arsenal |
| JEZI NAMBA: | 9 |
| MABAO: | 5 (Kabla ya mechi ya jana) |



ROBERT LEWANDOWSKI

# WAPYA WA5 WALIOFANYA VIZURI LIGI TANO BORA ULAYA

**LONDON, England**

WACHEZAJI kadhaa wapya waliosajiliwa wamefanya vizuri barani Ulaya msimu huu. Msimu unaoendelea wa 2022-23 umekuwa wa kufurahisha kutazama na wachezaji wengi wamezoea haraka katika klabu zao mpya.

Makala haya yanaangazia wachezaji watano wapya waliofanya vizuri zaidi katika ligi tano bora za Ulaya kufikia sasa msimu huu, haya twende...

**#5. Paulo Dybala (AS Roma)**

Raia huyo wa Argentina alijiunga na AS Roma kutoka Juventus kwa uhamisho wa bure msimu uliopita wa majira ya joto na mchango wake katika safu ya ushambuliaji umekuwa muhimu kwa kikosi hicho cha kocha, Jose Mourinho.

Dybala ana mabao sita na asisti mbili katika mechi 10 alizoicheza AS Roma msimu wa 2022-23 hadi sasa.

Pia, Dybala anasalia kuwa mchezaji muhimu wa AS Roma katika safu ya ushambuliaji na itakuwa ya kuvutia kuona kama anaweza kudumisha uthabiti wake msimu huu. Zaidi ya hayo, kutokana na uchezaji wake hadi sasa, huenda akajumuishwa katika kikosi cha Argentina cha Kombe la Dunia nchini Qatar, licha ya kwamba hivi sasa ni majeruhi.

**#4. Gabriel Jesus (Arsenal)**

Mbrazil huyo bila shaka ndiye anayeongoza mashambulizi ya Arsenal na uchezaji wake umekuwa bora katika safu ya ushambuliaji hadi sasa msimu huu. Jesus amefunga mabao matano na kusajili asisti tatu katika mechi nane za Ligi Kuu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, amekuwa nyota muhimu zaidi kwa 'Washikabunduki' hao wa London ambao hivi sasa wapo kileleni mwa msimamo wa ligi (kabla ya mechi za mwishoni mwa wiki).

Jesus anabaki kuwa mchezaji muhimu kwa Arsenal na atakuwa muhimu ikiwa klabu hiyo itaweka changamoto ya ubingwa msimu huu.

**#3. Folarin Balogun (Reims)**

Muingereza huyo alijiunga na Reims kwa mkopo kutoka Arsenal msimu uliopita wa majira ya joto na kiwango chake katika klabu ya Reims kimekuwa bora msimu huu. Balogun amefunga mabao sita na amesajili pasi mbili za mabao kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao mengi zaidi kuliko mchezaji mwingine yeyote aliyezaliwa katika karne ya 21 kwenye ligi tano bora za Ulaya msimu huu.

Balogun atakuwa na matumaini ya kufurahisha kwa klabu yake, na ikiwa ataweza kudumisha kiwango hiki, anaweza kupata fursa ya kucheza katika kikosi cha kwanza cha Arsenal msimu ujao.

**#2. Robert Lewandowski (Barcelona)**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland, amebadilisha mtazamo wa safu ya ushambuliaji ya Barcelona msimu huu. Lewandowski ana mabao tisa na asisti mbili katika mechi nane za Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu. Pia amefunga mabao matatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Barcelona watatumaini mabao ya Lewandowski yatawasaidia kushinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu pamoja na mataji mengine.

**#1. Erling Haaland (Manchester City)**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, bila shaka ndiye mchezaji aliyefanya vizuri zaidi katika ligi tano bora za Ulaya msimu huu na uwapo wake umeboresha kwa kiasi kikubwa safu ya mashambulizi ya Manchester City inayonolewa na Pep Guardiola.

Haaland amefunga mabao 20 ya ajabu katika michezo 13 kwenye mashindano yote kwa Man City hadi sasa.

Raia huyo wa Norway ana wastani wa kufunga bao kila baada ya dakika 48, ambao ndio wastani wa juu zaidi kwa mchezaji katika historia ya Ligi Kuu England.

Guardiola anatumaini kuwa mabao ya Haaland yanaweza kumsaidia kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya huko Manchester.

## JE, WAJUA?

Bukayo Saka ni mchezaji wa pili kinda kwa Arsenal (akiwa na miaka 21 na siku 34) , kuweza kufikisha mabao 20 katika Ligi Kuu England baada ya Nicolas Anelka (wakati huo akiwa na miaka 20 na siku 41).





## Wafurahia taa za barabarani kuongeza mzunguko wa fedha

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAFANYABIASHARA wa Mji wa Ipinda Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wamesema taa za barabarani zilizowekwa na serikali katika mji huo zimeongeza mzunguko wa fedha kutokana na saa za kufanya biashara kuongezeka.

Waliyasema hayo juzi walipozungumza na Nipashe kuhusu faida za uwapo wa taa hizo na kwa sasa wanafanya biashara tofauti na ilivyokuwa mwanzo walipokuwa wanafunga biashara mapema.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Honson Mwakitalima alisema kwa sasa wanachelewa kufunga biashara na wakati mwingine huwa wanafunga saa 6:00 usiku.

Alisema kabla ya taa hizo hazijawekwa walikuwa wanafunga biashara kati ya saa 2:00 na saa 3:00 usiku kutokana na mizunguko ya watu kuisha muda huo tofauti na sasa wanakuwapo muda wote.

"Sasa hivi huwa tunagundua kuwa ni usiku kwa kuangalia saa, lakini usipoangalia unaweza ukajikuta bado upo dukani mpaka usiku wa maanani," alisema Mwakitalima.

Naye Neema Mwakingwe alisema, wajasiriamali wadogo ambao wanapanga bidhaa zao pembezoni mwa barabara walikuwa wanashindwa kuuza bidhaa zao usiku kutokana na giza, lakini kwa sasa wanauza vizuri.

Aliishukuru serikali kwa kuweka taa hizo kwa maelezo pia zimesaidia kuupamba mji huo ambao kwa sasa unang'aa.

# Waelezwa kilimo mapasheni kilivyo na soko kubwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kuchangamkia kilimo cha matunda aina ya pasheni ili kujiongezea kipato kutokana na soko la matunda hayo kuzidi kuongezeka ndani na nje ya nchi.

Aidha, matunda hayo yametajwa kuwa na uwezo wa kuimarisha afya ya uzazi kwa wanaume hasa kuongeza nguvu kutokana na kuwa na madini mengi ya zinki.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Ushauri ya programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT.

Programu hiyo inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini na kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inatekelezwa katika mikoa mitatu ya Mbeya, Songwe na Katavi.

Dk. Anney alitoa ushauri huo kwa wakulima baada ya kamati hiyo kutembelea shamba la mapasheni linalomilikiwa na kikundi cha wakulima cha UAMSHO lililoko katika Kijiji cha Utengule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema zao hilo kwa sasa soko lake limeanza kuongezeka kwa kasi kutokana na kuwa na faida nyingi kiafya na hivyo akawataka wakulima kuchangamkia kulima ili kufaidika na soko hilo.

"Lakini nawashauri wananchi hasa wanaume kutumia matunda haya, yana zinki ya kutosha na hivyo husaidia kukabiliana na tatizo la nguvu za kiume ambazo kwa sasa limekuwa tatizo kubwa sana," alisema Dk. Anney.

Mwenyekiti wa Kikundi cha UAMSHO, Agnes Ndeka, alisema walianza kulima zao hilo miaka mitatu iliyopita, lakini kwa sasa wanaona mafanikio makubwa kutokana na matunda yao kuanza kuzaa na kuwaingizia kipato.

Alisema matunda hayo kwa sasa wanavuna kila wiki na huwa wanauza debe moja kwa kati ya Sh. 8,000 na 10,000 kulingana na msimu fedha ambazo alisema zinawasaidia kwenye mambo mengine ya kijamii pamoja na kuongeza kuupanua mradi.

Alisema matunda yao wanayasafirisha na kuyauza kwenye moja ya hoteli zilizoko katika Jiji la Dodoma na kwamba mnunuzi huyo huwa anasafirisha mwenyewe kwa gharama zake.

"Ili matunda yetu yasiharibike kabla ya kusafirishwa tumetengenezewa kifaa cha kuhifadhia na programu ya kilimo bora kwa wanawake na vijana (KIBOWAVI) inayotekelezwa na Shirika la HELVETAS kwa hiyo huwa tunayauza yakiwa katika hali nzuri," alisema Agnes.

Alisema mbali na soko la matunda hayo kuwa kubwa jijini Dodoma lakini wamepata soko jipya Dubai na hivyo wanakusudia kupanua zaidi mashamba yao ili kulifikia soko hilo.

Mkurugenzi wa Programu ya KIBOWAVI, Daniel Kalimbya, alisema baada ya kuona juhudi za kikundi hicho waliamua kukisaidia kuboresha baadhi ya miundombinu hasa ya umwagiliaji, uhifadhi na kuwasaidia kuwaunganisha na masoko ya uhakika.

Alisema pia waliaamua kuwasaidia mbinu za kisasa za kilimo cha zao hilo ili kuhakikisha wanazalisha kwa tija zaidi tofauti na ilivyokuwa mwanzo wakati wanaanza.



Moja wa wakulima wa vitunguu katika Skimu ya Igomelo wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, wanaowezeshwa na Shirika la HELVETAS, akipakia vitunguu kwenye mfuko kwa ajili ya kwenda kuvihifadhi kwenye ghala la Chama cha Ushirika walilojengewa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakazi wa vijiji saba walilia maji ya bomba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa vijiji saba vya Kata ya Ilembo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanalazimika kutumia maji ya kwenye vijito na makorongo kutokana na kukosekana kwa bomba maeneo hayo.

Wananchi hao waliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama katika kata hiyo kwa lengo la kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na serikali kwa kushirikiana na wadau.

Diwani wa Kata ya Ilembo, Abel Mpyambala, alisema kata hiyo ina vijiji saba, lakini ni kimoja pekee cha Ilembo chenye maji ya bomba.

Alisema vijiji vingine wananchi wanakunywa maji yanayotoka kwenye makorongo na baadhi ya vijito hali inayohatarisha afya za wananchi hao.

Alisema katika baadhi ya vijiji makorongo ya maji yako mbali na makazi ya watu ambayo inawalazimu kutumia muda mwingi kufuata huduma hiyo badala ya kufanya shughuli za maendeleo.

"Tunaomba tusaidiwe kufuata maji ya bomba maana tunapata shida kwa muda mrefu sana, walikuja watu wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), wakakiangalia chanzo kilichoko jirani na wakaahidi kutuletea maji, lakini mpaka sasa wako kimya," alisema Mpyambala.

Alisema katika kijiji cha Mwala kunakojengwa Shule ya Sekondari ya wasichana, pia hakuna maji hali aliyosema italeta tatizo kwa wanafunzi shule zitakapofunguliwa.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Mwala, waliiomba serikali kuharakisha mradi wa maji ambao waliahidiwa kwa maelezo kuwa wamekuwa wakipata wakati mgumu kutafuta hasa kipindi cha kiangazi.

Mmoja wa wananchi hao, Sauda Daniel, alisema wanawake wa kijiji hicho ndio wanaoteseka zaidi kutafuta huduma hiyo na kwenye baadhi ya makorongo kuna miteremko mikali ambayo huwa inahatarisha maisha yao.

Alisema kipindi cha kiangazi huwa wanachangia maji hayo na mifugo kwa kuwa makorongo hayo ni ya wazi na hakuna ulinzi wa kuzuia mifugo kwenda kunywa.

"Huwa tunalazimika kuwahi sana alfajiri ili tuchote kabla hayajachafuliwa na mifugo, lakini wakati mwingine matumbo huwa yanatuuma na tunahisi haya maji pia yanaweza yakawa yanachangia," alisema Sauda.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema atatoa maagizo kwa Meneja wa RUWASA ili kushughulikia tatizo la maji katika kata hiyo kwa kutafuta chanzo cha uahakika cha maji.

Alisema serikali ilianzisha chombo hicho kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini na kusisitiza atafuatilia na kuhakikisha chombo hicho kinashughulikia matatizo ya wananchi.

Alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Mbeya na viongozi wengine wa wilaya hiyo kusimamia miradi yote kwa umakini ili ikamilike mapema na kuwanufaisha wananchi.



## HABARI DODOMA

# Askofu aonya wagonjwa wa afya akili kupelekwa kwa wapigaramli

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

ASKOFU wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania PHAM (T) Kanda ya Kati, Brayson Msanjila, amezitaka familia zenye wagonjwa wa afya ya akili, ziache kuwapeleka kwa waganga wa kienyeji na wapigaramli.

Alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wakazi wa Kijiji cha Chalinze Nyama wilayani Chamwino wakati wa ibada iliyoandaliwa kwa ajili ya kumpongeza Mchungaji Saimon Sandiya aliyetimiza miaka 40 ya utumishi wake.

Askofu Msanjila alisema wagonjwa wa aina hiyo wanapaswa kupelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ya akili ili waanze matibabu mapema badala ya kuwachelewesha kwa waganga hao.

"Niziombe familia pindi kunapotokea kuwapo mgonjwa wa afya ya akili, ni vizuri akapelekwa hospitalini badala ya huko kwa waganga na kwa wapigaramli.

"Tatizo la afya ya akili likipatiwa matibabu haraka kwa asilimia kubwa linatibika haraka tofauti kama mgonjwa huyo akipelekwa kwa waganga wa kienyeji," alionya.

Alisema serikali kupitia hospitali zake, ina wataalamu wa kutosha kwa ajili ya magonjwa ya afya ya akili, hivyo hakuna sababu ya kuwapeleka kwa waganga wa kienyeji watu wanaogundulika kuwa na tatizo hilo.

Pia aliwashauri wakulima kuhakikisha wanaandaa mashamba yao mapema ikiwamo kuweka mbolea kwa ajili ya maandalizi ya kupanda mbegu kwa wakati.

Mchungaji Sandiya aliwataka wazazi na walezi ambao wana wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi, kuwaendeleza kielimu zaidi badala ya kuwaweka majumbani.

Alisema wanafunzi hao wanatakiwa kuwaendeleza kielimu ikiwamo kwenye vyuo vya ufundi na kwa kufanya hivyo watakuwa wamewekeza kwao kitaaluma.

Alisema watoto hao wakiachwa bila kuendelezwa, taifa litakuwa na tabaka la vijana wanaojiingiza kwenye makundi maovu kama vile 'panya road' na mengineyo.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akitembelea banda la Bank of Africa katika tamasha la Vicoba Night Out lililoandaliwa na benki hiyo ikishirikiana na Altenative FM Radio. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Adam Mihayo, anayetoa maelezo ni Mwenyekiti wa FM Radio, Emmanuel Rutagonya. Tamasha hilo lilifanyika mjini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mjumbe wa NEC ataka vijana wafundishwe kuhusu Nyerere

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Taifa, Heppey Mgongo, amewataka viongozi nchini kuwafundisha vijana kumfahamu kwa kina Hayati Mwalimu Julius Nyerere ili kuyaishi maisha yake yatakayowafanya wawe viongozi bora wa baadaye.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wanafunzi walio wanachama wa Taasisi ya Harakati za Vijana Duniani (GYL) kutoka shule za sekondari za Wilaya ya Chamwino ikiwa ni sehemu ya kumbukizi ya kifo cha Mwalimu Nyerere.

Alisema viongozi hao wana wajibu wa kuwafundisha vijana umuhimu wa Mwalimu Nyerere ili kuenzi mambo ya kizalendo aliyoyaacha kwa Taifa la Tanzania. Mjumbe huyo aliwahimisha vijana wanaohitimu elimu ya sekondari, kujiwekea malengo kuhusu maisha yao kwa kile walichojifunza kwa muda wote waliokaa darasani.

Mgongo ambaye ni Ofisa Taaluma Wilaya ya Chamwino, aliwataka wanafunzi kuitumia elimu yao hiyo wanapomaliza, kubadilika kimaisha na kiuchumi ili ndoto hizo zisigeuke kuwa kilio cha ukosefu wa ajira mtaani.

"Maendeleo yoyote hayana mganga wa kienyeji, bali ni juhudi na bidii zenu ndizo zitakazowabadilisha kiuchumi na kuweza kufikia malengo yenu kupitia elimu mliyoipata kwa muda wote mkiwa shuleni," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya GYL, Kelvin Sanula, alisema lengo la taasisi hiyo ni kuhakikisha vijana wanapewa mafunzo endelevu pindi wanapohitimu.

Alisema kuonyesha na kukuza vipaji vya vijana walio shuleni ili viendelezwe badala ya kuishia kwenye majukwaa bila kuendelezwa.

## Bodi ya Taifa ya Maji yakagua ujenzi bwawa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

BODI ya Taifa ya Maji imekagua mradi wa ujenzi wa bwawa la maji la Mtamba wilayani Mpwapwa na Bwawa la Manda wilayani Chamwino mkoani Dodoma ambayo yatatumika kwa shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwamo kilimo cha umwagiliaji.

Mabwawa hayo yanajengwa na Bodi ya Maji ya Bonde la Rufiji na yanatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 1.3.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Mbogo Futakamba, alisema mabadiliko ya tabianchi yameathiri sehemu mbalimbali nchini, hivyo uamuzi wa kujenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua utasaidia wananchi kuwa na uhakika wa usalama wa chakula, mazingira, nishati na afya.

Alitaka ujenzi wa mabwawa hayo ukamilike kwa wakati ili wananchi waanze kunufaika nao.

Pia aliwahimisha kuweka alama za mipaka ili kuzuia shughuli za kibinadamu ambazo zitaathiri uendelevu wa mabwawa hayo.

Akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa mabwawa hayo, Mhandisi Geofrey Semkonda wa Bodi ya Maji Bonde la Rufiji, alisema mabwawa yote mawili yanatarajia kukamilika mwishoni mwa Oktoba mwaka huu.

"Haya mabwawa yatatatua kero ya huduma ya maji kwa wananchi na mifugo inayozunguka maeneo haya," alisema.

Pia alisema ujenzi wake umezingatia mahitaji ya wananchi kwa sasa na baadaye katika maeneo yanayozunguka mabwawa hayo.

Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulika na Uhifadhi na Utunzaji Vyanzo vya Maji wa Wizara ya Maji, Rosemary Rwebugisa, alisema mabwawa yanayojengwa ni sehemu ya mkakati wa wizara kuhakikisha rasilimali mvua inatumika kama chanzo cha maji ili kuhudumia maeneo ambayo hayana vyanzo.

Pia alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.



## ZECO yaahidi kufikisha umeme Kiboje kuondoa adha matumizi jenereta

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shabaan Ali Othman, amewaahidi wakaazi wa eneo la Kinooni, Shehia ya Kiboje, Unguja kuwa ndani ya wiki moja Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), litafikisha umeme katika eneo hilo ili waondokane na gharama za kupandisha maji kwa kutumia umeme wa jenereta.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara katika Jimbo la Uzini, Unguja kufuatia malalamiko ya mwakilishi wa jimbo hilo kwamba wakaazi wa eneo hilo hawana huduma ya umeme wala majisafi na salama.

Alisema atahakikisha ndani ya mwezi huu Oktoba, umeme utafikishwa katika maeneo hayo ili wakaazi wa eneo hilo waandokane na gharama za kutia mafuta kwenye jenereta kwa ajili ya kupandisha maji kutoka kwenye kisima hadi tangi la kuhifadhia maji.

Alisema wizara yake kupitia ZECO inatoa nguzo za umeme bure ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais wa Zanzibar na atahakikisha Shirika hilo linafikisha umeme haraka eneo hilo.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri alitembea maeneo mengine ya jimbo hilo la Uzini ikiwamo Kwambani na Kidimni na wakaazi wengi wanakabiliwa na changamoto ya majisafi ya salama.

Alisema wizara yake inatekeleza miradi ya maji kwa ajili ya kuwaondolea changamoto ya maji wananchi na miradi hiyo karibu itakamilika.

Mkaazi wa Shehia ya Kinooni Mastura Mgeni Hamadi, alisema wanawake wa eneo hilo wanachangishana Sh. 3,000 kwa ajili ya kutia mafuta ya dizeli kwenye jenereta ili wapandishe maji kwenye tangi kutoka katika kisima.

"Naiomba serikali iwafikirie wanawake hii shida ya maji kwa sababu wanateseka sana, hali duni ya maisha wakati mwingine mtu anakua anakosa fedha hiyo ya mchango," alisema Mastura.

# Zanzibar yavunja rekodi ukusanyaji mapato bahari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR imevunja rekodi ya kiwango cha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na uhifadhi wa bahari kutoka Sh. 241,308,001 kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia Sh. 552,582,159 kwa mwaka huu wa 2022.

Hayo yalisemwa jana mjini hapo na Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, katika hafla ya mgao wa fedha za mapato ya utalii yatokanayo na uhifadhi wa bahari na ni kwa wanajamii.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. 125,751,600 ambazo ni asilimia 30 ya mapato yaliyopatiwa wizara kutoka Hazina zitatolewa kwa wananchi.

Aliwataka wadau wote kuungana kuhifadhi mazingira ya bahari kwa kupiga vita uvuvi haramu, utupaji wa taka baharini na ufukweni.

Alisema lazima kujitahidi kulinda na kuyakuza mazalio ya samaki na uhifadhi wa mikoko, matumbawe na nyasi za bahari na ili kuongeza mapato, wadau wote kuunga mkono dhana ya utalii endelevu na unaojali mazingira kwa wote.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Aboud Suleiman Jumbe, alisema hifadhi za bahari ni muhimu katika uhai na ustawi wa jamii kote ulimwenguni kwa sababu ni mazalia ya samaki, hujenga misingi ya uvuvi endelevu na kitovu cha uhifadhi wa bayoanuai.

Alisema hifadhi ya bahari ni kinga dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, udhibiti wa hewa ukaa na vituo vya utafiti wa sayansi na teknolojia inavyosaidia katika utafutaji wa mali ghafi mbalimbali ikiwamo dawa na vitega uchumi kwa ajili ya usalama wa chakula na maendeleo endelevu.

"Hifadhi ya bahari ni kiini cha ajenda nzima cha usimamizi wa bahari na safari yetu ya uchumi wa buluu ni takwa la mkataba wa kimataifa wa bayoanuai, shabaha ya 11 ya mkutano wa kimataifa wa nchi, lengo la 14 la malengo ya maendeleo endelevu ya usimamizi wa bahari na uchumi wa buluu pamoja na mkakati wa usimamizi wa bayoanuai wa mwaka 2020," alisema.

Alisema kwa wastani duniani kuna maeneo tengefu ya hifadhi ya bahari yapato 18,000 ni sawa na asilimia 8.16 ya bahari ambayo ipo chini ya aina moja au nyingine ya uhifadhi wa bahari au ni eneo la kilomita ya mraba milioni 30 katika ukanda wa bahari ya magharibi ya Bahari ya Hindi kuna maeneo tengefu 143 yenye eneo la kilomita ya miraba laki tano au sawa na asilimia saba ya eneo zima la bahari hiyo.

Alisema ipo haja ya kuongeza bidii kwa jumuiya ya kimataifa ya kufikia lengo la 30 kwa 30 ulimwenguni ifikapo mwaka 2030.

Alisema kwa Zanzibar kunahifadhi za bahari tano ikiwamo Hifadhi ya Ghuba ya Minai, Hifadhi ya Mnemba, Hifadhi ya Kisiwa cha Changuu na Bawe, Hifadhi ya Kisiwa cha Tumbatu na Hifadhi ya Mkondo wa Bahari wa Pemba sawa na kilomita za miraba 2281 au asilimia 7.36 ya eneo lote la bahari ya ndani katika visiwa vya Zanzibar.

Alisema hifadhi za bahari katika visiwa vya Zanzibar ni msingi wa ajenda endelevu ya uchumi wa buluu, mipango yote ya uvuvi mdogo, kilimo cha mwani, ufuaji wa viumbe hai vya bahari, ufugaji wa pweza na chaza, uhifadhi wa mikoko, nyasi za bahari, matumbawe na mafungu ya mchanga.

Alisema utalii wa Zanzibar hauwezi kunawiri bila ya kuwekeza katika ulinzi na usalama wa bahari pamoja na ikolojia yake.

Mkurugenzi wa Idara ya Uhifadhi wa Bahari, Dk. Makame Omar Makame, alisema bila ya kuwa na bahari yenye mandhari nzuri hakuna utalii wala uvuvi na uhifadhi una umuhimu mkubwa hasa katika kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta ya uvuvi. Aidha, alisema wastani wa wageni 100,000 walitembelea maeneo manne ya hifadhi ya Unguja kwa mwaka 2021/2022 na kiwango cha fedha kilichokusanywa kwa mwaka huu ni 552,582,159.

Alisema bado wanakabiliwa na changamoto za ukwepaji wa kulipa na ukusanyaji wa mapato lakini ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mtandao (Zan Malipo) kwa kiasi kikubwa imepunguza changamoto kwenye ukusanyaji wao ambao kwa mwezi Julai hadi Septemba mwaka huu walikusanya Sh. 450,000,000.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema uhifadhi ndiyo roho ya uchumi wa buluu na kuwaomba wananchi, kuenzi na kuitunza bahari ili dhana ya uchumi huo kufikiwa na kuahidi kutoa ushirikiano katika jambo hilo.

Katika mgao huo wa fedha unategemea na kiasi kilichokusanywa katika hifadhi ya eneo la MENAI ina gawio la Sh. 46,603,760, hifadhi ya MIMCA imepatiwa Sh. 45,058,040, hifadhi ya CHABAMCA ni Sh. 32,822,925 na hifadhi ya eneo la Tumbatu TUMCA imepata Sh. 1,266,873.




Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame (kushoto), akiwa na watendaji wa wizara yake wakimkabidhi hundi mwanauhifadhi wa bahari kutoka ghuba ya Chabamka, Abdallah Said (kulia), katika hafla ya mgawo wa fedha za mapato ya utalii yatokanayo na uhifadhi wa bahari. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## SMZ kuendelea kushirikiana na 'UN Women'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kushirikiana na Shirika la Wanawake Duniani katika kuhakikisha wanatimiza malengo yao waliyojiwekea.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo wakati wa mazungumzo yake na Katibu Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wanawake (UN Women), Sima Sami, ofisini kwake juzi Vuga Zanzibar.

Alisema Umoja wa Mataifa (UN) unaendesha miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali na serikali itaendelea kusimamia miradi hiyo ili kukamilika.

Hemed alisema serikali inatambua umuhimu wa wanawake katika maendeleo na Rais Mwinyi amewaamini wanawake na kuwapa nyadhifa mbalimbali katika uongozi.

Hemed alimwomba Katibu Mtendaji huyo kuandaa utaratibu wa kuwaongezea uzoefu wanawake wa Zanzibar ili kuendana na kasi ya dunia kimaendeleo.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia wanawake, Sima Sami amefurahishwa kuona serikali inathamini mchango wa wanawake kwa kuzingatia uwezo wao.

Alisema shirika hilo lina mikakati mingi kwa kuwainua wanawake na kuiomba Serikali ya Zanzibar kutoa ushirikiano wa kutosha kufikia malengo yao.





# Bomu lajeruhi watoto wakilipasua kwa panga

**Na Halima Ikunji** TABORA

WAKAZI wawili wa Kata ya Kabila, Manispaa ya Tabora wamenusurika kifo baada ya kujeruhiwa kwa kulipukiwa na bomu walilolikata kwa kutumia panga wakitaka kufahamu ni kitu gani.

Tukio hilo lilitokea Oktoba 12 katika kata hiyo ambako vijana hao walikuwa wakichunga ng'ombe ndani ya Hifadhi ya Taifa Igombe na kuokota kitu ambacho walitaka kukifahamu.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao aliwataja waliojeruhiwa kuwa ni Kikombe Kishagembe (17) na Said Cosmas (10), wote wakazi wa Kitongoji cha Igosha.

Alisema vijana hao walichukua kitu hicho hadi nyumbani bila kutambua ni kitu gani na kisha kutaka kufahamu kwa kina kilichoko ndani yake ndipo wakachukua uamuzi wa kukikata kwa panga na mlipuko kutokea na kuwajeruhi.

Kamanda Abwao alisema kuwa uchunguzi wa awali umebainisha bomu hilo ni aina ya Stick Hand Grunet na wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Alisema mpaka sasa majeruhi wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora (Kitete) na wanaendelea vizuri.



Vijana wakiwa wamembeba mmoja wa wazee mkazi wa Manispaa ya Shinyanga, ambaye alifika juzi kwa ajili ya kupatiwa huduma ya matibabu ya macho bure, katika Chuo cha Ualimu Shinyanga (SHYCOM), ambayo inatolewa na madaktari bingwa kutoka hospitali mbalimbali hapa nchini, ikiwamo KCMC, Muhimbili, Aghakhan, Hindu na Mandali, matibabu yaliyoratibiwa na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Lucy Mayenga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BAKWATA yashtukia talaka, wanandoa kuuana

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BARAZA la Waislamu Tanzania (BAKWATA) mkoani Mwanza limewataka wazazi na walezi kuwapeleka kwao vijana wa kike na kiume wanaotarajia kufunga ndoa ili wapatiwe mafunzo maalum kwa siku 21 kabla ya kuingia huko ili kuwaepusha na migogoro inayosababisha wanandoa kuuana.

Vilevile, baraza hilo limesema mafunzo hayo yanalenga kuwafundisha vijana wa kiume na kike namna ya kuishi kwa amani, upendo, heshima ya mke na mume ili kuepusha ndoa kuvunjika muda mfupi baada ya kufungwa.

Kiongozi wa BAKWATA mkoani Mwanza, Sheikh Hassan Kabeke, alibainisha hayo jijini hapo mwishoni mwa wiki wakati akifungisha ndoa kwa vijana wanne wa kike na kiume waliohitimu mafunzo hayo ya siku 21. Sheikh Kabeke alisema hivi karibuni kumekuwa na migogoro mingi katika ndoa na mingine kusababisha wanandoa kuuana, akisisitiza kiini chake ni watu kutopata mafunzo ya ndoa kutoka kwa viongozi wao wa dini.

Aliwataka vijana wa Kiislamu kuepuka kuingia katika ndoa kwa kufuata mali, badala yake waingie wakiamini wanafanya hivyo kama sehemu ya ibada.

"Ndugu zangu Waislamu, ndoa ni ibada na sio kitu kingine na hii lazima tuwaambie vijana wetu wajue kupitia mafunzo maalum na mtu asiingie huko akidhani anakwenda kutafuta mali kwa mwenzake," alisema.

Alisisitiza vijana wakiandaliwa vyema na viongozi wa dini, kuna uwezekano wa kuishi katika ndoa maisha yao yote bila migogoro kwa sababu kila mmoja atakuwa anajua wajibu wake kwa mwenzake.

"Leteni BAKWATA vijana wenu wa kike na kiume wapate mafunzo maalum kutoka kwa viongozi wa dini, watafundishwa mambo mengi kuhusu ndoa na elimu ya Qur'an ambayo ndiyo msingi wa kuishi kwa amani," alisema Sheikh Kabeke.

Alisema Mkoa wa Mwanza umekuwa wa kwanza kuanzisha utaratibu huo na wataendelea kufanya hivyo kwa vijana wa Kiislamu ili kuwaweka katika mstari ulionyooka.

Sheikh Kabeke pia aliongoza harambee ya kuchangia ujenzi wa vituo vya afya 21 mkoani Mwanza na kufanikiwa kukusanya Sh. 400,000.

Alisema Waislamu wanajitoa katika kujenga misikiti mikubwa ya gharama kubwa, lakini wamesahau suala la afya kwa waumini wao na wale wasiokuwa waumini wa dini hiyo.

Mfanyabiashara maarufu jijini Mwanza, Baraka Chilu, katika harambee hiyo aliahidi kuchangia mbao na fedha ili kufanikisha ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

Aliwataka wazazi na walezi wengine wa Kiislamu kuangalia namna bora ya kuwasaidia vijana wao katika maisha ikiwamo kuwapatia elimu ya dunia pamoja na Qur'an.

## 3,000 wapewa elimu ya ufuatiliaji mali za umma

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI 3,000 kutoka kata sita za Mkoa wa Shinyanga wamepewa elimu ya ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma zilizotolewa kwa ajili ya uboreshaji huduma za kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kuhakikisha viwanda vinapata malighafi ya kutosha.

Elimu hiyo imetolewa kwa wakazi hao kutoka Kata za Tinde, Didia, Nyandekwa, Igunda, Kinamapula na Bukomela chini ya Chama cha Watu Wasioona mkoani Shinyanga kwa ufadhili wa Shirika lisilo la kiserikali la Foundation for Civil Society (FCS).

Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Shinyanga, Marco Nkanjiwa aliyabainisha hayo jana wakati wa uendeshaji wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika Kata ya Igunda Halmashauri ya Ushetu.

Alisema wamepokea mradi huo wa Sh. milioni 43.9 na ulianza kutekelezwa Septemba Mosi mwaka huu, ukitarajiwa kukamilika Aprili 30, mwakani.

Alisema lengo la kutoa elimu ya ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma zilizotolewa kwa ajili ya uboreshaji wa kilimo katika jamii, ni kuongeza uelewa kwa wananchi na kuhakikisha msimu ujao wa mavuno wa mazao ya chakula na biashara unakuza uchumi kwa kila mkulima.

Nkanjiwa alisema serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 954 kwa ajili ya sekta ya kilimo nchi nzima, zikiwamo za ruzuku kwa ajili ya pembejeo za kilimo, lakini baadhi ya wananchi hawatambui namna sahihi ya kuzifuatilia fedha hizo na kuhakikisha zinawanufaisha kwa kupata pembejeo za kilimo kulingana na bei iliyotolewa na serikali.

Alisema jukumu lililobaki ni kwa maofisa ugani walioko kila kata kuwatembelea wakulima wao na kuwashauri namna bora ya kulima kulingana na mazingira yao ya kilimo ili kupata mazao mengi.

Mwezeshaji wa Mafunzo hayo, Diksoni Maganga alisema wananchi walikuwa hawana uelewa kuhusu ufuatiliaji wa rasilimali za umma, hata ruzuku za pembejeo zilizotolewa kupitia kwa maofisa ugani walioko kila kata wanazotoka.

Alisema kila mmoja baada ya mafunzo hayo anatakiwa kuwa mfano wa kuigwa katika eneo analotoka kwa kushirikiana na ofisa ugani na kuanzisha mashamba darasa ambayo yatakuwa yakitoa elimu ya kulima kisasa kwa vijana ambao watakuwa wamehitimu elimu ya msingi au sekondari.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Matha Andrew kutoka Kinamapula, alisema alikuwa hafahamu kama wana uwezo wa kufuatilia miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao na hivyo elimu aliyoipata itamsaidia kuwa anahoji kila kitachokuwa kinafanya kwa lengo kuhakikisha kinafanyika kwa ubora unaohitajika.

Charles Kafuku, mkazi wa Igunda alisema atahakikisha anashirikiana na kamati ya maendeleo ya kata anayotoka ili kufuatilia masuala mbalimbali yanayohusu kilimo ili msimu ujao apate mavuno mengi na kuondokana na njaa kwenye familia na taifa kwa ujumla.

## FAO: Magonjwa yanayotokana na chakula husababisha vifo 420,000

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) limesema magonjwa yanayotokana na chakula husababisha vifo vya watu 420,000 kila mwaka duniani, huku vifo 125,000 vikiwa ni vya watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Kwa mujibu wa Mwakilishi wa FAO nchini, Nyabenyi Tipo, mtu mmoja kati ya 10 huugua baada ya kula chakula hicho kichafu.

Anasema utafiti unaonyesha wanaoathirika zaidi kwa tatizo hilo ni kutoka Bara la Afrika na kusini mwa Asia.

"Tishio la usalama wa chakula huathiri watu wa rika zote hususani watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, na watu wanaoishi katika maeneo yenye kipato cha chini duniani, vyakula visivyo salama ni tatizo kubwa na ni tishio kwa afya duniani.

"Ni muhimu kuhakikisha chakula ni salama katika kila hatua kuanzia uzalishaji, kuvuna, usindikaji, uhifadhi, usambazaji, utayarishaji na matumizi yake.

"Na kupitia kampeni ya Lishe Bora ni Mtaji inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), tunalenga kukuza lishe bora ikiwamo kurekebisha kanuni za lishe bora kwa afya na ustawi wetu," anasema.

Anatoa wito kwa wadau wote wakiwamo maofisa ugani kuhakikisha chakula kinachozalishwa kinazingatia kanuni zote za usalama na kuepuka ulaji wa chakula kisichofaa.

Pia alisema katika kupambana na tatizo la sumukuvu kwenye chakula, FAO kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania kupitia programu inayofadhiliwa na EU ya Agri-Connect, imezindua kampeni ya kitaifa inayolenga kuimarisha lishe bora nchini.

"Kampeni hiyo inajulikana kama lishe bora ni mtaji na inalenga kuwajengea Watanzania tabia ya kula mlo bora kwa kutumia vyakula vinavyopatikana nchini.

"Na katika kampeni hii suala ya sumukuvu linalengwa kwa sababu katika vyakula vinavyopatikana nchini hilo ni miongoni mwa yanayochangia katika kuhatarisha usalama wa chakula," anasema.

# Shekhe Ponda aibukia Sheria ya Ndoa

**Na Oscar Assenga, TANGA**

WAKATI Wizara ya Katiba na Sheria ikiwaita wadau kutoa maoni ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na wanaharakati wa haki za wanawake na watoto wakitaka marekebisho ya sheria hiyo, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Tanzania, Shekhe Issa Ponda ameishauri serikali kuachana na suala hilo.

Ponda alisema kurekebishwa kwa umri wa mtu kuolewa kutatengeneza fursa ya uhalifu na uovu na kwamba hakuna mantiki ya kuzuia mtu kuolewa kwasababu ni mtoto, liachwe kuwa jambo la maumbile na sio kujadiliwa bungeni.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa uzinduzi wa kongamano la Muslim Swadakatul Jaariya Fund uliofanywa na Taasisi ya Islamic Development Foundation ya jijini Tanga, kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa hospitali ya Kiislam.

Aprili mwaka 2018, aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi, alilieleza Bunge kuwa, kufumua Sheria ya Ndoa kutasababisha mtikisiko na kushauri iachwe ilivyo kwa kuwa inamlinda mwanamke kwenye vifungu vingi.

Mwaka 2016 mwanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto wa Shirika lisilo la kiserikali la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, alifungua kesi Mahakama Kuu ya Tanzania kupinga umri wa mtoto kuolewa.

Aidha, Mahakama iliagiza serikali kufanya mabadiliko ya baadhi ya vifungu vya sheria hiyo ambavyo vinapingana na Katiba ya nchi kwa kuweka umri tofauti wa mtoto.

Katika Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1977, binti wa miaka 15 anaruhusiwa kuolewa kwa ridhaa ya wazazi/walezi huku aliye chini ya umri huo anaweza kuolewa kwa ridhaa ya Mahakama na Katiba ikimtambua mtoto ni mtu mwenye umri wa miaka 18 na anapofikisha umri huo anaruhusiwa kupiga kura.

Shekhe Ponda alisema suala la umri wa mtoto wa kike kuolewa linategemea balehe na maumbile yake badala ya kujadiliwa bungeni kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria za dini ya Kiislamu inavyoolezwa kwenye vitabu vyake.

Aidha, alisema kumekuwapo na mjadala wa umri sahihi wa mtoto wa kike anaopaswa kuolewa kwa uchunguzi walioufanya wamegundua hitaji la mabadiliko hayo halitoki kwa jamii bali ni kwa makundi ya haki za binadamu.

"Kwanza tunataka sheria ibaki vilevile na hakuna sababu ya kuongeza umri wa mtoto wa kike kuolewa kwa sababu unapozidisha umri unasababisha ongezeko la zinaa," alisema Shekhe Ponda.

Alisema serikali kuingilia suala hilo ni kuingilia imani za watu na kanuni za maumbile na kushauri ingejiweka mbali na kuacha kusikiliza homa ya makundi yanayotetea haki za binadamu.

Alisema suala la mabadiliko ya mtoto anayepaswa kuolewa sio jambo la viongozi wa serikali kujadili miaka mingapi na vigezo gani vinataonyesha umri sahihi wa kuolewa kwa mabinti na kwamba lipo kiimani zaidi.

Awali, Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Shekhe Juma Mohammed, alisema ujenzi wa hospitali hiyo utakaozingatia utu wa mwanamke ni jambo la kijamii na halitakuwa na ubaguzi wa kiimani.

Shekhe Juma alisema kuna umuhimu wa serikali kuunga mkono jitihada zinazomuhifadhi mwanamke hasa kwa kutibiwa na mwanamke mwenzake jambo litakalomfanya kuwa huru.

"Labda niweke sawa lengo la hospitali hii sio kubagua wasio kuwa waislam bali tutashirikiana na hata wasiokuwa waislam na lengo letu ni moja tu la kumuhifadhi mwanamke na utu wake pindi anapohitaji kufanyiwa matubabu," alisema.

Alisema ujenzi wa hospitali hiyo utagharimu Sh. bilioni 1.5 na kuiomba jamii bila kujali itikadi za dini kuchangia ujenzi huo.



Msimamizi wa mradi wa barabara ya zege ya kilomita 0.4 wa Serc Contractor, Mhandisi Emanuel Kisoka, akitoa maelezo kwa wanachama wa Chama Cha Mapinduzi na wananchi wanaoishi Mtaa wa Golani Kimara Manispaa ya Ubungo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Dastan Mlingwa na Mwenezi wa Tawi la Nzasa, Sadiki Msangi, wapotumia Siku ya Nyerere kutembelea miradi inayotekelezwa kwenye mtaa wao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu 14 mbaroni tuhuma udanganyifu mtihani la VII

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia walimu 14 kwa tuhuma za kukiuka sheria, kanuni na taratibu za mtihani wa darasa la saba uliofanyika Oktoba 5 na 6 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema uchunguzi unaendelea na utakapokamilika, taarifa zitatolewa na mamlaka zinazohusika na masuala ya elimu.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muliro alibainisha kuwa jeshi hilo linawashikilia watuhumiwa sita ambao majina yao yamehifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi, kwa tuhuma za wizi wa vifaa mbalimbali vya miundombinu ya Shirika la Umeme (TANESCO) vinavyotumika katika ujenzi wa umeme wa msongo wa kati.

"Watuhumiwa hao walikamatwa Oktoba 6 mwaka huu majira ya saa za mchana maeneo ya Mwenge wilayani Kinondoni, wakiwa na vifaa mbalimbali vya miundombinu ya TANESCO kwenye gari aina ya Noah.

"Upelelezi wa Jeshi la Polisi umebaini kwamba vifaa hivyo ambavyo ni mali ya Kampuni ya State Grid Electrical and Technical LTD na Tropical Industrial LTD, viliibwa mkoani Morogoro na Lindi na watuhumiwa hao walikuja Dar es Salaam kutafuta soko," alisema Muliro.

Alitoa onyo kuwa jeshi hilo halitavumilia mtu au kikundi chochote kinachojihusisha kwa namna yoyote ile kukwamisha maendeleo katika miradi yenye maslahi mapana kwa taifa na ambayo imejengwa kwa manufaa ya umma, akisisitiza ufuatiliaji na uchunguzi wa kina unaendelea.

Kamanda Muliro pia alisema wamewakamata Mohamed Amani (45), mkazi wa Dar es Salaam, Salome Richard (32), mkazi wa Mwanza na wenzao wanane kwa tuhuma za wizi wa magari katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam.

Alisema kuwa katika operesheni hiyo, jeshi hilo liliyakamata magari 23 ya aina mbalimbali, ambayo ni IST (matano), fuso, Nissan Civilian, Coaster, Toyota Hilux Pickup, Nissan Patro, Toyota Premio (mawili), Probox, Spacio (mawili), Harrier (mawili), Rav4 (matatu), Town Hiace (mawili) na Hiace.

Alibainisha kuwa magari hayo yalikamatwa katika mikoa ya Mwanza, Iringa, Kilimanjaro, Kagera na Dar es Salaam na baada ya kuwahoji kwa kina, waliwapeleka wapelelezi yaliko magari hayo.

"Upelelezi wa Jeshi la Polisi umebaini kuwa watuhumiwa hawa kabla ya kuiba, huvizia magari hayo yakiwa yameegeshwa kwenye maegesho ya jumla, binafsi na majumbani baadaye huvunja vitasa vya milango ya upande wa dereva na kuwasha gari kwa kutumia funguo bandia na kuondoka.

"Pia baada ya kuiba magari hayo hubandika namba za usajili na chasses za magari yaliyopata ajali na kuuzwa kama vyuma chakavu na kampuni za bima na baadaye kuyauza tena.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA IRINGA**

**KITUO CHA KALENGA MKOA WA IRINGA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 12/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAJI KASIM KALINGA WA IRINGA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA YAHYA YASINI ABDALLAH**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MAHAKAMA YA MWANZO KALENGA IRINGA

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 903 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late RITHA ANDREW MDUMA**

**and**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by JOYCE CHIBOMBO MWAMBENE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 2 day of November, 2022.

Dated at DAR ES SALAAM this **5 day of October, 2022.**

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIE ROSE DUSABEYEZU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 835 AWG - TOYOTA RAUM.** Chassis namba **EXZ100084550.** Engine namba **SE1353434.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/404409/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BRUNO LAURENT KAPINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 126 DHZ – TOYOTA COASTER.** Chassis namba: **HZB500001191.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **RUV/MBI/RB /397516/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DEO KRISTIAN MAPUNDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T 339 AWG – SANLG SL125.** Chassis namba: **LBRSPJB5889003038.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /578/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KLETUS EDMUNDI NINDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T 514 CBX – SANLG SL1255.** Chassis namba: **LBRSPJB59C9009245.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /5218/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUNNA HEMED KYUNGU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 573 AGZ – TOYOTA RAV4.** Chassis namba: **SXA117041633.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /5778/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHARI RAMADHANI MASHOKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 113 DKB – TOYOTA IST.** Chassis namba: **NCP600098708.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /5778/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROMANUS NESFORT DUWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 690 DKF – MAZDA BONGO.** Chassis namba: **SSKF2T103847.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /4889/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MASSOUD SULEIMAN KHAMISI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 149 BMF – TOYOTA SPACIO.** Chassis namba: **ZZE1223031341.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /5778/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MADAI Na. 41/2022**

**ELIAS CHIJA NTAGANDA:.....MDAI**
**DHIDI YA**
**SELEMAN TOMSON KANYONZA:... 1. MDAIWA**
**LITE MWANKENE..............2. MDAIWA**

**WIYO/KUITWA SHAURINI**

**SELEMAN TOMSON KANYONZA**
**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 31/10/2022 saa 2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.
Endapo hutafika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutelewa uamuzi.
Imesainiwa leo tarehe 12 Mwezi 10 Mwaka 2022

E. B. USHACKY
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MOROGORO.

---

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 111 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late**
**MICHAEL CHARLES MGOMBELA**

**By 1. CHARLES YORAM MGOMBELA**
**2. .................................**

All Person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the 26th day of October/2022.
Dated at Morogoro, this 13rd day of OCTOBER 2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA**
**LILILOPO MASWA**
**MAOMBI MAKUBWA NA. 37 YA MWAKA 2022**
**KATI YA**
**DOTTO NHANDI...................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**BUSIGA MASANJA, MBILIZI MACHEMBA, MBOJE KIDAKO, CHONA MAYOLWA, NG'HUMBU SAGADI (MRS MALONGO MASUKE), SAYI NYABUDIMA, HAMISI NHANDI**
**WITO/TAARIFA**
**KWA: SAYI NYABUDIMA NA HAMISI NHANDI – POPOTE MLIPO KATIKA JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi dhidi yenu na wenzako katika Baraza hili la Wilaya ya Maswa, maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani. Mnatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wenu wa maandishi (WSD) kabla ya tarehe 27.10.2022. Pia mnajulishwa kuwa shauri hili limepangwa kutajwa siku ya tarehe 27.10.2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe. J.T. KAARE Mwenyekiti, Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Maswa. Na pia mnafahamishwa kuwa iwapo mtakaidi wito huu na kushindwa kutoa utetezi wa maandishi kwa muda uliopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza shauri hili upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yenu.
**IMETOLEWA** kwa **MKONO** wangu na MHURI wa Baraza hii leo tarehe 28.09.2022.

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA

---

**FOMU YA MIRATHI 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO**
**Kituo cha MOROGORO Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 72/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ANNA AFWILILE KALINGA wa MWERE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA FRANCO JIMMY MWAKISOPILE**

**TANGAZO**

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Majhakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19/ Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 11/ mwezi 10 mwaka 2022**

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# WEMA ATISHIA KUJIUA AKIACHWA

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa kike wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, amesema akiachwa na msanii wa Bongo Fleva, Whozu basi watu wakaribie msibani kwa ajili ya kumzika.

Wema ambaye yupo kwenye penzi motomoto na Whozu huku wakituma picha kila wakati kwenye mtandao wakiwa pamoja na kula raha sehemu mbalimbali, amesema hawezi kuishi bila penzi hilo.

Wema kupitia ukurasa wake wa Instagram amesema pamoja na kwamba hakujiua kwenye uhusiano wake wa kimapenzi huko nyuma likiwemo penzi la msanii Diamond Platnumz na wengineo, lakini safari hii akiachwa na Whozu, atakuwa kama MC Joas aliyekuwa Katibu wa Kanisa la Feel Free Church la Masanja Mkandamizaji ambaye alidaiwa kujinyonga hivi karibuni, kisa kikidaiwa ni kukataliwa penzi na mke wa Masanja.

Wema amesema kuwa, kama akiachwa na Whozu, basi watu wakaribie msibani kwa ajili ya kumzika kwa sababu jamaa huyo amemheshimisha mno.

Penzi la Wema na Whozu limechipuka kipindi cha hivi karibuni na limeanza kuteka mazungumzo mtandaoni.

Wema anasema kuwa, pamoja na kwamba watu wanambeza, lakini anataka aachwe na maisha yake kwani ukweli ni kwamba amezama kabisa kwenye dimbwi la mahaba na ana furaha mno.

# ARIANA, TOM WAKANUSHA KUACHANA

**NEW YORK CITY, Marekani**

MASTAA wa kipindi cha televisheni cha maisha halisi cha 'Vanderpump Rules' cha Marekani, Ariana Madix na Tom Sandoval, ambao ni wapenzi, wamekanusha uvumi kwamba wameachana.

Wakizindua msimu wa 10 wa kipindi hicho Jumamosi iliyopita, ambacho kimetokana na kile cha miaka 1990 cha 'The Real Housewives of Beverly Hills', walibainisha kuwa wao bado wako pamoja.

Ariana mwenye umri wa miaka 37, aliiambia Us Weekly, Jumamosi, kwamba, yeye na Tom mwenye umri wa miaka 39, wako "sawa" licha ya tetesi kuzagaa kuwa wametemana baada ya kuwa pamoja kwa zaidi ya miaka nane.

Uhusiano wa mapenzi wa nyota hao ulianza wakati wa upigaji picha wa msimu wa pili wa kipindi hicho.

"Unajua ni nini cha kuchekesha? Nilikuwa nikimwambia mtu mwingine tu, mimi sizingatii sana yale yanayosemwa kwenye mitandao, nakuwa kama kipofu sitaki kuona," alisema Ariana katika uzinduzi huo wa msimu wa 10 wa kipindi hicho pale jijini New York.

Aidha, Tom alisema bado wanaendelea kuimarika. "Sisi ni bora. Tunafanya vizuri sana, na nimeona vichwa vya habari kuhusu madai ya kuachana kwa miaka."

Tom alisisitiza kwamba, hawana mchezo wa kuigiza kwenye mahusiano yao na kwamba msimu wa 10 wa Vanderpump Rules utaangazia mapenzi mengi tofauti na utakuwa na burudani za kutosha.

"Sisi bado tupo sana pamoja na sioni namna tunaweza kuachana hivi karibuni, hayo mambo ya kwenye mitandao yaacheni huo huko," aliongeza Ariana.

# DIAMOND: SIWEZI KUMUOA ZUCHU

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz amesema kwamba, hawezi kumuoa msanii mwenzake, Zuchu.

Mmiliki huyo wa Lebo ya Wasafi Classic Baby (WCB), amekuwa akitajwa kuwa kwenye penzi zito na msanii wake, Zuchu ambaye jina lake halisi ni Zuhura Othman.

Msimamo wa Diamond umekuja baada ya kauli ya mmoja wa mameneja wake, Babu Tale kumwambia aoe kufuatia kuposti video akibusiana mdomoni na Zuchu.

Ikumbukwe kuwa, kwa muda mrefu kumekuwa na tetesi kuwa, Diamond na Zuchu ni wapenzi kutokana na ishara za mahaba wanazozionyesha, lakini amesema kwamba, hawezi kumuoa mrembo huyo kwa sababu ni msanii wake.

"Sasa nitamuoaje wakati ni msanii wangu bosi, hilo busu hapo lisiwatishe viongozi, ni salamu tu za Kijerumani," aliandika Diamond kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Diamond na Zuchu wametoa pamoja ngoma tatu ambazo ni Litawachoma, Cheche na Mtasubiri, huku wakidaiwa kuwa ni wapenzi.

# DSTV YAJA NA OFA IKITENGA CHANELI KOMBE LA DUNIA

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha wateja wake wanapata burudani murua kabisa bila kero, DStv kupitia chaneli zake za SuperSport imetenga chaneli mahsusi kwa ajili ya michuano ya Kombe la Dunia 2022 inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Novemba 20 hadi Desemba 18, mwaka huu huko nchini Qatar.

Kutengwa kwa chaneli hizo kutawawezesha watazamaji wa DStv kuona mechi hata zile ambazo zitachezwa kwa wakati mmoja.

Hatua hii inatokana na SuperSport kupata haki hodhi za kuonyesha mechi zote 64 za michuano hiyo katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania.

Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, aliliambia Nipashe jijini Dar es Salaam jana kuwa ni wateja wa DStv pekee ndiyo wataweza kushuhudia mechi zote 64 za michuano hiyo mubashara kupitia chaneli za SuperSport. "SuperSport wamepata haki za kuonyesha michezo yote ya michuano hiyo na ili kuhakikisha kuwa wateja wetu hawapati usumbufu, zimetengwa chaneli mbili mahususi kwa ajili ya michuano hiyo ambapo chaneli hizo muda wote zitakuwa zikionyesha matukio mbalimbali yanayohusiana na mashindano hayo ikiwamo uchambuzi wa wataalamu wa soka, makala za matukio muhimu katika mashindano yaliyopita pamoja na kurusha mubashara mechi zote," alisema Shelukindo na kuzitaja chaneli hizo kuwa ni Fifa World Cup Central na Fifa World Cup Africa.

Ametaja mechi zitakazoonekana mubashara ndani ya SuperSport kuwa ni zote 48 za hatua ya makundi, nane za hatua ya 16-bora, nne za robo fainali, mbili za nusu fainali, mechi ya kutafuta mshindi wa tatu na ile ya fainali.

Mbali na kuonyesha mechi hizo mubashara, Shelukindo alisema pia zitatangazwa na kuchambuliwa kwa kiswahili na watangazaji na wachambuzi nguli wa soka hapa nchini. "Tunafurahi kuwa kwa mara ya kwanza kabisa, sasa tutaweza kufuatilia michuano hii kwa lugha yetu ya kiswahili kwani tuna timu ya watangazaji mahiri wa kiswahili watakaowaletea watazamaji wetu wa DStv mitanange hiyo kwa lugha yetu adhimu ya kiswahili."

Ili kuhakikisha kuwa Watanzania hawapitwi na uhondo wa michuano hiyo ya Kombe la Dunia, DStv inatoa ofa kabambe kwa wale wanaotaka kujiunga kwani ofa maalum ya msimu huu ni Sh. 79,000 tu kwa seti nzima ya DStv pamoja na kifurushi cha DStv Compact, ambacho kitaonyesha mechi zote mubashara.

"Ofa hii ni mahsusi kwa msimu huu ili kuwawezesha Watanzania wengi kushuhudia michuano hii ambayo ndiyo mikubwa ya soka ulimwenguni," alisema Shelukindo na kuongeza kuwa wameamua kutoa ofa ya kifurushi cha Compact kwa wateja wapya kwani kifurushi hicho kitaonyesha mechi zote 64 za michuano hiyo.

Hata hivyo, amesema wateja wote wa DStv watapata burudani ya michuano hiyo kwani hata kwenye vifurushi vya DStv Shangwe cha Sh. 10,000 DStv Bomba cha Sh. 23,000 na DStv Shangwe cha Sh. 34,000 nao watashuhudia baadhi ya mechi za mashindano hayo mubashara.

## Polisi yaona mwezi Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Polisi SC imepata ushindi wake wa kwanza tangu kuanza Ligi Kuu Zanzibar msimu huu wa 2022-2023.

Polisi SC imeonja ushindi huo baada ya juzi kuwachapa Maafande wa JKU bao 1-0 katika kukamilisha mzunguko wa saba wa Ligi Kuu hiyo huku bao hilo pekee likiwekwa nyavuni na Haji Haji dakika ya 39.

Kwa matokeo hayo sasa Polisi inafikisha pointi sita baada ya kushuka dimbani mara saba ikishinda mchezo mmoja, sare tatu na kafungwa mitatu, hivyo kushika nafasi ya 13 kati ya timu 16 zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Mtuli, alisema ana matumaini kuwa hata mchezo wa nane watafanya vizuri kwa kuwa wanahitaji kushinda ili kuwa salama.

Alisema kuanza vibaya kwenye ligi hiyo haimaanishi kuwa wachezaji hawajitumi, bali ni mabadiliko na ushindani mkubwa msimu huu.

Mtuli alisema wanaendelea kuiboresha timu hiyo kwa kuyafanyia kazi mapungufu yote yanayojitokeza ili kuhakikisha timu yao inabaki Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

"Kila timu ina lengo la kufanya vizuri katika mzunguko huu wa kwanza kabla ya kwenda dirisha dogo, lakini kama ukiwaza vibaya kumaliza kunakuwa kugumu zaidi kwa sababu kila timu inafanya usajili mdogo kulingana na mapungufu iliyoyaona mwanzoni. Hivyo na sisi tunajitahidi kuhakikisha michezo nane iliyobakia kabla ya kwenda dirisha dogo tunapata matokeo mazuri ili tuiweke timu sehemu salama.

Timu ya Polisi itashuka tena dimbani Ijumaa wiki hii kucheza mchezo wao wa nane, ambapo itakuwa na shughuli pevu dhidi ya Wanajeshi wa Kipanga katika

MITINDO...



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya St Mary's Mbezi Beach, wakionyesha mitindo ya mavazi kwenye mahafali ya kidato cha nne ya shule hiyo, yaliyofanyika mwishoni mwa wiki shuleni hapo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kocha Simba Queens aona mwanga CAF

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukulu, amesema mechi mbili za kirafiki alizocheza zimemsaidia kupata mwanga wa kikosi chake kuelekea katika michuano ya LigI ya Mabingwa Afrika.

Simba Queens imeshacheza mechi mbili dhidi ya Baobab Queens na Ceasia Queens FC kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea kwenye michuano hiyo inayotarajiwa kutimua vumbi Oktoba 30, mwaka huu nchini Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Lukulu alisema ameona mapungufu na ubora wa kikosi chake na kufanyia kazi kwenye mapungufu na kujiimarisha zaidi kuwa kikosi imara.

Alisema malengo makubwa kuelekea michuano hiyo ni kuhakikisha wanafanya kweli kwa kwenda kushinda na kuuwakilisha vema Ukanda wa CECAFA.

"Ni kweli tunaenda kwenye michuano hiyo kukutana na timu nzuri, inamaana tunahitaji kujiandaa vizuri kuhakikisha tunaenda kushinda na kufikia malengo yetu," alisema Lukulu.

Alisema anaamini viwango vya wachezaji aliona na wanaweza kuwafikisha katika malengo ya kufanya vizuri katika michuano hiyo ambayo ni mara yao ya kwanza kushiriki.

Simba Queens inatarajia kuondoka nchini Oktoba 25, mwaka huu na watakuwa na kibarua katika mchezo wa kwanza dhidi ya ASFAR utakaopigwa Oktoba 30, mwaka huu nchini humo.

Kikosi cha Simba Queens ambacho kinauwakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati katika michuano hiyo itakayoanza Oktoba 30 hadi Novemba 13, mwaka huu nchini Morocco, kipo Kundi A na timu ya ASFAR (Morocco), Green Buffaloes (Zambia) na Determines Girls ya Liberia.

Kundi B linaundwa na mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Bayelsa Queens ya Nigeria, Wadi Degla ya Misri na mwakilishi wa Ukanda wa UNIFFAC.

## ZISIKUPITE

### RICE AKATAA MKATABA
KIUNGO wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23, hana mpango wa kusaini mkataba mpya na West Ham msimu huu, licha ya kupewa ofa ya miaka nane na mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki. ***(Football Insider)***

### SALIBA AWINDWA NA PSG
MLINZI wa Arsenal na Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 21, anaivutia Paris St-Germain. ***(CBS Sport, via Sun)***

### NEWCASTLE YAMTAKA BRUNO
KLABU ya Newcastle United inaandaa ofa itakayoweka rekodi ya Klabu kwa kiungo wa Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 24 na mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki. ***(Football Insider)***

### TROSSARD ANYATIWA ATLETICO
KLABU ya Atletico Madrid inatarajiwa kupambana na Chelsea kuwania saini ya fowadi wa Brighton na Ubelgiji, Leandro Trossard, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, mkataba wake wa sasa ukimalizika msimu ujao wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### EVERTON NA GORDON
MAZUNGUMZO ya Everton na winga wa England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21, yamesimama, huku mchezaji huyo akitaka mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. ***(Sun)***

### LEAO KATUMIWA MASKAUTI
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, alituma maskauti kwenda kumwangalia fowadi wa Ureno, Rafael Leao wakati AC Milan ikicheza na Chelsea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne. Chelsea na Manchester City pia zimekuwa zikimwinda mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye thamani yake inatajwa kuwa pauni milioni 60. ***(Mirror)***

### NKUNKU AWINDWA VIKALI
LIVERPOOL wametuma maskauti kumwangalia fowadi wa RB Leipzig na Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia anawaniwa na Chelsea. ***(Sun)***

### MARTINEZ KWA UNITED, PSG
MANCHESTER United na Paris St-Germain zimemuulizia straika wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 25. ***(Gazzetta dello Sport, via Mail)***

### JONG AFUNGUKA BARCA
KIUNGO wa Uholanzi, Frenkie de Jong amesema Barcelona walimpa presha kubwa ili aondoke klabuni hapo, huku Manchester United ikijaribu kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kipindi cha majira ya joto. ***(Ziggo Sport, via Mail)***

### TRAORE NA MKATABA
STEVEN Gerrard ameiambia Klabu ya Aston Villa kukubali ofa ya kumsajili kwa mkataba wa kudumu Januari winga wa Burkina Faso, Bertrand Traore mwenye umri wa miaka 27, ambaye anacheza kwa mkopo katika Klabu ya Uturuki ya Istanbul Basaksehir. ***(Football Insider)***

### TOTTENHAM YAMFUATA CIRKIN
KLABU ya Brentford inatarajia kushindana na Hotspur kwenye mbio za kumwania mlinzi wa kushoto wa Sunderland, Dennis Cirkin mwenye umri wa miaka 20. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN AFIKISHA MABAO 100 LALIGA

●●●Awali, Morata alinyimwa bao la kwanza na VAR, na walipata penalti ambayo nayo....

**MADRID, Hispania**

ANTOINE Griezmann aliifungia Atletico Madrid bao kwenye ushindi muhimu wa 1-0 dhidi ya Athletic Bilbao, Jumamosi na kufikisha mabao 100 aliyoifungia klabu hiyo kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Atletico ilitangaza Jumatatu kwamba Griezmann amesajiliwa kwa mkataba wa kudumu baada ya kucheza hapo kwa mkopo kutoka Barcelona, na fowadi huyo wa Ufaransa alicheza mechi yake ya kwanza ya ligi baada ya kumaliza kipindi cha pili.

Awali, Alvaro Morata alinyimwa bao la kwanza na VAR, lakini juhudi za Griezmann zilitosha kwa vijana wa kocha Diego Simeone kuweza kupata ushindi huo.

Atletico walipata penalti, lakini VAR ikaikataa. Ushindi huo unaifanya Atletico kuwaruka wenyeji wao hao hadi nafasi ya tatu ya msimamo wa LaLiga, wakiwa nyuma ya Barcelona na Real Madrid kwa pointi tatu ambao jana Jumapili walikuwa wanakutana kwenye mchezo wa Clasico.

Morata alionekana kutumia nafasi ya kuteleza kwa Yeray Alvarez na kuupata mpira kabla ya kumfunga golikipa Unai Simon, lakini baada ya mwamuzi kutazama marudio ilionekana kwamba, mshambuliaji huyo wa Hispania alifanya faulo.

Vijana hao wa Simeone walishindwa kuandikisha shuti hata moja kati ya bao lililokataliwa la Morata hadi kipindi cha mapumziko.

Lakini walipata bao lao ndani ya dakika mbili za mchezo huo kipindi cha pili, wakati Griezmann alipotumia vizuri pasi ya kisigino ya Morata na kufunga kwenye kona ya chini kulia.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS.374,

MECHI KALI
TANZANIA PRISONS
VERSUS
COASTAL UNION
1 | 2.35
X | 2.70
2 | 3.65

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JAMES HATIHATI KUKOSA KOMBE LA DUNIA QATAR

**LONDON, England**

MLINZI wa England, Reece James anaonekana anaweza asishiriki Kombe la Dunia mwaka huu nchini Qatar, huku Chelsea ikithibitisha kuwa anatarajiwa kuwa nje kwa angalau wiki nane kutokana na jeraha la goti.

Beki huyo wa kulia mwenye umri wa miaka 22, ambaye amecheza mechi 15, alipata jeraha katika ushindi wa mabao 2-0 wa Chelsea dhidi ya AC Milan kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Michuano ya Kombe la Dunia itaanza baada ya wiki tano tu kutoka sasa, Novemba 20, nchini Qatar.

Mabeki wenzake wa kulia wa England, Kyle Walker na Trent Alexander-Arnold kwa sasa wako nje kutokana na majeraha pia.

Walker wa Manchester City alifanyiwa upasuaji wa paja mapema Oktoba, huku Alexander-Arnold wa Liverpool akipata jeraha la kifundo cha mguu wakati wa mchezo dhidi ya Arsenal wiki moja iliyopita.

Walker inadaiwa anaweza kuwa fiti kwa wakati kwa Kombe la Dunia. Kieran Trippier wa Newcastle ndiye chaguo jingine kali katika nafasi hiyo.

Chelsea ilithibitisha kuwa James alipata matibabu kutoka kwenye klabu hiyo na alifanyiwa uchunguzi wa kitaalamu zaidi mwishoni mwa wiki.

"Baada ya mashauriano kati ya pande zote, Reece sasa atapitia programu maalum na anatarajiwa kuwa nje kwa wiki nane," taarifa ya klabu ilisema.

Na baada ya ushindi wao dhidi ya AC Milan, kocha wa Chelsea, Graham Potter aliulizwa kuhusu wachezaji ambao wanaweza kukosa Kombe la Dunia kutokana na majeraha.

"Ikitokea kitu kama hicho, watakatishwa tamaa. Ni binadamu na wanataka kwenda," alisema.

"Wanajua pia ni taaluma ambayo mambo yanaweza kutokea na wanashindana kwa kiwango cha juu na huwezi kukwepa jambo hili wakati mwingine."



# De Gea ataka kubaki miaka mingi Man Utd


**MANCHESTER, England**

DAVID de Gea ameelezea nia yake ya kutaka kubakia Manchester United kwa "miaka mingi zaidi" kabla ya mkataba wake kumalizika mwaka 2023.

De Gea jana Jumapili alitarajiwa kufikisha mechi yake ya 500 wakati 'Mashetani Wekundu' walipokuwa wanakutana na Newcastle United Uwanja wa Old Trafford Jumapili, na kuwa mchezaji wa 11 kuichezea United idadi hiyo ya mechi katika historia ya Klabu.

Ni Ryan Giggs, Sir Bobby Charlton, Paul Scholes, Bill Foulkes, Gary Neville, Wayne Rooney, Alex Stepney, Tony Dunne, Denis Irwin na Joe Spence ndio wamefikia idadi ya kucheza mechi 500 kwa United.

Hata hivyo, mustakabali wa muda mrefu wa De Gea katika klabu hiyo hauna uhakika kwani mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania unamalizika 2023 na bado hajakubali masharti mapya.



De Gea anatumaini kuwa na nafasi ya kucheza mechi nyingi zaidi za United, hata hivyo, alisema: "Hii ni klabu yangu na hapa ndipo ninapojisikia vizuri. Ninacheza vizuri, najisikia vizuri sana.

"Nadhani nina miaka mingi zaidi ya kucheza. Najiamini.

"Ndiyo, ningependa kukaa hapa kwa miaka zaidi na kutengeneza rekodi za michezo na rekodi za kila kitu. Ili kujaribu kuwasaidia vijana wa hapa pia kwa uzoefu wangu na kujaribu kushinda makombe."

De Gea atafikisha umri wa miaka 32 mwezi ujao na tayari ametumia miaka 11 kama golikipa namba moja wa United, lakini anaamini kuwa sasa anaingia kwenye ubora wake.

Alipoulizwa kama alifikiri anaingia katika miaka yake ya kilele, De Gea alisema: "Ninajisikia vizuri sana katika michezo na mazoezi. Bila shaka, kwa uzoefu zaidi unajisikia vizuri sana. Kwa hiyo, ndiyo, nadhani hivyo.

"Ninajisikia vizuri na ninataka kucheza miaka zaidi, na muhimu zaidi ni kujaribu kushinda mataji na kusaidia timu, kama ninavyojaribu kufanya kila siku."

## HABARI MICHEZO


,935,160

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/10/22 | 20:00 | Cadiz CF vs Betis | 2.85 | 3.25 | 2.43 |
| 02. 19/10/22 | 20:00 | Valladolid vs Celta Vigo | 2.47 | 3.19 | 2.85 |
| 03. 19/10/22 | 20:00 | AIK Football vs BK Hacken | 2.39 | 3.40 | 2.58 |
| 04. 19/10/22 | 21:30 | Bournemouth vs Southampton | 2.72 | 3.27 | 2.46 |
| 05. 19/10/22 | 21:30 | FC Luzern vs St. Gallen | 2.50 | 3.55 | 2.55 |
| 06. 19/10/22 | 21:45 | Wigan vs Middlesbrough | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 07. 19/10/22 | 21:45 | Mechelen vs Standard Liege | 2.54 | 3.39 | 2.59 |
| 08. 19/10/22 | 22:00 | Millwall vs Watford | 2.71 | 3.20 | 2.51 |
| 09. 19/10/22 | 22:15 | Manchester Utd vs Tottenham | 2.23 | 3.42 | 2.94 |
| 10. 20/10/22 | 20:00 | Almeria vs Girona | 2.35 | 3.20 | 3.00 |
| 11. 20/10/22 | 20:00 | Degerfors vs IFK Goteborg | 2.73 | 3.32 | 2.31 |
| 12. 20/10/22 | 21:00 | Osasuna vs Espanyol | 2.22 | 3.20 | 3.25 |
| 13. 20/10/22 | 21:30 | Fulham vs Aston Villa | 2.77 | 3.22 | 2.45 |

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 17/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3197 | Benfica U23 vs Estoril Praia U23 | 1.70 | 3.75 | 4.10 |
| 15:30 | 3795 | Inter Youth vs Sassuolo Youth | 1.97 | 3.65 | 3.50 |
| 16:00 | 3992 | KF Erzeni vs Kukesi | 2.31 | 3.10 | 2.90 |
| 16:00 | 5739 | Tanzania Prisons vs Coastal Union | 2.35 | 2.70 | 3.65 |
| 16:30 | 1059 | Lokomotiv Tashkent vs FC Olimpik | 1.89 | 3.06 | 4.08 |
| 16:30 | 4064 | Ajax Cape Town vs Mm Platinum FC | 2.26 | 2.82 | 3.31 |
| 17:00 | 4010 | Al-Jalil vs Buqaa Amman | 1.68 | 3.55 | 4.47 |
| 17:00 | 5941 | Al Ahli Amman vs Sama AL Sarhan | 2.33 | 3.11 | 2.86 |
| 18:00 | 2467 | FK Ekranas vs FK Babrungas Plunge | 1.99 | 3.75 | 3.02 |
| 18:00 | 5850 | Pyunik Yerevan vs Ararat Armenia | 2.67 | 2.86 | 2.67 |
| 18:15 | 3318 | AL Akhdood vs AL Ain | 2.26 | 2.82 | 3.30 |
| 18:15 | 5524 | FC Otelul Galati vs Concordia Chiajna | 2.02 | 3.21 | 3.40 |
| 18:30 | 3386 | SOL FC vs Racing Club Dabidjan | 2.90 | 2.85 | 2.65 |
| 19:00 | 1625 | Raufoss vs Kfum Oslo | 2.81 | 3.49 | 2.18 |
| 19:00 | 2640 | Stjordals-Blink vs Fredrikstad | 3.75 | 3.85 | 1.74 |
| 19:00 | 3030 | Kongsvinger IL vs Sandnes Ulf | 1.87 | 3.75 | 3.36 |
| 19:00 | 3072 | FC Elva vs Parnu Jalgpalliklubi | 1.19 | 6.80 | 12.01 |
| 19:00 | 3300 | Brann vs Skeid Fotball | 1.03 | 10.64 | 25.15 |
| 19:00 | 3489 | AEK Larnaca vs Olympiakos Nicosia | 1.48 | 4.18 | 6.37 |
| 19:00 | 4078 | Omonia Nicosia vs Nea Salamis | 1.49 | 4.10 | 6.41 |
| 19:00 | 5195 | Vmfd Zalgiris-3 vs FM Auska Alytaus | 5.61 | 5.03 | 1.38 |
| 19:00 | 5805 | Apollon Limassol vs Aris Limassol | 2.09 | 3.40 | 3.35 |
| 19:30 | 4109 | Sampdoria vs Roma | 4.66 | 3.62 | 1.70 |
| 19:30 | 4345 | Maccabi Netanya vs Hapoel Katamon | 1.94 | 3.40 | 3.45 |
| 19:55 | 3101 | Jeddah Club vs Hajer Club | 3.21 | 2.77 | 2.34 |
| 20:00 | 1324 | Landskrona Bois vs Vasteras SK | 2.47 | 3.39 | 2.78 |
| 20:00 | 1660 | Arsenal Sarandi vs Barracas Central | 2.10 | 3.07 | 3.36 |
| 20:00 | 1958 | Wehen vs VfB Oldenburg | 1.50 | 4.26 | 5.54 |
| 20:00 | 2187 | Utsiktens BK vs Halmstads BK | 3.34 | 3.59 | 2.07 |
| 20:00 | 2509 | Olympiakos vs PAOK | 1.68 | 3.39 | 5.38 |
| 20:00 | 2927 | Sivasspor vs Giresunspor | 2.05 | 3.33 | 3.48 |
| 20:00 | 4018 | Trelleborgs FF vs Orebro SK | 2.19 | 3.53 | 3.13 |
| 20:00 | 4184 | Silkeborg vs Randers | 1.81 | 3.69 | 3.99 |
| 20:00 | 4883 | Ankaragucu vs Fenerbahce | 4.59 | 3.84 | 1.68 |
| 20:00 | 5169 | Hapoel Beer Sheva vs Sectzya Nes Ziona | 1.29 | 4.86 | 8.35 |
| 20:10 | 3515 | IFK Goteborg vs Malmo | 3.70 | 3.60 | 1.81 |
| 20:30 | 1573 | FC Trollhattan vs Lindome Gif | 1.51 | 4.17 | 5.04 |
| 20:30 | 2252 | Maccabi Haifa vs Hapoel Hadera | 1.16 | 6.21 | 13.59 |
| 21:00 | 2621 | CFR Cluj vs Sepsi Osk | 2.06 | 3.12 | 3.66 |
| 21:15 | 1134 | FC Thun vs Yverdon-Sport FC | 1.94 | 3.74 | 3.15 |
| 21:15 | 5116 | Neuchatel Xamax vs FC Schaffhausen | 2.32 | 3.31 | 2.72 |
| 21:30 | 3088 | Mantova vs Pordenone | 3.95 | 3.20 | 1.98 |
| 21:45 | 4096 | Bastia vs Bordeaux | 2.77 | 3.02 | 2.57 |
| 21:45 | 4860 | Lecce vs Fiorentina | 3.56 | 3.27 | 2.03 |
| 22:00 | 4115 | Sporting Gijon vs Eibar | 2.77 | 2.97 | 2.62 |
| 22:00 | 4393 | Charlton vs Portsmouth | 2.53 | 3.28 | 2.63 |
| 22:00 | 5823 | Villarreal vs Osasuna | 1.60 | 3.95 | 5.20 |
| 22:30 | 5725 | Velez Sarsfield vs Estudiantes LP | 2.08 | 3.07 | 3.41 |
| 23:30 | 1198 | Envigado FC vs Junior Barranquilla | 3.46 | 2.92 | 2.13 |
| 23:30 | 4563 | Mvo Wanderers vs Plaza Colonia CD | 2.24 | 3.02 | 3.11 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MSIMU WA 4 GOBA HILLS MARATHON WAZINDULIWA

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya GOBA Road Runners (GRR), imetangaza mbio zake ziitwazo Goba Hills Marathon, zilizopangwa kufanyika Januari 28, mwakani katika viwanja vya Shule ya Sekondari Goba.

Huo utakuwa ni msimu wa nne wa mbio hizo zinazokadiriwa kushirikisha zaidi ya wanariadha 2,000 kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo Dar es Salaam jana, ilieleza kuwa wanariadha wataokimbia watatumia uwanda mzuri wa barabara za vilima vya Goba na viunga vyake.

"GRR inatangaza rasmi uandikishwaji wa kushiriki mbio hizo ulioanza tangu Oktoba 14, 2022, siku ya Kukumbuka Kifo cha Baba wa Taifa, Hayati Mwl. Julius Nyerere," ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Iliongeza kuwa kutakuwa na mbio za Kilomita 42, Kilomita 21.1, Kilomita 10 na Kilomita tano huku ikitaja ada ya kujiandikisha ni Sh. 35,000 na pia inazialika klabu nyingine mbalimbali za taasisi na jamii nzima ya wakimbiaji.

Ilieleza malengo makuu ya mbio hizo ni kuokoa maisha ya mama na mtoto ambapo kwa miaka mitatu iliyopita wamekuwa wakisaidia zahanati (kituo) ya Goba kwa kuelekeza asilimia 10 ya mapato ya mbio hizo.

"Klabu inawaalika wadau na washirika kuja kudhamini mbio hizi. Waandaji wanatoa rai kwa wadau wote kujiandikisha mapema kwa sababu nafasi za ushiriki ni chache," iliongeza taarifa hiyo.

Ilieleza kuwa malipo ya ada ya ushiriki yanatakiwa kufanyika kupitia namba ya Mpesa Lipa Namba 5550800 na Tigo Pesa Lipa Namba 8403615 jina Goba Roads Runners, halafu taarifa za jina, umbali utakaokimbia na 'saizi' ya T-shirt zitumwe kwa Johnson Mbunda +255715616374.

## KIKAZI ZAIDI...



Brigedia Jenerali, Suleiman Gwaya (katikati), akizungumza na Kanali Dorah Kaita kutoka Guinea ambaye ni Katibu Mkuu Mstaafu wa Michezo ya Majeshi duniani (CISM), pia ni Mwambata wa Jeshi la nchi hiyo nchini Ubelgiji, kwa sasa ni Balozi wa CISM aliyekuwapo nchini kwa ziara ya kikazi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Michezo ya CISM na nchini BAMATA, Kanali Joseph Bakari. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Samia aipongeza Serengeti Girls

INATOKA UK. 32

Kutokana na ushindi huo, Tanzania inakamata nafasi ya pili kwenye Kundi D, ikiwa na pointi tatu na hii ni baada ya Japan kuwakung'uta Canada mabao 4-0 kwenye mechi nyingine ya kundi hilo iliyochezwa juzi.

Wakati Japan ikiwa na pointi sita, Tanzania ina pointi tatu, huku Canada na Ufaransa zote zikiwa na pointi moja moja.

Tanzania inahitaji ushindi tu kwenye mechi ya kesho dhidi ya Canada kuweza kutinga hatua ya robo fainali.

## Simba yatinga makundi Afrika

INATOKA UK. 32

wapinzani wao kumiliki zaidi, lakini tatizo lilikuwa ni kuuvuka ukuta wa Simba uliokuwa unaongozwa na Inonga, chini ya Aishi Manula.

Shambulizi pekee la hatari la Agosto lilifanywa dakika ya 55 wakati krosi iliyopigwa na Manuel Londaka, ulimkuta Zidane Cotraio aliyeruka tik-tak, lakini mpira ukatoka nje ya lango.

Kocha Juma Mgunda aliwatoa Okrah aliyeumia, Pape Sakho, Tshabalala na kuwaingiza Kibu Denis, Gadiel Michael, na Habib Kyombo ambao walionekana zaidi kuingizwa kwenye kukaba maeneo na si kushambulia zaidi hadi pale mwamuzi kutoka Afrika Kusini, Abongile Tom alipopuliza kipenga cha kumaliza mechi, kilichoashiria kuwa Simba kutinga hatua ya makundi baada ya msimu uliopita kushindwa kufanya hivyo ilipotolewa na Jwaneng Galaxy ya Botswana.

De Agosto washangaa uwanja kujaza Maofisa wa Primeiro de Agosto walionekana kushangazwa kuona mashabiki wa Simba wamejitokeza kwa wingi na kujaza uwanja mapema ikiwa saa 8:30 tayari nusu ya uwanja umejaa huku zikisalia sehemu ndogo kujaza uwanja.

Hadi saa 9:40, tayari uwanja ulikuwa umebakiza mapengo machache, kwani zaidi ya asilimia 90 mashabiki walikuwa wameshaingia uwanjani.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 17, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Griezmann afikisha mabao 100 LaLiga

MWENDO WA SALUTI...



Moses Phiri (katikati) akishangilia kwa staili ya saluti na wachezaji wenzake wa Simba, Pape Sakho (kushoto) na Clatous Chama, baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: SIMBA**

# *Simba yatinga makundi Afrika*

●●●Phiri aendelea kuandika rekodi ya mabao, maofisa wa De Agosto washangaa mashabiki kufurika kwa Mkapa huku...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAO lililofungwa na Mzambia Moses Phiri liliwafanya wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Simba kushinda 1-0 dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kutinga hatua ya makundi ya ligi hiyo.

Simba inatinga hatua hiyo kwa jumla ya mabao 4-1 kutokana na mechi ya kwanza iliyochezwa Oktoba 9, mwaka huu nchini Angola kushinda 3-1.

Ni bao lililomfanya Phiri kupachika mabao matano tangu kwenye mechi za awali, pia akifunga mabao katika mechi zote nne ambazo timu yake imecheza.

Kwenye mechi ya ugenini dhidi ya Nyasa Big Bullets alifunga bao moja, akapachika mawili mchezo wa marudiano, na katika mechi ya Raundi ya Kwanza ugenini Angola alifunga moja.

Phiri aliwainua vitini mashabiki wa Simba waliojazana Uwanja wa Benjamin Mkapa dakika ya 32, alipofunga bao kwa shuti kali la mguu wa kulia.

Ilikuwa ni krosi fupi ya Mohamed Hussein 'Tshabalala', ambayo ilimkuta mfungaji akaupokea kwa mguu wa kushoto, akawahadaa mabeki wa Primeiro de Agosto, akageuka ghafla na kuachia shuti la chini kwa mguu mwingine, lililompita kipa, Adilson da Cruz na kutinga wavuni.

Mechi ilianza kwa Simba kukaa nyuma na kuwaacha wageni wao kupasiana hapa na pale, lakini walipoupata mpira walikuwa wakipiga mipira mirefu kwa wachezaji wao wenye mbio kama Pape Sakho na Augustine Okrah.

Hata hivyo, wachezaji waliokuwa wakipiga mipira mirefu mbele walionekana kushindwa kukadiria, hivyo kuifanya kuwa kazi rahisi kwa kipa Cruz ambaye jana ndiye aliyesimama langoni badala ya Sebastiao Colo aliyedaka kwenye mechi iliyopita nchini Angola.

Dakika ya tatu ya mchezo mpira mrefu ulitua miguuni mwa Phiri, lakini wakati akiwa katika harakati za kuwahadaa mabeki wa Primeiro de Agosto, akaanguka mwenyewe chini nje kidogo ya eneo la hatari.

Kona fupi iliyopigwa na Clatous Chama dakika ya 12 ilimkuta Tshabalala ambaye alipiga krosi iliyomkuta Henock Inonga akiwa kwenye nafasi nzuri, lakini mpira wake wa kichwa ulitoka juu la lango.

Tshabalala tena alirudia kama alivyofanya mwanzo, lakini safari hii dakika ya 21, mpira ukamkuta Inonga ambaye alipiga kichwa kiliochokuwa kikiambaa kwenye uso wa lango la wageni, ukakosa muunganishaji baada ya Sadio Kanoute kuchelewa kidogo kufika kwenye tukio.

Kipindi cha pili Simba walionekana kuupozesha mpira na kuwafanya

INAENDELEA UK. 31

## Samia aipongeza Serengeti Girls Kombe la Dunia

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ameipongeza Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17, Serengeti Girls, kwa ushindi ilioupata dhidi ya Ufaransa kwenye fainali za Kombe la Dunia zinazoendelea kupigwa nchini India.

Katika salamu zake za pongezi alizozitoa, Rais Samia aliwataka Watanzania waendelee kuiombea na kuwatia hamasa vijana hao ili waendelee kuipeperusha vema bendera ya Tanzania.

"Hongereni vijana wangu Serengeti Girls kwa ushindi wa mabao 2-1 mlioupata leo (juzi), dhidi ya Ufaransa. Nawaomba Watanzania tuendelee kuwaombea na kuwatia hamasa vijana wetu ili waendelee kuipeperusha vema bendera ya Tanzania katika Kombe la Dunia kwa Wanawake chini ya miaka 17 huko India," aliandika Rais Samia kwenye mtandao wake wa Instagram.

Serengeti Girls ilipata ushindi wake wa kwanza kwenye historia ya soka la Tanzania katika michuano hiyo ikicheza Uwanja wa Fatorda, Goa nchini India kwa mabao ya Diana Mnaly na Christer Buhera.

Ushindi huo ulikuja baada ya kufungwa mabao 4-0 kwenye mechi ya kwanza dhidi ya Mabingwa Watetezi, Japan.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, alisema ushindi huo ni furaha kwa Watanzania wote na umewaweka vizuri kwa ajili ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Tumeshinda, lakini niwapongeze wapinzani wetu jinsi walivyokuja kipindi cha pili, mechi ilikuwa na presha sana, mwisho wa siku tumepata matokeo mazuri, kikubwa ni furaha na umetuweka vizuri kwenye nafasi ya kusonga mbele katika michuano hii," alisema kocha huyo.

Naye Mnaly alisema anamshukuru Mungu kwa kuweka rekodi ya kuwa Mtanzania wa kwanza kwa soka la wanawake kufunga bao kwenye michuano ya Kombe la Dunia, akisema atabaki na kumbukumbu hiyo siku zote, kwani hatarajii tena leo wala kesho kuweka rekodi nyingine inayofanana na hiyo.

"Nawashukuru pia wachezaji wezangu na kocha ambaye aliniona nafaa na kunipanga, hivi si vitu ambavyo vinapangwa, hutokea, ni kwa mpango wa Mungu," alisema.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >